ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.

68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 4 Julai, 2010

(Kikao Kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HAZI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Waziri Kivuli Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika sote hapa wazima, lakini la pili nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kidogo tu katika Wizara ya Biashara, Utalii na Uwekezaji.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kuisoma ilani ya CCM inayozungumzia masuala ya Afya katika aya ya 93 ukurasa wa 112 inasema kwamba afya bora kwa wananchi wote ni miongoni mwa malengo muhimu ya mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964. Lakini katika 93© inasema ni kuimarisha huduma za Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja ili kufikia hadhi ya kiwango cha hospitali ya

rufaa, aidha kiwango cha huduma za hospitali na vituo vyengine vya afya vitaimarishwa.

Mhe. Spika, ilani ni nzuri na tatizo sasa ni utekelezaji sina wasi wasi na Waziri na Naibu Waziri lakini baadhi ya wafanyakazi naamini hawaitaki ilani hii, na kwa maana hiyo wanarudisha nyuma malengo ya serikali hawaitaki kwa sababu moja kubwa Mhe. Spika, humu katika ilani inasema kwamba ni kuimarisha vituo vilivyopo katika miji na vijiji. Tuna masikitiko makubwa sana kwamba pengine lengo la Waziri alilokuwa akilionyesha miaka ya nyuma limeharibiwa na baadhi ya wafanya kazi, hiyo lawama tutambebesha yeye.

Mhe. Mwenyekiti mimi nakuja katika suala la tiba sote tunajua kwamba kwa mujibu wa kitabu hiki kikubwa tiba ni hospitali saba, tano za Unguja, tano za Pemba na mbili za Unguja. Fedha ambazo zimegawiwa Mhe. Spika, ni kitu ambacho kinaonyesha dhahiri kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina ubaguzi wa hali ya juu kabisa na inadhalilisha wananchi wa Pemba na inataka kwa makusudi kuwaua, nitatoa sababu sasa hili hatulikubali hata siku moja na leo nimeshaagizishia *ma - renbut* badala ya buti hizi nilizovaa za kawaida zitakuja.

Mhe. Spika, mfano wa mambo yaliyomo humu kwa mfano hospitali tano za Pemba zimepewa milioni thamanini na tisa nukta saba, kwa hivyo kila hospitali ni shilingi milioni kumi na saba wakati hosptali mbili za Unguja Makunduchi na Kivunge zimepewa kila hospitali moja ni shlingi milioni mia moja na ishiri laki sita na hamsini, sasa kampeni hii sasa sijui inakwenda vipi. Lakini ukitizama madawa hamna katika hospitali za Pemba wakati hospitali za Unguja mbili hizo ni milioni sabiini. Vifaa thamani na mapazia hamna ni ziro wakati hospitali mbili za Unguja ni shilingi milioni kumi na tano.

Mhe. Spika, hapa ndio nikasema hawa madaktari wanaopelekwa Pemba wana kila sababu ya kwamba wasende kwa sababu wakienda kule hakuna mapazia ni magunia au vitenge, hakuna thamani, hakuna fanicha, hakuna chochote. Sasa daktari gani aliyekuwa daktari utakayampa uhamisho wa kwenda Pemba akaenda mimi siwalaumu hao madaktari nawalaumu hawa waliofanya bajeti na hii wamefanya makusudi kwa sababu sioni sababu kwa nini wakafanya hivyo.

Mhe. Spika, tuje kwenye chakula kwa hospitali mbili ni milioni thalathini na sita kwa hivyo kila hospitali moja ni milioni kumi na nane, lakini kwa Pemba hospitali moja milioni saba kwa sababu chakula ni milioni thalathini na tisa sasa ukitizama katika kitabu cha bajeti table namba tatu nukta tano na table namba tano nukta moja, wagonjwa waliolazwa katika hospitali tano za Pemba ni wagonjwa 14,853 kwa mujibu wa tarakimu zao. Wakati Zanzibar wagonjwa waliolazwa kwa hospitali mbili ni 3,195. hii ina maana kwa mujibu wa hesabu

zao walizotuletea kila mmowa wa Unguja anapata shilingi milioni kumi na mbuli elfu mia mbili sitini na saba nukta sita kila mgonjwa.

Wakati mgonjwa wa Pemba anapata shilingi mia mbili na sitini na sita hata chipsi hupati, sasa haya ni maonevu ya kutosha Wizara hii ina ubaguzi wa hali ya juu , wizara hii inataka kuwaua kwa makusudi wananchi wa Pemba na hii hatukubali hata kidogo kama hatujapata majibu sahihi ya kuonyesha kwa nini fedha hizi zikagaiwa hivi na tukapewa sababu ambazo zinatukidhi sisi sote. Mhe. Spika, bajeti ya serikali ya Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii hatuikubali katu abadan, watu watasema kuna makubaliano na nini sasa lakini mimi jukumu langu ni kutoa matatizo kuonyesha matatizo na kupendekeza, lakini isije suala la makubaliano ukaja ukafanya udhalimu namna hii kwa sababu ni udhalimu wa hali ya juu.

Mgonjwa wa Pemba unampa shilingi mia mbili na sitini na sita na mgonjwa wa Unguja unampa shilingi kumi na moja elfu mia mbili na sitini na saba kwa shilingi kumi na moja elfu zaidi haiwezekani, sasa mkinambia wagonjwa wa Makunduchi na Kivunge na wao hawapati chakula basi hawa wanaoshughulika ni wezi, maana yake fedha ziko nyingi na kama hawazipeleki huko itakuwa na wao wanawaibia hawa wagonjwa.

Mhe. Spika, matibabu ya nje nimetizama hapa kila mgonjwa wa Unguja anapata angalau shilingi milioni moja laki mbili kwa mujibu wa tarakimu zao, wakati mgonjwa wa Pemba anapata shilingi mia mbili na arubaini elfu yaani laki mbili na arubaini. Sasa jamani ugawaji huu na ukichukua ilani inasema afya bora kwa wananchi wote, sasa wananchi wote ni pamoja na Unguja na Pemba au mnambie ilani ilikuwa imekosewa hapa ilikuwa wasema afya bora kwa wananchi wote wa Unguja sasa hapo nitakubali, lakini sifikirii kama inaweza kufika hali hiyo.

Mhe. Spika, haya ni maonevu makubwa kwa wananchi wa Pemba na sisi kama ndio wasemaji wao tutatoa kauli ya hali ya juu kabisa kuhusu suala hili na ndio maana wagonjwa wa Pemba wanafariki tu ovyo ovyo kwa kukosa kutibiwa, kwa kukosa kuangaliwa na mifano tunayo naomba nitoe mifano mwili au mitatu.

Hivi juzi karibu miezi miwili au mitatu nyuma shemegi yangu mimi mke wa ndugu yangu alikwenda hospitali ya Wete alipokwenda anasema anaumwa na tumbo, daktari aliyekuwepo kusema anaumwa na tumbo akampa panadol hata kumtizama hakuthubutu sijui kwa sababu alikuwa muislam sana yule daktari mwanamme hawezi angalau kumguza yule mwanamke wala haiji katika *medical ethics.* Akarudi siku ya tatu tumbo limezidi akambadilisha akampa brufeni wanazijua wenyewe, bahati nzuri yule shemeji yangu anakuja huku

kikazi alikuwa akifanya kazi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, anakuja huku alipofika nyumbani akasema nakwenda hospitali alipokwenda akatizamwa akapimwa kumbe ameshapasuka *apendex,* akaambiwa sasa hivi aende upere sheni hata nyumbani usende akapiga simu tu bahati mbaya yule shemeji yangu tukamkosa.

Sasa tumemkosa kwa sababu gani kwanza hakuna vifaa kule Pemba na hakuna kwa sababu ndio hii milioni mia moja na kumi na nne unapeleka millioni thalathini na tisa ni maonevu ya hali ya juu kabisa, akafariki dunia tumeshamkosa mungu amlaze mahali pema peponi amin. Lakini inasababishwa na baadhi ya matatizo yaliyoko katika hospitali za Pemba, sasa tukifika hivi hatutokubaliana na Wizara ya Afya hata kidogo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naomba nielezwe hasa sababu ya kugawa fedha hizi zikawa namna hii ni kwa ajili gani na kwa nini hospitali za Pemba hamkuzifanyia ugawaji ulio sahihi, kuna mifano mingi lakini hiyo nafikiri inatosha kwa suala hili.

Suala jengine ni katika hospitali hii ya Mnazi Mmoja katika hayo hayo masuala ya tiba, kwanza hapa suala hili nilimwambia Mhe. Waziri na Katibu Mkuu bahati mbaya nilisafiri sikuwahi kumpa lakini nilikuwa na ahadi ya kumpa na nitampa nimeshatoa nakla lakini bahati mbaya tu nilikuwa sipo, kuna hizi hospitali zinazofunguliwa ovyo ovyo bodi inayohusika na ukaguzi haifanyi ukaguzi.

Kuna Hospitali iko Kiponda nasikia lakini hata katika hili buku hawakuandika hospitali gani mgonjwa akienda hayo matibabu yanayofanywa ni shilingi milioni moja ili kumtibu yule mgonjwa, hapa nina buku la huyo mgonjwa maradhi aliyoandikiwa mara moja tu wala hakupimwa na wala hakufanywa chochote, anasema *checking body, result internal and external hemorroid, ……. pain,lumbar pain, cervical pain, respiratory system, chest pain, kidneys and lungs pain, heart pain and hypertension, leg and foot problem, arm pain and arteries problem* yote hayo siku moja tu hiyo.

Sasa huyu ni daktari gani mwenye mambo haya bado yanaendelea *blood pressure, loss appetite, cholesterol, shoulder pain and allergic* hayo ndio maradhi yote yaliyoonekana basi sio mgonjwa tena huyo ni maiti maana yake mambo yote haya kaandika daktari huyo ambae *board of hospital* haishughuliki kwenda kuzitizama hospitali hizi, sasa tizameni halafu akaandika *product* sijui ni kitu gani kwa utaalam wa kihospitali, lakini ameandika madawa yake hapa. *Citazon 2x3 thirty eight thousand four hundred* daktari gani anayeandika madawa namna hii akatia na bei. Yaani dawa hizi sita kwa thalathini na nane elfu, halafu dawa nne shilingi thalathini na sita elfu na mia mbili, mgonjwa

gani atakayemudu haya bado bodi inayohusika imekaa hivi hivi haishughuliki, hizi hospitali za vichochoroni zinaua.

Mgonjwa yule jumla anatakiwa laki moja ishirini na nane elfu na mia tisa kwa madawa yale kwa sababu ameshamtisha amemwambia anaumwa na mgongo, unaumwa na tumbo na maradhi yote hayo ameshakuwa maiti tena huyu, sasa maiti kwa shilingi laki moja na ishirini na nane atapona kweli. Mhe. Spika, hii ndio hali ya hospitali zetu za vichochoroni ilivyo sasa ikiwa bodi inayohusika na kukagua hizo hospitali hifanyi kazi yake watu wetu watapata tabu na wataibiwa pesa zao, hakuna utibabu. Sasa dawa hizi ndio zitatibu maradhi yote haya yaliyotajwa katika buku hili haiwezekani,

Kwa hivyo tunachoomba kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwamba hii bodi inayohusika na ukaguzi wa hospitali hizi lazima iwe makini ishughulike na mambo haya kwa haraka, ili watu wetu wanapokwenda waweze kupata tiba vyenginevyo hospitali kama hizi Mhe. Spika, zifungwe hazina maana na hazifai.

Mhe. Spika, suala jengine Mnazi Mmoja Hospital mimi natoa kesi zangu mwenyewe tu kesi hii ni ya mjukuu wangu nilimtuma kwenda kunichukulia vocha kiasi saa mbili usiku akapigwa na pikipiki akaumia sana, nikapigiwa simu mimi ameshafika polisi. Yule aliyempiga pikipiki ni kesi nyengine alikimbia lakini baadae tulimpata nikenda nae hospitali mimi mwenyewe saa nne za usiku, cheti ninacho hichi daktari nilipofika pale mapokezi yupo mwanamke kavaa suweta naona tabu hata kusema, alipofika hakunyanyua hata kidole chake kumtizama pale alipochanika *wallahi billahi tallahi* hakumtizama daktari huyo, mimi pale nikahamaki lakini nikasema nitatizama nitakapofikia. Akanambia shindano ya tetnasi unayo nikamwambia ndio kitu gani hicho akanambia dawa ya tetnasi huijui kwani, nikamwambia siijui mie kwa sababu natoka shamba Pemba huko hakuna mambo hayo akanambia nenda kachukue nikenda kuchukua akampiga hajamtizama chochote.

Halafu akasema twende *theater* ndio daktari *out patient* ameshakaa nikenda *theater* kule na wao wakapiga danadana wakasema twende kwenye *surgical wood* pale nikasema sasa ngojea, kwa bahati nzuri siku hiyo ingelikuwa matatizo. Kwa bahati nzuri akatokea daktari anayenifahamu akanambia vipi mbona uko hapa Mheshimiwa nikamuelezea ndiye aliyeshughulika akenda akamsafisha yule mtoto amechanika, ikabidi ashonwe usiku ule ule alazwe vyeti ninavyo hivi nitamkabidhi waziri. Sasa Mhe. Spika, tukifikia hatua huyo halafu tukasema kuna baadhi sio wote ya madaktari hawafai, kuna baadhi ya madaktari wanamtia aibu waziri, kuna baadhi ya madaktari wanakorofisha hii sekta ya afya hatulaumiki ni kweli na ushahidi upo.

Sasa Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba hawa madaktari wanaohusika awe makini nao sisi tuna uhakika kwamba yeye anafanya kazi nzuri na Naibu wake na katibu Mkuu wake, lakini baadhi ya madaktari wake watamtia doa ambalo tutamlaumu yeye. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii asubuhi hii ya jumapili tangu kuanza Baraza hili sijawahi kuingia Barazani siku ya jumapili kama hii ya leo.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na kitengo cha malaria naipongeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kufanikiwa kutokemeza malaria kwa kiasi fulani, lakini kutokomezwa kwa malaria na mbu tu haitoshi yapo maradhi mengine ambayo yanaathiriwa na mbu nayo ningemuomba ayatokomeze.

Mhe. Spika, nikija kwenye kichocho kipindi hichi ni kipindi cha mvua nyingi, maji mengi hivi sasa yanatuwama katika mito na vimelea vingi na makono kono ambao huwa pembeni ya mito katika sehemu ya majani, kwa hivyo humo ndimo mnamopatikana maradhi ya kichocho. Kwa hivyo basi namuomba Mhe. Waziri kwa kupitia vitengo vyake ichukue hatua ya kuangamiza wadudu hawa kwa kupuliza madawa katika sehemu zile ambazo ziko pembezoni mwa mito ambamo ndimo mwenye vimelea vya maradhi haya ya kichocho, pia na kuua wale koa ambao wamo katika mito ile. Namuomba Mhe. Waziri badala ya kutibu aangamize kwanza kuweka kinga.

Mhe. Spika, nikija kwenye mpango wa damu salama pamoja na kuanzishwa kwa kitengo hiki upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba mtu anayepimwa ile damu ni salama, kwa mfano hivi sasa wako wagonjwa wa UKIMWI, wako wagonjwa wa homa ya maini, wako wagonjwa wa uasharati. Mtu huyu anahitajika apimwe awe salama lakini inasemakana kwamba unapopata ukimwi leo na ukapimwa leo au kesho ukimwi ule hauonekani. Lakini mtu yule atakwenda pale atatolewa damu akishatolewa inaonekana ni nzima wakati ukwimwi ameshaupata kama jana damu ile inatolewa inatundikwa. Je, Mhe. Waziri Mtu yule atakapokuja kutiwa damu kama ile na bado hajapimwa tena si itatokezea athari. Naomba Mhe. Waziri aje atueleweshe zaidi.

Mhe. Spika, nikija kwenye Hospitali ya Kodongo Chekundu hospitali hii ni ya zamani sana inahitaji majengo mazuri ingawaje ni hospitali ya wagonjwa wa akili, lakini akili ikiwa na afya njema unakuwa na ugonjwa wa akili tu na vile vile wagonjwa hawa waangaliwe hali zao licha ya kuwa na ugonjwa wa akili lakini waangaliwe kwa kupimwa virusi vya ukimwi, isiwe mgonjwa yule anaumwa na ugonjwa wa akili na akazidishwa akawa hana nguvu katika mwili hili namuomba Mhe. Waziri pia ahakikishe kwamba wagonjwa wale

wanahudumiwa badala ya kuwa na ugonjwa wa akili wahudumiwe kwa kuangaliwa virusi vya ukimwi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze katika hospitali ile ya Kidongo Chekundu ina wataalam wangapi waliokuwa na elimu ya ugonjwa huu wa akili.

Mhe. Spika, nije kwenye kitengo cha mazingira kitengo hiki kina majukumu makubwa sana, lakini pamoja na majukumu yao ni kuhakikisha kinadhibiti kuenea kwa maradhi. Hivi sasa katika vijiji vyetu tunao ng'ombe wengi ambao wanaitwa machotara, ng'ombe hawa ambao wanatawanya vinyesi na wako karibu na majumba kwa sababu wamejengewa karibu na majumbani wanatoa kinyesi kinazagaa na wakati wale wahudumu wao hawana taaluma hata moja yaani wale wafugaji. Kinyesi kile kinazagaa mitaani wanakwenda kutua nzi wakishakutua wanakuja kueneza kwenye chakula.

Hivi karibuni kulikuwa na maradhi ya matumbo katika Shehia ya Kangani ambayo yanasemekana kulikuwa na nzi wanaokwenda kutua kwenye kinyesi na baadae wanakwenda kutua kwenye vyakula ndio ikasababisha maradhi haya ya matumbo yakaenea. Kwa hivyo namuomba na Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira washirikiane ili kuwapa taaluma wafugaji hawa waweze kuendeleza mifugo yao waweze kulinda mazingira, waweze kulinda afya zao pamoja na watoto wanaotembea ovyo.

Mhe. Ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana asubuhi ya leo na mimi kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mimi mchango wangu utakuwa mfupi kidogo.

Kwanza kabisa niungane na wenzangu kumshukuru Waziri kwa kitabu kikubwa cha bajeti lakini akasoma kwa muhtasari kwa muda mfupi kabisa, kwa hivyo hili naungana na wenzangu kumwambia Mhe. Waziri kumbe unaweza na ingekuwa vizuri kama na wewe ungechukua fomu ya Urais na tungekuwa wapiga debe wako.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa nianze mchango wangu kwa kutoa shukurani za dhati kabisa baada ya kelele zangu nyingi za muda mrefu sasa Mhe. Waziri ameona kama Micheweni wale wanawake waliokuwa hawana wodi ya wazazi na sasa Mwenyezi Mungu ametujaalia tumejengewa.

Kwa hili namshukuru sana na natoa shukurani zangu za dhati kwa suala hili. Namuomba Mhe. Waziri isiwe kwa sababu tumejengewa lile jengo ikawa ndio

basi linatosha lile jengo limejengwa lakini linahitaji madaktari na nesi ambao kuwa watakuwa wanauguza pamoja na hao madaktari wanaoshuhulikia uzazi.

Mhe. Spika, mimi kila siku nakuja hapa napiga kelele na kusema kwamba hospitali ya Micheweni ina upungufu wa madaktari. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri afanye jitihada zake zote atupelekee madaktari Micheweni. Ingawa Mhe. Abubakar amesema kwamba madaktari wakielekezwa kule Pemba wanaona kama wanakwenda jela. Ni ukweli usiofichika kwa sababu hiyo iliyoelezwa. Lakini namuomba pamoja na kuwa madaktari wakielekezwa kule wanakataa basi japo wale wazalendo waliokuwepo karibu na kwao wao wataona wanakwenda kuwasaidia ndugu zao. Namuomba Mhe. Waziri baada ya jengo basi tupatiwe na madaktari na vifaa vinavyohitaji kwa ajili ya uzazi.

Mhe. Spika, hospitali yetu ya Micheweni ina upungufu wa vitanda na magodoro. Mimi nilimwambia Mhe. Waziri wakati tulipopata matatizo ya maradhi ya mripuko ilibidi watu kuchukua vitanda vyao majumbani wakenda wakalaziwa kule. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri hili alione na atufanyie haraka ili tupate tuongezewe vitanda na magodoro na mashuka ya wagonjwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo namuomba Mhe. Waziri, Kilindi nilichokuja nilizunguza na leo nitazungumza tena kwa ukali kabisa. Kule Micheweni kwa bahati mbaya mshahara wa madaktari uliibiwa. Cha kusikitisha mshahara ule baada ya kuibiwa na serikali kufanya uchunguzi wake mpaka ikafika ilipofika mpaka leo madaktari wale hawjalipwa mshahara wao. Hili ni suala la masikitiko huu ni mwaka wa tatu bado watu hawajalipwa mshahara ule. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze lakini hili suala hasa ni la Waziri wa Fedha. Na hiyo siku ya Wizara yake mimi nitakuwa mkali kweli kweli kwa suala hili na nitataka anieleze kwa suala hili Mhe. Waziri.

Kwa sababu gani mpaka leo watu wale hawajalipwa mshahara wao, watu wamefanya kazi, mshahara umeibiwa ina maana kama wanalipizwa wao. Inaonekana kama wao ndio waliouiba. Sasa itakuwaje leo mtu keshafanya kazi halafu asipewe pesa zake. Mhe. Waziri naomba hili suala ukija unieleze lakini hasa nasubiri hiyo siku ya Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa naomba Mhe. Waziri anieleze kuhusu haya maradhi yaliyoingia ya sukari. Namuomba hasa anieleze hii sukari inasababishwa na nini mwanzo wake. Kwa sababu naona maradhi haya sasa hivi imekuwa ni maradhi makubwa katika nchi yetu na kila leo yanaripuka, halafu namuuliza je, wameshafanya utafiti wa kina wakajua hasa chanzo chake hasa inasababishwa na nini? Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie hili suala.

Mhe. Spika, suala jengine ninalozungumza kama wenzangu walivyozungumza kuwa madaktari tunawanyima mishahara na madaktari wazuri wanatukimbia. Kwa hivyo naiomba serikali kupitia kwa Waziri wafanye jitihasa zao wahakikishe kwamba madaktari wana kazi ngumu kwa hivyo wanahitaji kuongezwa mishahara na maposho na marupurupu ili wajione kama wao wanafanya kazi wakiwa wanajiona kuwa wanafanya kazi ambayo kuwa ni nzuri, wawe na hamu hasa ya kufanya hii kazi.

Mhe. Spika, suala jengine na mimi nizungumze hasa kuna madaktari wengine wazuri na kuna wengine huruma zao zinakuwa ni ndogo. Bahati nzuri juzi nilikwenda hospitali ya Mnazi Mmoja kulikuwa kuna ndugu yangu alikuwa anaumwa. Nilivyofika pale bahati nzuri katika kuangaliwa yule mtoto ikabidi akalazwe lakini huko kulazwa keshaandikiwa basi ilifika masaa mawili tunasubiri bado hajapata kuwekwa wodini.

Bahati mbaya akaja mtoto mmoja na mama yake anaumwa na tumbo mpaka pale imekuwa hapaeleweki. Mhe. Spika, haki ya Mungu masaa mawili mtoto yule hajashuhulikiwa madaktari wapo wanamuangalia tu, mtoto analia mpaka na mama ake analia. Kwa kweli jamani huu sio uungwana, kuma madaktari ambao kuwa wanatia aibu.

Mhe. Waziri nakuomba ufanye jitihada ya makusudi upite kule hospitali uwaangalie madaktari wako wakati wa utendaji wa kazi, wala hutokuwa umefanya kosa kwa hilo. Kuna madaktari wengine wanakutia aibu, wewe una imani, unahuruma, unawapenda watu lakini wenzako wanakutia aibu. Hiwezekani mtoto tena mdogo anakwenda pale tumbo linamkata masaa manne madaktari wapo wanamuangalia mama mtu analia naye. Hii inasikitisha . kwa hiyo nakuomba Mhe. Waziri tafadhali kaka angu pita ukiwaangalia madaktari wako, lawama zikija zinakuja kwako.

Mhe. Spika, jengine naomba niungane na wenzangu kusema kama zile sh. 40,000/= wanazotoleshwa wazazi basi zisamehewe, umefika wakati sasa wakuwa zisamehewe. Serikali yetu itakuwa haikosi kwa sababu imewasamehe wazazi shilingi 40,000/=. Hili naliomba Mhe. Waziri na yeye alizingatie na aona kwamba sasa imefika wakati wa kuwa wazazi waonewe imani. Kuzaa pekeyake ni matatizo, na huku tena abebeshwe mzigo huo na pengine watu wake hawana 40,000.

Pamoja na kuwa Mheshimiwa anasema kuwa watu wanasamehewa mama wa huruma yupo. Lakini mama wa huruma hata akikamilisha utaratibu kwa sababu hato kwenda mama huruma akasema nendeni mkamtengenezee, hapana. Mpaka lazima upite utaratibu, aandikiwe mpaka akubaliwe. Naomba urasimu huu

Mheshimiwa tunaomba uondoke iwe hamna malipo haya na mzazi afanyiwe utaratibu kama anavyostahiki kufanyiwa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba kumalizia.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukawa na afya njema na tukawa hai. Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mawazo yangu katika hii Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara hii kama ilikuwa uchangiaji si kila mtu na uwono wake basi mimi ningesema inatosha hutuba yake na mimi ningeunga mkono tu. Lakini ni wajibu wa kila mtu kutoa mawazo yake ili yakafanyiwa kazi na hatimaye kupata maslahi ya watu.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 75, Baraza la Wauguzi na Wakunga ni Baraza muhimu sana kwa sababu ndio chanzo na ndio dalili ya mzazi kupata huduma ya salama, bila ya kupata mkunga basi ukumbuke matatizo yatamfika mzazi.

Mhe. Spika, kutokana na kitengo hiki ningemuomba Waziri wakunga waliyokuwepo vijijini kila wakati wawe wanapewa mafunzo

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe mnaotoka nje tuelewe kwamba si muda mkubwa nategemea kumwita Mhe. Waziri ili kufanya majumuisho kwa hiyo niwaombe baada ya kumaliza dharura kidogo mrudi ili tuje kumaliza kazi hii. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Jadi endelea.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Spika. Ili mzazi anapopata matatizo ya uzazi pale kijijini aidha hana nguvu ya kwenda hospitali kwa sababu hana fedha mkononi ya kuweza kupata gari au pengine hospitali iko mbali na yeye. Lakini kama watakuwa wana mafundisho ambayo ya kila wakati kuweza kujua uzazi ukiwa una matatizo haya, uzazi ukiwa una tatizo hili, basi nina imani wanapunguza ile rasimu ya foleni katika uzazi. Ningemuomba Mhe. Waziri ingawa nina imani zoezi hili linafanyika lakini aongeze juhudi zake kuwapa taaluma wakunga waliyokuwepo vijijini.

Mhe. Spika, nikiondokea hapo nende katika ukurasa wa 57 kusafirisha wagonjwa nje ya nchi. Hiki ni kilio kikuwa cha wananchi wetu. Angalia leo pale kuondoka kijijini mfano Mwera akasema anakuja mjini pengine hana nauli. Leo mgonjwa ambaye kuwa anataka kusafirishwa nje matatizo yake. Hili fungu kwanza ningeomba liongezewe liwe kubwa lakini halafu Mhe. Waziri

aeleze ule utaratibu hasa wa mgonjwa anaekuwa yupo vipi atapelekwa nje na gharama yake kwa serikali itakuwa ipo vipi ?

Kama mtu ana mgonjwa wake ameshindwa na shilingi 20,000 za kumkodia gari akampeleka mpaka hospitali Kuu atazipataje shilingi laki 5 au milioni moja kuongezea pale ili mgonjwa asafirishwe.

Mhe. Spika, ningeiyomba serikali na kwa sababu matatizo yapo kila wakati ya maradhi basi kitengo hiki cha kusafirisha wagonjwa nje kikaongezewa fungu la dharura ili matatizo yale yakitokea basi raia apewe. Nafikiri Mhe. Spika, serikali imenisikia na Waziri ameyafahamu hayo.

Nikiondoka hapo nende ukurasa wa 52 hospitali za vijijini tumezipa majina tu kama ni spitali au ni tuseme ni vituo vya afya vilivyokuwepo katika vijiji. Lakini bado huduma zake ni ndogo kulingana na wakati ulivyo, kutokana na hali ya maradhi sasa hivi napata kuthubutu kusema kama zinaliwa dawa zaidi kuliko chakula kingine chochote.

Mhe. Spika, hospitali zilizokuwepo vijijini zingepewa umuhimu wa peke yake ili wananchi waliokuwepo katika sehemu zile wakapata huduma hatima yake maradhi pengine makubwa ndio akapata kwenda hospitali nyengine. Vyenginevyo kila siku serikali itakuwa ipo midomoni.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kupitia kwako madaktari waliokuwepo vijijini wakapewa umuhimu sana na wakapewa changamoto ya huduma zao hasa wale waliokuwa wanafanya kazi vituo vya mbali katika vijiji vyao basi usafiri pia wapewe.

Mhe. Spika, mimi ninae daktari wangu anafanya kazi Kisiwa cha Kojani anakaa sehemu za Kiuyu kila siku anavutana na baskeli kwenda na kurudi. Binaadamu yule unapomtoa binaadamu kama yule kwenda kwa baskeli kila siku, hatima yake na yeye utamfanye awe ni mgonjwa. Lakini kungekuwa na utaratibu kwa kila kituo kama kile kikawekwa angalau vespa moja daktari ambaye kuwa anafanya kazi sehemu za mbali atapata kujisaidia katika usafiri wake.

Mhe. Spika, si hilo tu hospitali nyingi zilizokuwepo vijijini zimejengewa nyumba za madaktari lakini madaktari mpaka leo hii bado hawajakabidhiwa nyumba zile au hawajawekwa nyumba zile wakaweza kuwahudumikia wananchi, nyumba bado zipo. Mfano kama kijiji changu cha Kojani nyumba za madaktari tayari zipo, huduma ndogo ndogo zinaendelea lakini nyumba mpaka leo hazijahamiwa.

Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri anieleze ni tatizo gani linalopelekea mpaka nyumba zile ikawa hawajakabidhiwa wahusika ili wakakaa pale kuwasaidia wananchi. Katika hapo hapo kama hospitali iliyokuwepo Kojani, serikali imeitangaza kwamba ni Wilaya ndogo, kwa nini isifunguliwe angalau japo wodi ndogo ya wazazi kupunguza urasimu wa kuvuka mzazi nakumpeleka sehemu nyenginezo. Ningeiyomba tena serikali isichoke kufanya kazi zake angalau kupitia Wizara ya Afya waweke japo wodi ndogo ya Wazazi kwa huduma ya mwanzo pale matatizo yakiwa makubwa ndio atakwenda hospitali ya Wete na Chakechake.

Mhe. Spika, kuna kituo ambacho kinaanzishwa kujengwa sasa hivi katika Kijiji cha Maziwani, Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii kupitia mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman ambaye kwa umarufu wake ni Shihata, alichukua ahadi kwa sababu kituo kile mimi mwenyewe kama Mwakillishi nishaanzisha kukipigisha *foundation* na sasa hivi nina matofali 1000 ambayo kuwa tayari kuwakabidhi wajenge, lakini bado kuna wengine hawajapatikana.

Nakuomba Mhe. Spika, kupitia kwako, Mhe. Ali Suleiman nina imani yupo hapa ananisikia, tumuhimize waziri ili wananchi wakishakusimamisha matofali yao kwa wanapobakia basi serikali ijitutumue kuwamalizia pale wananchi ili wapate huduma.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nende katika ukurasa wa 3. Kitengo cha Afya Bandarini. Sasa hivi dunia imegubikwa na maradhi ya miripuko kila sehemu. Yanapotokea maradhi katika sehemu nyengine basi si muda mrefu maradhi yale kama hayakuwekewa vikwazo maalum siku ya pili yapo sehemu nyengine tayari yameshaingia.

Kitengo hiki cha Afya Bandarini, Mhe. Spika, kingepewa changamoto sana na kikawekewa vifaa maalum cha mgeni yoyote, sio kuangalia paspoti tu lakini iwe ni kupima afya yake ndio aingie katika sehemu. Vyenginevyo maradhi yanayotuingia sasa hivi katika dunia ya miripuko basi si hasha nchi yetu kupata kuvamiwa mara moja Mungu atunusuru nayo.

Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri hili aliangalie na wanaoshuhulikia Afya Bandarini basi awape umuhimu zaidi kuwaboresha ili wafanye kazi zinazostahili kulinda maradhi kuingia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kitengo cha takwimu na mienendo ya maradhi, ukurasa wa 14. Sasa hivi tukitaka tusitake maradhi ni mengi sana ndio maana ukaona vifo vya siku hizi vya kushtukiza, yameshamuingia mtu yameshamuuwa kumbe kuna maradhi ambayo yamo katika mwili lakini kwa sababu mtu anajiona anatembea yeye anajihesabu ni mzima tu. Kumbe kwa sababu ana maradhi ya msononeko

katika mwili wake naye kwa sababu anafanya shughuli zake hajipi umuhimu wa kwenda kuangalia afya yake. Siku ya pili maradhi yamekuja juu mauti yapo tayari yanamchukua watu wanashangaa kaumwa lini? Kumbe alikuwa anaumwa muda mrefu lakini utafiti wa maradhi kwa mgonjwa mwenyewe hafanyi na wizara haiwapi taaluma wananchi ili kupima afya zao kila mtu akajijua.

Mhe. Spika, mimi nasema kila mmoja kuangalia afya yake ni muhimu sana tena sana. Mimi leo nathubutu kusema tema. Kama kiumbe wa Mungu nasema *Alhamdulillah* Mungu kanijaalia bahati. Napata kuringa katika Baraza hili maana hapana aliyepima hapa akajua afya yake, lakini leo navaa koti kwa kujinata, afya yangu nashukuru *Alhamdulillahi*, nikiumbe cha Mungu akifanya rehema zake Mwenyezi Mungu sina mjadala lakini napata kujinata katika Baraza hili kama bado afya yangu uko nzuri na ipo salama.kuliko wote waliokuwepo hapa. (*Vicheko*)

Na ndio nikasema hii myenendo ya maradhi kila mmoja ni ugonjwa uliyo katika mwili wake lakini hajijui yukoje. Mimi nilianza msimu wa maradhi muda mrefu nilikuwa nina afya yangu nzuri nikawa na nguvu zangu maradhi yalikuwa yanakwenda taratibu lakini yalipokuwa kunikaba yakanikaba maradhi bahati nzuri hayakuhusiana na maradhi ya vitengo vya hospitali. Lakini kila mmoja hapa hajijui afya yake ikoje na hapo ndio nikapima vipimo 16. Vipimo vile 16 vyote vikanionesha kama afya yangu ni nzuri.

Mhe. Spika, ningemshauri Mhe. Waziri akawahimiza wananchi hasa Waheshimiwa kupima afya ni muhimu. Kukonda kwa mtu ni mazingira lakini unaweza ukajiona una tumbo kubwa kumbe masikini ni matatizo. Wengine wanatembea maguu upande kumbe masikini wana maradhi mengine wanaficha. Tusifiche maradhi.

Mhe. Spika, kitengo hichi kipe umuhimu na kiongezee bajeti wataalamu wake wape taaluma wapate taaluma zaidi, Kitengo hiki cha mwenendo wa maradhi na Utafiti ni muhimu sana, wala usiogope Mhe. Waziri kwa hilo, afya ni mali jamani. Kaa miaka 100 duniani ukipata homa siku moja tu unanung'unika. Unasema homa hii imekuja kwa nini, wewe kiumbe cha Mungu. Lakini kwa sababu hujui afya yako yanaweza yakakushtukiza maradhi yakakuondoa.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya ni Wizara muhimu ni wizara ambayo kuwa inawagusa wananchi wote, ukiwa upo mzima, upo mgonjwa, upo Mwakilishi, upo raia, upo Rais, basi Wizara hii ya Afya ni muhimu kwa kila jamii. Kwa hivyo Mhe. Spika, ningeomba Wizara ya Afya tuipe umuhimu wa bajeti yake japo kipindi hiki kimepita lakini kipindi kinachokuja basi Wizara ya Afya iboreshwe zaidi hususan Afisi Kuu Pemba iongezewe fungu lake Mhe. Spika.

Kwa uwezo wa Mungu kama tutakuwepo hai basi nitakuja kuingia Baraza hili nikija nikaiona Wizara ya Afya Afisi Kuu Pemba fungu lako bado limeminywa basi naweza kuja kusema naizuia shilingi mpaka nione sababu gani limeminywa fungu. Kipindi hiki bajeti imeshaandaliwa naomba tuende kwa hicho kidogo lakini kwa uwezo wake Mungu akituweka hai kipindi kinachokuja basi Wizara ya Afya hawa iangaliwe Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika nije katika madawa ya kulevya. Madawa haya yamekuwa ni athari kubwa sana kwa jamii hasa vijana wetu. Ingawa wengine si vijana ni wazee, starehe haina kijana peke yake na mzee anaitaka starehe. Samahani wazee wangu na akina mama samahanini natoa mifano. Nilimkuta mama mmoja ni mzee si chini ya miaka 70 anagombana na kijana kwa kibiriti kile kinachounga anataka na yeye apate avute. Nikamshangaa sana mama yule. Mimi nikamwamkia kumpa shikamoo, hajaitaka, sijui alielekea wapi mama yule. Ni mtu ananizaa karibu ya kunijukuu lakini shikamoo yangu hakuitaka. Nikaona sina haja ya kumueleza lolote nikaondoka.

Mhe. Spika, bado serikali ina kazi, serikali ina jukumu, viongozi pia wana majukumu kuwaelimisha vijana wetu kutokana na athari ya madawa ya kulevya. Ukishakuingia pale kutoka si rahisi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache niunge mkono hoja nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo nami niwe mmoja wa wachangiaji wa bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake wote ambao wamekaa wakaandaa hotuba hii kwa ufanisi na kwa utaalamu mkubwa.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa sana nikakwenda moja kwa moja katika kitabu hiki, niingie katika ukurasa wa 102. Nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuanzisha mradi huu wa Afya ya Akili. Kwa kweli wamekaa wakaona kwamba ipo haja ya kuanzisha mradi huu. Mimi nawashukuru kabisa pamoja na mambo mengi waliyoandaa katika kitabu hiki lakini kwa mawazo yangu naona kwamba kuna mambo ambayo muhimu lakini hawakuyatia katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, katika nchi yetu wagonjwa wa afya ya kili kila siku wanaongezeka siku hadi siku. Lakini si hilo tu wapo wagonjwa wengi wanazurura ovyo na wengine wanavunja magari, wanapiga watu, lakini kubwa wapo wagonjwa wa

afya hii ya akili wanavua nguvu ovyo majiani. Namuomba Mhe. Waziri hili nalo angelitia katika mkakati wake maalum wa kuwadhibiti wagonjwa hawa na kuwakusanya pamoja wakawahifadhi.

Mhe. Spika, pia wapo wagonjwa wa akili wanawake inawapelekea kuharibiwa pengine labda pengine wanavua nguo ovyo inawapelekea kuwatamanisha watu na watu wenye akili timamu wanawabaka na kuwafanyia vitendo ambavyo sio vya halali. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri hili alitie katika mpango na ikiwezekana wawe na mkakati maalum wa kupita majiani wakawakusanya wagonjwa wale.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika wizara, hapo nyuma tulikuwa tunasikia kwamba kuna mkakati wa kujenga hospitali kuu ya rufaa kutokana na hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja imekuwa ndogo na haitoshi. Lakini kwa sasa hivi Mhe. Spika, naona dhana ile hatuisikii tena kutajwa kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri akija kutoa majumuisho atwambie kwamba mpango ule umefikia vipi, upo au haupo tena?

Mhe. Spika, sote tunajua katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja imekuwa inabanabana magari hapo hapo, sehemu za kuhudumia wagonjwa hapo hapo. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Waziri alione hili na aone upo umuhimu wa kutanua hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, si hilo tu, wewe unaweza ukampeleka mgonjwa wako pengine anaumwa na anatakiwa alazwe, lakini ukaambiwa kwamba subiri kuna mgonjwa anatarajiwa kupata ruhusa. Mhe. Spika, jambo hilo sio zuri kwa sababu pengine mgonjwa wako hajuulikani hali yake aliyokuwa nayo na kitendo cha kukaa akasubiri mgonjwa apate ruhusa pengine afike daktari kwanza katika kuzunguka amuone mgonjwa huyo. Mhe. Spika, pengine ni kweli atapewa ruhusa na kama hajapewa ruhusa huyu mgonjwa mwengine itakuwaje.

Mhe. Spika, wenzangu wengi wamechangia na kila siku kila bajeti ya Wizara ya Afya kina mama wa Baraza hili tunachangia mambo ya uzazi kwa kina mama. Mhe. Spika, mimi nilitegemea katika kitabu hiki Mhe. Waziri atatwambia kwamba kina mama ambao wanajifungu kwa operesheni ile ada ambayo walikuwa wanachangia ikaondoshwa, lakini kinyume chake hajatueleza kitu. Mhe. Spika, mwana mama anapokuwa anaumwa kuelekea wakati anakwenda kujifungua anakuwa na hali ngumu. Mhe. Spika, mimi nitaelezea katika kikao hiki pengine hutonielewa kwa sababu wewe sio mwana mama, lakini naamini kwamba unaishi na akina mama na pengine mwenyewe huwa unawapeleka hospitali.

Mhe. Spika, nikwambie kwamba mwana mama anapokuwa anakwenda kujifungua labda niseme akili yake huwa haipo na ndio maana kuna wana

mama wanapopelekwa hospitali pengine anaanza kuvua nguo kabla hajafika ndani. Hii yote ina maana kwamba anakuwa katika hali mbaya. Mhe. Spika, mwana mama huyo anapoambiwa achangie pesa za uzazi kwa kweli hatumtendei haki.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atufikirie suala hili, pia nimpongeze au nishukuru kuwa pamoja na yeye mwanamme lakini Naibu Waziri wake ni mwana mama na uchungu wa kuzaa anaufahamu. Kwa hivyo, mimi nilidhani Mhe. Naibu Waziri atadhidi kumshauri Mhe. Waziri kuhusu suala hili la kuondosha ile pesa ambayo analipa mzazi wakati anapojifungua kwa operesheni. Mhe. Spika, sitaki niseme sana jambo hili kwa sababu naamini kwamba kina mama wenzangu wote wamelizungumzia suala hili. Kwa hivyo, niseme kwamba Mhe. Waziri nakuomba sana suala hili la kuondosha pesa ambayo anaitoa mwana mama naamini kwamba na kwa hekima zake alizonazo atakapokuja kutoa majumuisho hapa mbele ataondosha suala hili.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika suala la *fast track.* Mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuona kwamba ipo haja ya kutenga sehemu ile, nampongeza kwa dhati kabisa. Pia naamini kuwa na sisi tunataka twende na wakati kwa hiyo namuomba Mhe Waziri basi kuna mapungufu katika sehemu ile ayaangalie. Mhe. Spika, unaweza ukenda katika sehemu ile pamoja na kuwa mgonjwa analipia mimi nakumbuka kipindi cha nyuma mgonjwa anayelala pale kwa siku analipia shilingi 10,000.

Mhe. Spika, wananchi wetu ni masikini sana, haina maana kwamba mtu anapolipa shilingi 10,000 akawepo maeneo yale si kwamba anazo pesa nyingi, ni kwamba mtu anataka ile huduma nzuri ndio anajibana katika mambo yake yote anaona kwamba bora nilipie huku ili nipate nafasi pengine ya kumuuguza mgonjwa wangu vizuri. Mhe. Spika, mgonjwa anapokuwa sehemu ile huwa anamatarajio ya kwamba atapata huduma nzuri lakini ikawa ni kinyume cha hapo kwa kweli inatia huzuni.

Mhe. Spika, hakuna kitu muhimu kama kupata *hospitality* ni jambo muhimu, *hospitality* mgonjwa kwa kiasi anapata nafuu na mgonjwa anapopata kauli ambazo hadhirishi basi pengine mgonjwa huyo maradhi yanatazidi. Mhe. Spika, unaweza ukenda pale ukakuta mpaka saa nne hakujasafishwa katika chumba hicho na unapouliza unajibiwa kwa ujuba, kwamba tuna kazi nyingi. Mhe. Spika, kweli huu ndio utaratibu pamoja na kuwa na kazi nyingi basi angalau jibu kauli mzuri ya kumridhisha mtu, sio unajibu kwa ujuba. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama kuna wafanyakazi hawatoshi wako kidogo basi tujitahidi tuongeze wafanyakazi, pia kama kuna kozi maalum basi ya kuwasomesha hao wafanyakazi wetu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja tuwasomeshe umuhimu wa kutoa *hospitality*.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika homa ya malaria. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kwa kupunguza ugonjwa huu wa malaria katika nchi yetu. Mhe. Spika, pia nimpongeze zaidi kwa kuwa na utaratibu wa kupiga dawa majumbani kwetu, utaratibu huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza maradhi haya ya malaria. Lakini pamoja na kupungua maradhi haya hivi sasa malaria yamekuwa kwa kasi kubwa, labda nikwambie Mhe. Spika, mimi kwa mwezi pengine napata malaria mara mbili au tatu.

Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Waziri malaria bado ipo sijui labda wamefanya utafiti kuwa ni kitu gani kinachosababisha hivyo. Mhe. Spika, jengine labda kwa mawazo yangu ni kwamba pengine kuna baadhi ya wananchi kuwa hawataki kupigiwa dawa majumbani mwao kwa sababu tofauti, wengine wanasema dawa zinaharibu mapazia, dawa zinaharibu vyombo. Kwa hivyo, mimi nataka nitoe wito kwa wananchi wetu zaidi kina mama kwa sababu naamini kwamba kina baba wao hawakai majumbani wakati wote, kina mama wao ndio wanakaa majumbani muda mwingi. Kwa hivyo, niwaombe wananchi tukubali tupigiwe dawa hii ya malaria, na tusidhani kwamba kupigwa kwa dawa ya malaria majumbani kwetu kuna habari vitu vyetu vya ndani ya majumba.

Mhe. Spika, kwa kuwa imetoa dakika kumi na tano labda niseme kwamba namalizia kwa kuunga mkono hoja mia juu ya mia. Nakushukuru sana.

Mhe. Ali Moh'd Bakar: Mhe. Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuifikia siku hii ya leo tukawa tuko hai. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi kutoa mawazo yangu machache.

Mhe. Spika, kwa sababu bajeti hii imeshachangiwa sana ningependa sana nichangie kwa ujumla jumla. Mhe. Waziri kabla sijaendelea na mchango wangu kwanza niseme kwamba naunga mkono bajeti yako mia kwa mia ila kuna mambo nitahitaji kupata ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza kidogo nilitaka niulizie hili suala la kitengo cha kupambana na madawa ya kulevya. Mhe. Spika, kuna kitengo maalum, kitengo hiki dhamira zake ni kupambana na madawa ya kulevya kama ilivyotajwa na ilivyoandikwa humu ndani, lakini inaonekana kwamba kitengo hiki kinapambana na wanaotumia madawa ya kulevya na hakipambani na madawa ya kulevya. Mhe. Spika, inashangaza sana kuona kwamba kuna kitengo kinapambana na kina watu ambao wanaaminika sana na kuna watu ambao wameaminiwa na kuna watu wanafanya kazi vizuri, lakini chakushangaza ni kwamba kila siku naona haya madawa yapo yanaingizwa na watu wanatumia.

Kwa hivyo, hiki kitengo kinapambana vipi, naamini Mhe. Waziri alikiteua kitengo hiki ili kusudi kimsaidie kazi ya kupambana na matukio haya. Lakini unakuta kwamba watu kila siku unakuta vijana umo anatembea lakini yuko usingizini na watu wengine wengi kama alivyosema Mhe. Jadi hapa amemkuta mama huko njiani kamsalimia kakataa kwa kudhani kama ni mzee mwenzake kumbe yule mama ni kijana bado. Mhe. Spika, mimi nasema hiki kitengo bado hakijafanya kazi vizuri kama ambavyo wizara au serikali imekusudia na inashangaza kwamba watu wanaonekana humu mitaani lakini wanaweza wakakamatwa wale wanaotumia wale wanaoingiza hawakamatwi.

Suala ni je, tunawalinda au ni kitu gani kwa sababu haiwezekani kwamba kuna kitengo hiki lakini watu wanawaona na watu wanajua ukenda hapo Miembeni kuna nyumba maalum watu wanauziwa madawa ya kulevya. Mhe. Spika, hiki kitengo kinapambana na madawa ya kulevya kivipi Mhe. Waziri naomba kidogo uje unieleze ni namna gani kinapambana na madawa ya kulevya kwa sababu watu wamo wanavuta madawa, tunaona wanaathirika lakini wale wanaowauzia wako wapi. Kwa hivyo, kitengo hiki kinafanya kazi gani mpaka leo hii bado ikawa hawajaweza kuwakamata hao wahusika hasa ambao wanafanya shughuli hizi.

Mhe. Spika, pia nilitaka kujua kuna tathmini hapa ya maradhi ya minyoo maskulini ilifanywa, hii tathmini ilifanywa kwa Unguja tu. Mhe. Spika, afya za watu wetu, afya za Wazanzibari zinahitaji kulindwa, zinahitaji kuchunguzwa, zinahitaji kufanyiwa kazi. Mhe. Spika, matatizo mengi yako mashuleni wakati mimi nasoma niko kwenye madarasa ya chini pale kila siku Wizara ya Afya ilikuwa imejipangia utaratibu kila kipindi fulani inakuja mashuleni kupima kichocho na huwa wanawabaini vijana ambao wana maradhi ya kichocho. Wakati ule ilikuwa mvua ni nyingi kila eneo lilikuwa na madimbwi na maji, kwa hiyo vichocho vinafumuka sana kwa sababu watoto hata humo majumbani mwetu hatukogi tunakwenda tukikoga kwenye madimbwi.

Lakini sasa hivi madimbwi yamepungua kwa kiasi kikubwa lakini huu uchunguzi na haya maradhi bado yapo, lakini kwa nini huu uchunguzi ufanywe Unguja tu peke yake ama ulifanywa Unguja kwa kubaini kwamba huku ndio kwenye hayo maradhi Pemba hakuna au ilikuwa imefanyiwa Unguja baadae wakimaliza halafu watakwenda na Pemba. Mhe. Spika, kwa sababu humu kwenye kitabu haikueleza kwamba sisi tukimaliza Unguja tutakwenda na Pemba. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kidogo nataka uje uniambie ni kwa nini suala hili kule Pemba halikufanyika na watoto wapo na maradhi yapo.

Mhe. Spika, pia uchunguzi wa hawa makonokono pia nao ulifanyika hapa Unguja peke yake. Mhe. Waziri kule Pemba makonokono yapo mengi na yanasababisha maradhi haya. Kwa hivyo, tunapotaka kujadili afya za kila mtu

basi Mhe. Waziri ni vyema uwe wazi na ni vyema uwe muadilifu na uone kwamba kila pahala ipo haja ya kusimamia na kuhakikisha kwamba hizi afya za watu wote zinalindwa. Mhe. Spika, kuna kitu kimoja kinanipa tabu kidogo ambacho nilitaka Mhe. Waziri pia aje anibainishie nacho hiki Kitengo cha Afya Bandarini.

Mhe. Spika, sisi hapa Zanzibar tunatumia vitu vingi sana kutoka Bara kama vile mboga mboga na hizi mboga kutoka Bara kwa kweli kumea kwake zinakuwa zinatumia kemikali kwa kuulia wadudu. Kwa hivyo, hiki kitengo kina vifaa gani vya kubaini mboga mboga hizo zinapoingia kwamba hazina sumu na zinafaa kuliwa hapa Zanzibar. Mhe. Spika, kwa sababu naona haya maradhi ya miripuko, maradhi ya sukari, maradhi ya presha na maradhi mengine mengine mengi hapa kwetu yapo mengi mno. Kwa hivyo, hiki kitengo kina uwezo gani katika hali ya kusimamia na kubaini kwamba hizi mboga mboga zinazotoka Bara zina usalama kwa watumiaji.

Mhe. Spika, maana yake kila siku unapata kesi ambayo kwa kweli ukiziangalia hujui chanzo chake, lakini inawezekana chanzo chake ni zile mboga tunazokula kwa sababu sisi tunakula mboga kutoka Bara kwa kiasi kikubwa kwa sababu hapa Zanzibar ndipo kwenye soko lake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika hili hebu nataka kidogo uniabainishie kwamba je, hiki kitengo chako pale Bandarini kina uwezo gani katika hali ya kusimamia afya za walaji kwa mboga mboga ambazo zinaingizwa.

Mhe. Spika, nisema jambo jengine kwamba Mhe. Waziri amebahatika sana kule Pemba kupata Afisa Mdhamini ambaye yuko kule Pemba. Mhe. Spika, Afisa Mdhamini huyu kwa kweli anafanya kazi na hivi ndivyo watu wanavyotakiwa wawe huyu jamaa ni muadilifu. Mhe. Spika, nasema kulingana na ule uwezo wake na imani yake kwa binadamu wenzake huyu anatoka katika familia masikini sana, labda ni hilo ndilo lililompelekea kujali wenzake kwa kiasi kikubwa na hapo alipo Mhe. Spika, nakuomba umuwezeshe na pia umpatie madaktari. Mhe. Spika, kama Hospitali ya Wete leo mwaka wa tano hakuna *specialist* wa upasuaji hili ni jambo ambalo inakuwa ni tabu sana.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri kwa sababu nina nia njema na wewe mwenyewe binafsi unajali afya za wenzako na ndio maana unataka kila pahali paende vizuri lakini wakati mwengine mambo mengine hayawezi kwenda na wakati. Lakini Mhe. Waziri nakuomba kwa sababu kule unaye msaidizi wako mzuri, na unaye mtu ambaye ana imani basi muwezeshe ili aweze kukusaidia kazi vizuri. Kwa kweli sisi tunamshukuru sana tuliokuwepo kule Pemba kwani anatusaidia, anatujali na pale inapotokea vyenginevyo anatushauri la kulifanya. Mhe. Spika, hilo ni jambo kubwa na ni jamboa

ambalo sio kila mtu analo, kwa hiyo nakuomba Mhe. Spika, huyu jamaa muwezeshe katika hilo.

Mhe. Spika, wamezungumza waheshimiwa hapa hata Mhe. Assaa hapa juzi alizungumzia suala la operesheni hospitali ya Mnazi Mmoja na suala la ulipiaji wa operesheni hizo. Mhe. Spika, mimi naamini pesa ile si mchango, pesa ile si kwamba ni ada ya kumfanya mtu kwamba lazima atoe, lakini kuna mambo mengine yanahitajika kufanywa. Mhe. Spika, ni kwamba sisi ni binadamu tabia zetu tulivyo unapomwambia mtu toa shilingi mia mbili ili ufanye jambo fulani, tayari yule ambaye anataka kulifanya lile jambo anaona kwamba hii ni sheria. Kwa mfano, imetokea mwenzangu mimi hana ile pesa lakini pia hana mtu kwa wakati ule wa kumsaidia kuja kuitoa, inawezekana hiyo ndio ikawa ni sababu ya kifo chake. Watu wakaingia huku wakitoka huku na badala yake mtu akapotezewa maisha yake hivi hivi anajiona.

Mhe. Spika, ni vyema hili suala walilolishauri wenzangu waliopita ni vyema ile pesa pale iondoshwe na wizara itafute namna nyengine ambayo inaweza ikapata mapato yake kupitia maeneo mengine, lakini pale iondoke. Mhe. Spika, kwa sababu mtu akishaumwa na uchungu hali inakuwa ngumu mambo ni mawili anaweza akajifungua salama au anaweza akafa. Kwa hivyo, anapofika pale akenda akipata vikwazo vyengine ambavyo kwa kweli viko nje ya ile hali aliyonayo maana yake ni kumuonea.

Mhe. Spika, mimi kama ni mwakilishi kwa mfano mgonjwa ananiambia mwakilishi nisaidie mimi naumwa sana kwa hiyo naomba gari. Ina maana nimwambie basi gari hii hapa kwa hiyo nipe shilingi elfu arubaini nikatie mafuta, hapo mimi itakuwa nimemsaidia kitu gani, itakuwa sijamsaidia hata kidogo. Mhe. Spika, hayo ndio matatizo tuliyokuwa tunayapata.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri alione hili kulingana na hali zetu na hali ya ukwasi wa maisha tuliyonayo katika nchi yetu kwa kweli watu wetu ni wanyonge, ni masikini na hawana uwezo hata wa aina moja, atokee Mhe. Mati kaenda huko ana wagonjwa wake watatu akifika anaambiwa walipie wewe sasa. Mhe. Spika, sasa kama hayupo basi tayari mtu tunamkosa, hayo tunayasema kwa sababu yameshatokea katika maeneo yetu mengi tu, mtu anapoteza maisha yake kwa kukosa pesa kidogo tu. Kwa hivyo, ni vyema jambo hili kulipigia marufuku kwa nia safi ili kusudi litafutiwe utaratibu mwengine ambao unaweza ukawapa unafuu hawa mama wajawazito na halafu tukaliangalia kwenye eneo jengine.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naomba niendelee kusema kwamba naunga mkono hoja na Mhe Waziri ayazingatie yale yote ambayo yamesemwa

na halafu ayafanyie kazi kila moja kwa umuhimu wake. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nitajaribu kusema kwa ufupi sana ili nisije nikakhalifu miadi tuliyokubaliana.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri nakumbuka siku za nyuma nilikuwa nikipiga makelele sana kuhusu nyumba za daktari, nashukuru kilio kile kimeitikiwa na sasa ndani ya jimbo langu nina karibu nyumba tatu za madaktari. Kwa hivo, ni jambo zuri sana ila sasa ninachomuomba aharakishe kuzikamilisha na kwa kuwa nyumba zipo tupate madaktari, na katika madaktari ambao nawahitajia sana na *special* kwa Jimbo la Chonga ni hawa wakunga wanaozalisha watu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi hajanijengea njia hata moja katika jimbo langu, sina njia ya Tundaua, sina njia ya Pujini, sina njia ya Mgelema kote huko kuna vituo vya afya lakini kwa sababu hatuna madaktari hivi sasa hulazimika kuwapakia wazazi kwa gari na kutokana na njia kuwa mbaya hawafiki hospitali hujifungulia ndani ya gari yangu njiani. Naomba sana sasa nipatiwe madaktari na hasa wakunga.

Mhe. Spika, jambo la pili ni kwamba tuna tatizo kubwa la maradhi ya sukari katika jamii yetu, mheshimiwa jamii haina taaluma namuomba sana Mhe. Waziri wa Afya ajitahidi kutoa taaluma kwa jamii kuhusu maradhi ya sukari, juzi tu nilimpeleka mzee wangu mmoja hapa Mnazi Mmoja kwa kweli nilifurahi mno na ushauri aliopewa na daktari pale. Mhe. Spika, muda wote amekaa miaka minne anaishi na sukari hajui cha kufanya, juzi pal nilipata mwangaza. Kwa hivyo, nimepata hamu kwamba ingekuwa taaluma kama zile zinaenea katika jamii basi nafikiri tatizo la sukari watu wangekwenda nalo vizuri.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba tumekabiliwa na jinamizi la matatizo ya maradhi ambayo kwa kweli siku za nyuma tulikuwa hatuyaoni sana, maradhi ya miguu, maradhi ya sukari na maradhi ya saratani. Nafikiri ni muhimu Wizara ya Afya pia ikatoa taaluma na ingeieleza jamii hasa tatizo hili chanzo chake ni kitu gani kwa sababu naona yamekuwa mashaka makubwa hujui mkongwe, hujui kijana sasa hivi kila mtu aliyosema Mhe Jadi anakwenda upande upande. Kwa hivyo, naiomba sana wizara hii ijitahidi kuwaeleza watu sababu za matatizo haya ni kitu gani pengine ni sababu za vyakula au kitu gani lazima tupate taaluma pengine tunaweza tukajikinga.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu ukaguzi wa vyakula kama michele tunayokula, vyakula vya makopo, hata haya madawa katika hizi *dispensary* zetu isije ikawa

yanasababisha haya matatizo tunayoyataja kila mara. Kwa hivyo, naomba kama kuna kitengo hiki kiwe na juhudi ya kufanya ukaguzi kwamba vyakula tunavyokula ni salama, juhudi ni muhimu sana kwa sababu unaweza ukenda dispensary ukapewa dawa lakini ukiangalie kumbe imesha-*expire*.

Mhe. Spika, ni kwamba jamii yetu imekabiliwa na wagonjwa wa akili wengi na bahati mbaya wameachwa kudhurura mitaani na wagonjwa hawa wanasababisha matatizo mengi, wengine ni wagomvi kutokana na yale matatizo yao ya akili yanawafanya waharibu mali za watu njiani, wapige watu ovyo. Mhe. Spika, sijui dhamana ya kuwahifadhi hawa ni ya Wizara ya Afya moja kwa moja lakini nilikuwa naomba kama ni wao basi iwahifadhi kila watakapohisi kuna anazubazubaa basi ni muhimu mtu yule ahifadhiwe mahali maalum na apate huduma.

Kama yeye siye muhusika moja kwa moja basi atoe ushauri kwa wahusika lakini ni hatari kuwaona watu wakizubaa namna ile, mheshimiwa wengine wanaharibu mali za watu na wengine wanaharibiwa wao, hilo ni jambo la kusikitisha. Kwa hivyo, serikali ina wajibu wa kuhakikisha wale watu wanawahifadhi pahali na tupate usalama katika jamii.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu Mradi wa Malaria wenzangu wengi wamegusia mradi huu kwamba tunapigiwa dawa majumbani japo wako asilimia ndogo wasio taka lakini wengi wetu tunataka, lakini sasa ni kwamba dawa inamalizia ndani, vyanzo vya malaria haviko ndani tu. Mhe. Spika, cha msingi ni kuua yule mbu anayesababisha malaria nafikiri Mhe. Waziri ajipange vizuri zaidi pamoja na serikali kwa jumla iwe ni mradi mkubwa kuhakikisha mpaka mle mpembeni mwa nyumba mnapigwa dawa.

Mhe. Spika, kwa sababu unaweza ukapiga dawa wakati ule mbu hayupo amejificha kwenye vichaka, kwenye migomba, kwenye mashimo ya karo sehemu zote hizo ilikuwa mpatiwe dawa ili kuhakikisha kama malaria tunayakomesha. Mhe. Spika, ni kwamba malaria yapo na kwa kweli yakimpata mtu mara hii yanakuja kwa nguvu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hilo naomba alizingatie.

Mhe. Spika, jambo jengine la mwisho nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri na hili nasema kama ni yeye moja kwa moja au kama dhamana si yake basi atoe ushauri kwa taasisi inayohusika lakini kuna maeneo fulani yanahitaji kujengwa vyoo vya *public* kwa sababu watu wanajisaidia ovyo hasa maeneo ya madiko, maeneo ya masoko mle ambamo mna mkusanyiko wa watu mkubwa. Mhe. Spika, mtu anaweza kushikwa na haja akashindwa na pakuelekea inakuwa ni mashaka makubwa. Kwa hivyo, naomba sana hili lifanyike ili ionekane kama

mtu popote atakapobanwa na mambo basi asiende hatua nyingi apate pahala pa kujisaidia wenzetu wengi ndivyo wanavyofanya sasa hivi.

Mhe. Spika, ahsante sana ni hayo tu mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia hoja hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kutupa afya na nguvu tukaweza kufika hapa na kuweza kuchangia na kushauri mambo mbali mbali yanayohusiana na nchi yetu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani Abeid Karume. Kwanza kwa juhudi zake za kuendeleza nchi yetu kwa amani, salama na utulivu na tukaweza kutekeleza mengi kwa kipindi ambacho yeye amekaa madarakani lakini pia kwa kipindi ambacho wenzake ametuteuwa kumsaidia shughuli hizi zilizomo ndani ya serikali yetu.

Namshukuru sana tena Mhe. Rais kwa imani yake aliyoonesha kwangu kwa kuniteuwa kuwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ili kumsaidia shughuli ambazo zimo ndani ya serikali na naamini tumejitahidi kadiri tulivyoweza chni ya uongozi wake imara na mahiri kuweza kutekeleza mengi. Namshukuru sana Mhe. Rais kwa hilo.

Pia Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi kwa kutusaidia kutuelekeza na kutuongoza mambo mbali mbali yake ambayo tunawaendea kwa ushauri katika wizara yetu ambayo wakati mwengine huwa tunahitaji ushauri wao. Kwa hivyo, walikuwa karibu sana na sisi kwa kutusaidia katika kutekeleza shughuli zetu.

Vile vile nichukue nafasi hii maalum kumpongeza Mama Shadya Karume, Mwenyekiti wa *ZAYEDESA* kwa jinsi alivyoisaidia wizara yetu hasa katika suala la kupunguza vifo vya mama na watoto. Mama huyu amekuwa jasiri, amefanya mengi hasa katika suala hili la kupunguza vifo vya akinamama.

Mhe. Spika, mama huyu ameweza kutusaidia kutujengea *maternity* zetu, kutuongezea wodi yetu ya *maternity* iliopo Hospitali ya Mnazi Mmoja, wodi yetu ya *maternity* iliopo Wete, Wodi ya Kivunge, Wodi ya *Maternity* iliopo Nungwi na hivi karibuni tumefungua wodi ya *maternity* ilioko Micheweni. Tuna imani kwamba ameafanya haya kwa kuwa mama huyu alikuwa

mkereketwa kweli kweli na yuko mstari wa mbele kuona kuwa kinamama wanapunguza idadi ya vifo vinavyowakabili. Ametuunga mkono sana katika suala hili la *millennium* katika kupunguza vifo vya mama na watoto. Tunamshukuru sana Mama Shadya Karume.

Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Dole walionichagua kwa kura nyingi sana ambazo nahisi mchango wao pia umechukua nafasi kubwa ya mimi kuweza kupata uteuzi huu. Kwa hivyo, nawashukuru sana na nina imani wataendelea kuwa na imani na mimi wanirejeshe tena na niweze kufanya mambo mengine makubwa na mazuri zaidi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nimshukuru Waziri wangu wa Afya Mhe. Sultan Moh'd Mugheir, kwa jitihada na imani zake alizokuwa akionesha kwangu katika kushirikiana kutekeleza shughuli zetu za wizara yetu, kunishauri, kunipa maelekezo na kuweza kufanikisha mambo mengi ambayo tumeyafanya kwa karibu zaidi katika wizara yetu. Nashukuru sana Mhe. Waziri amejitahidi sana kwa hilo na kwa kweli alikuwa ananipa heshima kubwa kuwa naye karibu katika kutekeleza majukumu ambayo tumekabidhiwa na taifa letu hili.

Pia nimshukuru Katibu Mkuu wa wizara hii kwa kuwa tulipokuwa tukihitaji maelekezo na ushauri katika mambo ya kitaalamu alikuwa karibu na sisi sana kuweza kutekeleza. Kama hiyo haitoshi, ni katibu ambaye ni jabari na jasiri aliyekuwa akizaa mbinu mbali mbali katika kuiendeleza wizara yetu. Namshukuru sana kwa hilo.

Lakini pia niwapongeze Wakurugenzi na Watendani mbali mbali pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa jinsi walivyokuwa wakitusaidia katika kutekeleza wajibu wetu. Kwa sababu bila ya wao sisi wenyewe tu tukakaa pale wizarani kuweza kuyatekeleza yote kwa kweli isingekuwa rahisi. Kwa hivyo, tunawashukuru sana kwa hilo.

Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa jinsi walivyokuwa wanatusaidia changamoto zao walizokuwa wakitupa, masuala mbali mbali yalikuwa yakituchemsha na pia busara, ushauri na maelekezo yao kwa kweli tumeweza kufanya mengi katika wizara yetu, hususan kamati mbili ambazo tumefanyanazo kazi katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa kweli ni kamati ambazo zimetusaidia sana na wao wenyewe walikuwa wanakiri kuwa yale waliokuwa wanatuelekeza tukiyafanyia kazi kwa kadiri Mwenyezi Mungu alivyotujaalia. Kwa hivyo, tunazishukuru sana kamati hizo pia wajumbe wote wale waliokuwa akitueleza matatizo katika shughuli zetu tuweze kuyatekeleza na sisi tukawa tunajitahidi kutekeleza.

Mhe. Spika, pia nisiwe mchoyo wa fadhila nikushukuru na wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwa jinsi ulivyokuwa ukisimamia shughuli zetu katika Baraza kwa umahiri wako wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wako kwa kutuelekeza na kutufahamisha vizuri katika shughuli zetu hizi ukiwa pamoja na sisi katika kufanikisha mambo yetu yote ya shughuli za Baraza na tumekwenda vizuri. Tunakushukuru sana Mhe. Spika, kwa hilo.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo kama kuna wengine sikuwashukuru wachukulie na wao nimewaingiza humo, lakini nia yangu ni kuwashukuru wote wale waliokuwa wakitusaidia kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, mimi nataka nichukue nafasi maalum hii leo kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia hotuba yetu. Kwa kweli wametupa moyo na tukiondoka hapa tutajitahidi haya waliyotuelekeza ambayo wameyaona kama ni mapungufu basi kujitahidi kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, nataka kukwambia sisi viongozi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na watendaji wetu wote ni wasikivu, tukiambiwa na wenzetu tunasikia na yale wanayotueleza tunajitahidi kuyatekeleza kwa yale ambayo yamo ndani ya uwezo wetu, tunajitahidi kadiri ya uwezo wetu wote. Pia huwa tunawashauri na kuwaelekeza wale ambao wako chini yetu vipi wafanye, vipi watekeleze shughuli zao pamoja na wao wenyewe wanapenda kujituma na kufanya shughuli zao, lakini pia tunapowapa maelekezo wanasikia na wanatekeleza.

Sasa Mhe. Spika, tumepata wachangiaji wengi wametusifu sana, naamini ni haki yetu. Kwa sababu mwenye haki apewe basi na sisi naamini kwa kipindi hiki cha miaka mitano tumejitahidi katika wizara yetu. Watu wanasema raha ujipe mwenyewe, lakini katika Baraza hili raha tumepewa na wajumbe wenzetu. Kazi tuliyoifanya wameiona hasa kamati zinapopita zinaona, wanapokuja kutembelea wanajua hatua gani tumefikia, wapi tulikuwa na wapi tupo na tunaendeleaje wameona. Mapungufu gani tulikuwanayo na sasa hali gani tunaendelea nayo pia wameona.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nashukuru sana wajumbe kwa wale waliochangia na waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia kwa kweli mmetupa moyo mkubwa na sisi tutajitahidi kwa ambayo mnaona ni mapungufu kuweza kuyarekebisha.

Lakini nije kidogo kwa baadhiya hoja ili kuweza kumsaidia waziri wangu kidogo na yeye atakuja kuongezea nguvu baadae. Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa sisi ni wasikivu tukiambiwa tunajitahidi kutekeleza. Sasa ningeliomba yale tunayohisi mapungufu yaliyotokea basi tumeyasikia na

tutajaribu kuyatekeleza. Kwa maana hiyo basi, nataka nianze kwa kumuomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Kiongozi wa Upinzani wa Baraza hili. Nimuombe sana sana asiende kutafuta hizo *rain boot*. Kwanza nimpe pole kwa yale yaliyompata nadhani ni mtihani wa Mwenyezi Mungu na Mungu atamjaalia mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki ampe malazi mema.

Lakini nasema hili tutalichukua na tutalifanyia kazi kadiri ya uwezo wetu. Na yale mengine yote yaliompata katika hili na mengine ya mtoto. Nataka kusema kwamba, sisi ni viongozi na tunao viongozi wenzetu na tumekwenda mpaka ngazi ya chini kwa watendaji wa shughuli za kawaida. Hatukatai Mhe. Spika, kuwa hakuna mapungufu, mapungufu yapo na hatukatai kuwa sisi wafanyakazi wetu wote watakuwa safi kama malaika, tunajua lazima watatokea wengine wawe wakorofi, haya ni mapungufu ya kibinadamu na mengine haya yanatokea tangu mtu anapozaliwa tabia yake anakuwa tayari anavyo vitu hivyo.

Sasa bahati mbaya inayotokea ni kwamba, hatujafikia mahali pale watu wanapochukua fomu, wakajaza, wakaomba masomo, wakasomea hizi fani wanazozihitaji ya kuweza kumchunguza mto mmoja mmoja kujua tabia yake. Sasa nadhani labda kwa kushirikiana na nyinyi viongozi wenzetu, tutafute mbinu ya kuona tutafanya nini katika kuona tunaowaajiri au kuwachukua katika taasisi zetu hizi za kuanzia kusoma mpaka kuajiriwa, basi tunaangalia na tabia zao labda hilo litatusaidia.

Lakini matatizo ya kibinadamu Mhe. Spika, yapo na haya hayaepukiki kila mmoja ana tabia yake. Sasa wengine zile tabia alizokuwanazo kuzirekebisha ghafla pamoja na kuwa tuna *ethics* zetu, tuna mabaraza yetu, tuna kila kitu, lakini bado wengine wanakuwa watukutu. Sasa Mhe. Spika, mengine huwa tunasema japokuwa mnasema hili ni lenu mlifanyie kazi nyinyi, sisi hatuwezi kufanya hilo, lakini katika maeneo yote nasema shughuli zetu hizi lazima kusaidiana. Tunaposema kuwa serikali yetu ni yetu sote, basi tunapoona mapungufu katika taasisi zetu zozote zile kuna haja ya kusaidiana. Tunajua siku fulani, tarehe fulani na saa fulani aliingia mgonjwa mahali fulani na likatokea tatizo fulani tusaidiane Mhe. Spika, sisi hatutokuwa saa zote tunayaona yale.

Tumeshauriwa kuwa tuwe tunakwenda kwenye taasisi zetu, tunajitahidi Mhe. Spika, tunakwenda na tunapita, lakini pengine wewe utapokwenda kwa bahati yale yanayotendeka usiano na haya yakawa yanatendeka kwa wenzetu ambao wanafanyiwa mambo yale. Kwa hivyo, tunasema bado tunahitaji ushirikiano, yale yote ambayo yanafanyika ni maovu kwa upande wa watu wetu wanaopata huduma tusaidiane Mhe. Spika, kwa kupeana taarifa.

Hapa kuna mjumbe kuna siku aliniambia kwamba kuna madhila aliyoyapata mama mjamzito pale wodi ya watoto kwa kuwa hakufanyiwa operesheni,

alipofika pale alifanyiwa operesheni lakini kiwango alichotozwa sicho ambacho tumepanga. Kwa hivyo, lililofanyika amekuja kunieleza na tukatoka hapo hapo mguu kwa mguu tukenda kulishughulikia. Sasa na mengine yote yale yanayotokea kama haya tunapopata taarifa kama zile tunachukua *action* hapo hapo kwenda kufuatilia hili jambo. Kwa hivyo, mimi ningeliwaomba wenzetu wasiona kwamba ni wajibu wao wayatafute, wayafanye.

Halafu pia kulikuwa na mjumbe mwengine humu humu tena alikuwa mjumbe wa kamati, ilitokea kesi nyengine Mkoani Pemba akanieleza shida zake tulikuwa ndani ya kamati, nimekwenda kuzifuatilia mpaka animejua undani wake. Kwa hivyo sisi kama tunavyosema Mhe. Spika, ni wasikivu. Wenzetu tu, tunataka wawe karibu na sisi wasione kuwa hili lao ndio lao na sisi basi tunafanhiwa madhila haya iko siku tutasema. Tuseme pale linapotokea lile jambo ili tuweze kulichukulia hatua. Ningeomba sana Mhe. Spika, kwa hilo.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa ilani kasema pamoja na mapungufu, lakini kama yapo ni machache. Tulipokuwa tunaangalia na wasimamizi wetu wa Ilani ya Chana chetu cha Mapinduzi wakati tunaipitia ni asilimia 97.5 tuliyoitekeleza. Kwa ule utaratibu kwa miaka mitano hii tuliyopangiwa, labda kama tumekosa hio 2.3 tu, kwa mapungufu ya kibinadamu, lakini kwa yale tuliopangiwa tumefikia hatua kubwa kweli katika utekelezaji wa ilani yetu.

Kwa sababu sisi tulitakiwa tuiboreshe Hospitali ya Mnazi Mmoja na tumejitahidi Mhe. Spika, kadiri ya uwezo wetu hospitali hii tumeweza kuiboresha. Tumetengeneza maabara, tumeweka vifaa pale japokuwa vilipata hitilafu lakini baadae vilitengenezwa sasa hivi inaendelea vizuri. Tumetengeneza *ENT* pale kwenye koo, pua na masikio, palikuwa hapana huduma ya *theater* pale ya kuhudumia wagonjwa sasa hivi hali nzuri, tumetengeneza *Eye clinic*.

Eye clinic sasa hivi ni kitengo ambacho cha sifa sana mpaka vifaa Wachina wametuletea vya kisasa katika utaratibu wa kusafirisha wagonjwa wetu kwenda kutibiwa macho katika maeneo mengine limepungua hilo. Phisioferapy ilikuwa hata kuitizama Mhe. Spika, ulikuwa huwezi, lakini Mwenyezi Mungu katujaalia tumeweza kuitengeneza. Kama nilivyosema *maternity* imetanuliwa na mambo mengine.

Huduma ya *ultra sound* ulikuwa huwezi kuipata katika Hospitali ya Mnazi Mmoja watu wapelekwe Dar es Salaam au kwenye hospitali za watu binafsi. Tumejitahidi tumefika hapo. *X-Ray* za kisasa tunazo, *CT Scan*, mambo chungunzima, hiyo imo katika ilani ya uchaguzi katika kuiboresha Hospitali ya Mnazi Mmoja na hayo tumeyafanya na wenzetu hapo mmeyataja. Kwa hivyo,

katika kipindi hiki cha miaka mitano sisi tuliopo tumejitahidi kweli kweli kuona mambo hayo yamefanikiwa.

Lakini katika huduma za vituo vya vijijini nayo tumejitahidi, yamo katika ilani yetu kuboresha huduma hizo, tumejitahidi kuboresha huduma hizo na moja wapo tulilolifanya kuvijenga vituo vile vya kisasa kama vile vya *second line*, vilivyoko vya zamani tumevifanyia ukarabati na kubwa katika kuona kuwa tunapunguza vifo vya mama na watoto kama alivyosema Mhe. Omar Ali Jadi pale suala aliloliomba, mimi nadhani hili tayari tumeshajitahdi tumelitekeleza katika jimbo lake la Kojani hasa kule wanakovuka. Tayati tumeweka kituo cha *second line*, kinamama watajifungulia pale, wodi iko pale.

Mhe. Spika, Kojani mimi mwenyewe nimekwenda si chini ya mara tatu nimevuka kwa kwenda kuangalia hospitali tu ile na kweli tuliwaambia kuwa tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu itajengwa na imejengwa.

Kwa hivyo, katika suala la kuboresha vijini hilo tumelifanya na kuanza kuboresha vituo vya afya kwa kuviongezea nguvu ili watu wapate huduma kwa ukaribu zaidi, lakini kubwa zaidi ni lile la kujenga nyumba za madaktari ili waweze kukaa katika maeneo yale kuwapatia huduma wananchi hasa hao wakunga na ndio maana tunaanzisha fani mbali mbali za chuoni pale na tukaitilia nguvu hii fani ya *PHNB* ili wakunga hao wapate kusoma kwa haraka na kuweza kumaliza na kwenda kuhudumia katika maeneo yetu. Nyumba hizi tumezijenga kwa kweli kupunguza vifo vya akinamama ili nyumba hizi ziweze kuwasaidia watu wetu wa vijijini, wakae pale wakunga na waweze kutoa huduma hiyo. Kitu kilichotucheleweshe hapa mazingira.

Unguja sasa hivi baadhi ya nyumba tushakabidhiwa na nyengine karibu tutamaliziwa, lakini kilichotucheleweshe kwa upande wa Pemba ni katika suala zima la mazingira. Nilizungumza na mkandarasi anayeshughulikia nyumba zile juzi kanambia kutokana na mahali ya mazingira ya Pemba na hali ya mvua na maeneo mengine magumu kijografia kuvuka na nini ndio zimechelewa. Lakini anasema atajitahidi kadiri awezavyo kati ya mwezi huu na ujao ziwe zimemalizika aweze kutukabidhi. Kwa hivyo, tunaamini nyumba zitamalizika na wakunga wetu tunajitahidi kuwasomesha pindi nyumba zikimalizika basi waende wakakae.

Mhe. Spika, bado narudia tena kumuomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kuwa asiende kutafuta *rain boot*, hakuna lisilozungumzika, mengi wametueleza tumejitahidi kuyatekeleza. Kwa hivyo, namuomba sana, sana, hili alilotwambia tutalifanyia kazi na ikiwezekana baadae kama kutakuwa na ripoti kujua ilikuwaje? Ikafikiaje? Tutafanya hivyo na tutaweza kumuarifu, lakini

asitupigie buti kiasi ambacho alichotaka kutupigia na tumauomba sana yeye na wajumbe wenzake atuunge mkono sana wizara yetu hii.

Tunajua kwamba wizara yetu bado hali ya kifedha sio nzuri, sasa mkitupigia buti hata hii hatua tuliyofikia itatuwia ngumu. Kwa hivyo, tunakuomba sna suala hili utustahamilie kama unavyotueleza mengine na haya tutajitahidi. Umezungumza suala la Hospitali Wete tangu tulipotoka kwenye kikao cha kamati pale hospitali suala la kupatikana daktari, *gynaecologist* na *surgeon* tunalifanyia kazi usiku na mchana mpaka hii leo. Tumeshajitahidi kuzungumza na wenzetu wengi wanaofika pale wizarani kuwaomba kuwa suala hili liweze kufanikiwa. Hivi sasa tumeshawaomba watu wa *WHO* washasema watafanya kila njia watusaidie na wataharakisha sana waweze kutuletea huyu mtu wa *gynaecologist* halafu suala la taji liweze kufikia baadae.

Kwa hivyo, Mhe. Abubakar Khamis Bakary tunataka kukuthibitishia kwa kuwa tunakusikia na tunaelewa.
Nilikuwa na mengi ya kutaka kumsaidia Mhe. Waziri, lakini sasa naomba niyaache kwa sababu Mhe. Spika, ananihimiza. Mhe. Waziri atakuja kuyaelezea yaliyobakia, lakini nataka kusema kuwa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe mtuunge mkono sana.

Samahani Mhe. Spika, labda hili suala moja limenigusa ambalo amelizunguzma Mhe. Amina Idd Mabrouk suala la shilingi 40 elfu na kusema pale yupo Naibu Waziri mwanamke haoni uchungu? Mhe. Spika, mimi ninaujua uchungu na hali ya uchungu ninaielewa vizuri, lakini kutokana na hali tuliyokuwanayo Mhe. Waziri atakuja kuzungumza zaidi, lakini wataalamu wetu wanatwambia kutokana na hali yetu tuliyokuwanayo sasa hivi mambo yetu tunayokwenda nayo tunayopata misaada kuna hatari tukizitoa fedha hizi. Tatizo kubwa tusisahau jamani tumetoka wapi, tulikotoka ilikuwa mtu pale hawezi kufanyiwa operesheni mpaka vifaa avilete, hatua tuliyofikia sasa hivi mtu anafanyiwa kwanza halafu ndio anaambiwa alete hizo fedha.

Sasa kama kuna kauli zinatolewa pale na kuwa hapa hufanyiwi mpaka sisi hizo tutazifuatilia, lakini nasema hata hivyo sio mwisho wa safari, sisi bado tutakuwa wasikivu, tutawasikiliza na ikibidi tena huko siku za mbele Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi mwenyewe wa jumla. Kwa sababu mimi jana sikuwahi kushiriki siyajui hayo makubwa zaidi waliyozungumza huko ndani kutokana na kazi nyengine kubwa tuliokuwanayo, lakini waziri atakuja aelezee zaidi kutokana na jana walivyokaa na wataalamu kulijadili jambo hili atakuja kuelezea zaidi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nitamke kwamba, mimi mwenyewe na wananchi wa Jimbo la Dole tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana, tunakushukuru Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na zawadi yako inakuja muda mfupi ujao hii hapa. Nimejaribu kuangalia hapa chini *rain boot* sijaiona, lakini kuna kijana hapo nje anatembea tembea sijui ndiye aliyetumwa. Hatari ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary anakaa hapa jirani tu, anaweza akawahi akenda akavaa baadae akaja, lakini amesikia. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii fanya majumuisho taratibu, polepole na kwa uwazi na kwa ufupi. Nakusudia kwamba Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji asome kipindi hiki cha asubuhi ili jioni tupumzike bwana. Kwa hivyo, ukisema kwa ufupi itasaidia sana na makofi hayo wajumbe wamekubali jioni tupumzike. Endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza natoa shukursani kwa Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao yote waliyoitoa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa heshima naomba niwataje Waheshimiwa waliochangia hotuba yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii)
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Haji Faki Shaali
6. Mhe. Said Ali Mbarouk
7. Mhe. Moh'd Ali Salim
8. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
9. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
10. Mhe. Salmin Awadh Salmin
11. Mhe. Salim Abdulla Hamad
12. Mhe. Assaa Othman Hamad
13. Mhe. Ali Abdalla Ali
14. Mhe. Zahra Ali Hamad
15. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman
16. Mhe. Ali Denge Makame
17. Mhe. Najma Khalfan Juma
18. Mhe. Asha Moh'd Hilal
19. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
20. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

21. Mhe. Subeit Khamis Faki
22. Mhe. Omar Ali Jadi
23. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
24. Mhe. Ali Moh'd Bakari
25. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
26. Mhe. Shawana Bukheti Hassan

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe watano walichangia kwa maandishi, nao ni hawa wafuatao.

1. Mhe. Fatma Abdulla Tamim
2. Mhe. Mzee Ali Ussi
3. Mhe. Ashura Abeid Faraji
4. Mhe. Ame Ussi Juma
5. Mhe. Ame Mati Wadi

Mhe. Spika, kwanza ninawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote kwa michango yao mizuri sana na michango yote tunaithamini sana tumeipokea na tunaikubali.

Mhe. Spika, kwanza kwa ujumla *scheme of service* mishahara hivi sasa ni tayari kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na tumeipeleka kulikohusika nako ni Idara ya Utumishi.

Kama yatatokea maelezo zaidi waheshimiwa watataka kujua kuhusu habari hizi, basi naomba Mhe. Spika, kwa ruhusa yako Waziri anayehusika wa Fedha anisaidie kwamba tumefikia wapi mpaka leo fedha wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hawajapatiwa malipo yao mepya ya *scheme of service*. Mhe. Spika, kwangu mimi ni vigumu kujibu hoja hii, kwa hivyo nitaomba msaada kwa waziri husika nae ni Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, kuhusu shilingi 40,000 za upasuaji wa kuzaa. Kwanza tunawapongeza waheshimiwa wote waliopendekeza kwamba fedha hizi ziondoshwe. Sisi Mhe. Spika, tunaungana nao waheshimiwa wote kabisa na wala hatuna pingamizi. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spika, jana najua wewe ulikuwa Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui, mimi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wataalam wote wa wizara yetu tulilizungumza sio kwa dakika kwa masaa suala hili mpaka tukasahau michango yote iliyochangiwa na waheshimwa. Tumelijadili, tumejadili, nitaeleza tulivyolijadili.

Mhe. Spika, tulianza katika hali ngumu ya upatikanaji wa fedha na vifaa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kiasi ambacho ilitubidi hata kuchangisha shilingi 1,000 kwa kila mzazi anayekuja hospitalini lakini sasa halipo. Tuliweka mchango unaoitwa upatu maridadi. Mimi nilipoingia pale nilikuwa Naibu Waziri, Waziri aliyenitangulia wala sio siri nitasema Mhe. Spika. Tukapanga tuchangie shilingi 10,000, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wachangie shilingi 5,000, wafanyakazi wachangie shilingi 1,000 Mnazi Mmoja. Katika mazingira ya mshahara ule ilibidi tufanye hivyo lakini sasa hakuna.

Hali ya uzazi na upasuaji ilikuwa haifahamiki pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa ufupi ni kama biashara, shilingi 100,000, 150,000, 200,000, mifuko ya rambo, mifuko ya *plastic*, biashara iliyoingia *maternity* haijulikani. Tukafika pahala mimi waziri tukasema hapana tudhibiti jambo hili, tutadhibiti vipi, serikali ichangie shilingi 60,000 na mzazi anayekuja mwenye uwezo na si lazima atoe chochote, tuweke angalau shilingi 40,000.

Mhe. Spika, uzazi wa upasuaji tunaita ni *emergency* yaani operesheni wa dharura. Kwa mfano, mtoto akikwama, au ikitokea mapigo ya moyo ya mtoto mabaya, au kifafa cha mimba, mtoto akilala ubavu, kutokwa na damu nyingi, inatayarishwa pale pale mama mjamzito anapelekwa *theatre* timu inakaa tayari anafanyiwa hali ya *emergency operation* hakuna kuuliza pesa.

Mwaka 2007 vifo vilikuwa 468 katika watu laki moja. Mhe. Spika, tukapunguza mpaka tumefika 281 mwaka jana na bado tunaendelea na harakati za kupunguza na tutapunguza. Mhe. Spika, wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wamepania kweli kweli.

Mhe. Spika, bajeti ya Hospitali ya Mnazi Mmoja mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 268, tulichopatiwa ni shilingi milioni 132, mwaka huu bajeti imepunguzwa. Tuliwekewa mwaka jana shilingi milioni 268 tumepatiwa chini ya asilimia 50 shilingi milioni 132. Mwaka huu imepunguzwa tutapewa shilingi milioni 180 kasoro milioni 88.

Mhe. Spika, Mhe. Zahra Ali Hamad alifanya hesabu ya haraka haraka kama za kupasua 1,000 yeye akapata kama 43 milioni, sio 43 milioni mimi nakuchangia. Ikiwa tutafanya operesheni pale za kupasua 1,000 tutahitaji kama utaondosha shilingi 40,000 itakuwa milioni 100. Bajeti yangu mimi sasa hivi shilingi 180 milioni.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija anataka *reagents* za *laboratory*, *laboratory* kuiendesha kwa mwezi milioni 5 inatakiwa, tuna vifaa vya kisasa, vyombo vya kisasa, shughuli zimechangamka pale, maabara vitu tele wanataka milioni 5

kwa mwezi hatuna. Fanya 5 mara 30 inatakiwa milioni 150 kuiendesha maabara, kuendesha *maternity* na sehemu nyengine.

Tutaweza kukabiliana na hali halisi ilivyo tukiondosha shilingi 40,000? Hofu iliyowaingia wataalam wote tusije tukarejea tulikotoka. Kila aliyesimama jana Mhe. Spika, sote tunataka ziondoke, lakini wataalam wote hofu imewaingia tutarejesha tulikotoka. Daktari ukimwita pale akiambiwa mgonjwa anataka operesheni shughulikia vifaa, atasema mtakapokuwa tayari mimi niiteni. Pia akifa hutoambiwa kafa kwa sababu hakuna *caesarean kit*, utaambiwa aaa kafa kifafa cha mimba, hutoipata jawabu hiyo.

Mhe. Spika, *kit* moja ni shilingi laki moja. Mhe. Spika, tukivamia ni hatari, hivi sasa tuko katika hali ambayo nzuri tunakwenda vizuri. *Average* ya upasuaji kwa siku tunayofanya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni baina ya tano mpaka kumi, katika tano, tatu lakini kumi ndio nyingi. Mhe. Spika, msamaha upo, ushahidi huu naomba nikukabidhi. Hatuwezi kumpa kila mtu ushahidi huu kwa sababu ni siri ya wagonjwa, *ethics* zinatuzuia. Lakini ukitaka nenda kwa Mhe. Spika, akuoneshe, msamaha upo. Tumeweka kitengo maalum cha kusamehe watu ambao hawana uwezo.

Mhe. Spika, tupo pahala pazuri hivi sasa lakini tukifanya pupa tutarejea tulikotoka. Hiyo ndio hofu tuliyokuwanayo. Maamuzi Mhe. Spika, mimi la kulisema sinalo. Mzazi hadaiwi wakati wa operesheni huombwa baaade, kama hana basi hakuna ulazima. Mhe. Spika, hii ndio hali halisi.

Mhe. Spika, Chuo cha Afya Mbweni mwaka huu wanafunzi waliopitishwa na Baraza walikuwa 326, wanafunzi ambao ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii walikuwa 26, jumla ni 352. Wanafunzi waliorejea mwaka kielimu 43, wanafunzi waliorejea kwa sababu ya kinidhamu 24, wanafunzi walioahirisha kabla na kurejeshwa 19, jumla 440. Mhe. Spika, wanafunzi wote hawa tumeambiwa wana sifa.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nimeambiwa nikwambie kama Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wanataka kuja kufanya ukaguzi tunawakaribisha na hatuna tatizo lolote, wakati wowote. Lakini tunaomba Baraza la Wawakilishi liwawezeshe.

Mhe. Spika, uvamizi wa eneo la chuo, hatimiliki ya chuo tuliyonayo hivi sasa ni mpya na haina matatizo yoyote, eneo letu tulilokuwanalo ni salama. Uzio wa chuo Mhe. Spika, jitihada za ujenzi tutaziendeleza.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwa Mhe. Ali Suleiman Ali ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, pongezi

tumezipokea. Upungufu wa daktari wa *CT Scan* hivi sasa tumepata daktari bingwa *Radiologist* anaitwa Salim Ismail Salim amekwisharudi masomoni kutoka *Nairobi Kenyatta University,* atashirikiana na daktari bingwa wa Kichina ikiwa tatizo hilo lipo.

Kupatiwa nafasi maalum za mafunzo Chuo cha Afya Mbweni Vikosi vya SMZ safari hii tumewachukua wanafunzi watano ambao wana sifa. Mengine yote uliyotupa tumeyachukua na tumeyapokea.

Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pongezi tumezipokea. Afisa Mdhamini aliyepo Pemba ni mfanyakazi mwenye uzoefu wa kutosha, taaluma, muadilifu na anashirikishwa vikao vyote. *Outreach* wazo la kuwasaidia madaktari wetu tumelichukua na tutawasaidia. *ICU* Pemba tumo katika jitihada na inshaallah tukifanikiwa itakuwepo.

Mhe. Spika, wagonjwa wa akili Wete Pemba. Inavyotakiwa hivi sasa ni kuwa wagonjwa wa akili wawepo hospitalini na wasitengwe *(integrated services).* Kwa mfano, Hospitali za Muhimbili, Bugando, Mirembe, *Nairobi Kenyatta University,* kote sasa hivi wagonjwa wa akili wanakuwepo katika hospitali kuu. Kwa hivyo, Pemba usiwe na hofu watakuwepo *Wete Hospital.*

Mhe. Spika, idadi kamili ya wazazi waliofanyiwa upasuaji *Mnazi Mmoja Hospital* ni 1,091 na sio 2,572, ni sawa sawa na asilimia 14.65. *WHO* inataka iwe baina ya 5 mpaka 15, kwa hiyo tuko katika *range* ya *WHO*.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pongezi tumezipokea. Kufunga milango yote ni hatari. Ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi kuondosha usumbufu huo. Mpango upo wa kuweka lifti mpya. Hospitali ya Macho kitengo sasa hivi ni kidogo matatizo ya macho ingawa yapo. Lakini sasa wananchi wamekuwa na mwamko mkubwa, tunapata wananchi kutoka Tanzania Bara, Mafia, Kilwa, Lindi, Mtwara na hata kutoka Comoro. Wagonjwa wa macho *Mnazi Mmoja Hospital* Mhe. Spika, wameongezeka sana bila ya kiasi kwa sababu ya huduma bora na daktari bingwa Dk. Ji kutoka China. Kwa hivyo, sasa hivi hata kile kijumba kinaonekana kidogo kwa sababu tuna vifaa vizuri vya kisasa na kaletwa daktari hodari.

Wafanyakazi wa *x-ray* wanavaa *doors meter* kupima mionzi. Ikifikia kiwango anasimamishwa zinapelekwa Arusha Tanzania *Atomic Energy Commission* kupima mionzi zile nguo zao. *Safety Officer* yupo anaitwa Mr. Maulid Mjaka tahadhari zinachukua. *Ultra Sound* zinaendelea kama kawaida na ile iliyoharibika kioo tutakitengeneza.

Kisukari sasa hivi kliniki imekuwa ndogo, ushauri tumeupokea. Kwa sababu huduma zetu zimekuwa nzuri, taaluma imekuwa nzuri, watu wanafahamu afya zao, wagonjwa wa kisukari wanaongezeka, ni kweli kabisa.

Idara ya Ustawi wa Jamii. Kuhusu mtu ambaye hana mtu kwanza tunatoa pole kwa msiba na yaliyotokea. Mtu yeyote ambaye hana mtu huwa tunampokea tunampeleka Welezo na kumtazama kwa kula, kulala, nguo na kadhalika. Lakini nimeambiwa mgonjwa huyu ilibidi kwanza kupata matibabu. Nilivyoambiwa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii kwamba ma-*sister* walikuja kumtazama wakasema mgonjwa huyu bado hakutibika na wauguzi.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wanisikilize vizuri, mgonjwa yule marehemu pale hospitali ilikuwa hali yake si nzuri, maana yake mambo mengine yalikuwa haifai kusema sema na yeye ndio ameshakwenda mbele ya haki. Lakini ushauri wako tumeupokea na tutajitahidi kuufanyia kazi.

Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu *reagent*, mahitaji ya maabara sasa yameongezeka, kwa kweli hata *reagents* zitahitajika kwa wingi sana. Maabara imekuwa ya kisasa vipimo vingi vinapimwa badala ya kwenda Dar es Salaam. Ushauri wako tumeuchukua na tutajitahidi kuongeza *reagents* katika maabara ya *Mnazi Mmoja Hospital*. Wafanyakazi kweli ni kidogo pia tutajitahidi kuongeza wafanyakazi wa maabara.

Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu *HB* wataalam wamenambia 15.6 iliyopewa *Mnazi Mmoja Hospital* hii ndio kawaida. Ile 9.6 iliyopimwa *private hospital* haina haja ya *blood transfusion, quality control* ndio muhimu na wizara yetu itafuatilia jambo hili.

Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu malaria ulisema kwamba malaria ipo haijapungua tunamfurahisha mtu. Sisi hatumfurahishi mtu, ukweli malaria imepungua na wala hatujasema malaria imeondoka, iko chini ya asilimia moja. Kwa hivyo, malaria unaweza ukapata, hatujasema malaria imeondoka nchini.

Mhe. Spika, mafuta ya kupikia chipsi tumeambiwa kwamba ni mafuta ya *transformer*. Mhe. Spika, wizara tumelipokea suala hilo na wahusika watalifanyia kazi watapita kukagua mafuta yote yanayopikiwa chipsi. Kuanzia jana tumeshawaambia wachukue hatua za kufuatilia jambo hili.

Mhe. Spika, matunda Tanzania Bara yanachunguzwa na Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Suala la nzi hili tutashirikiana na Baraza la Manispaa kwa sababu wao ndio wanaoshughulikia usafi wa mji.

Mhe. Haji Faki Shaali Chuo cha Afya Mbweni sahihi ni ipi cheti, diploma au stashahada. Nimeambiwa *certificate* kwa Kiswahili ni cheti, diploma kwa Kiswahili nimeambiwa stashahada.

Mhe. Spika, Hospitali ya Abdulla Mzee ni kweli hali yake si nzuri tutalishughulikia jambo hili kutafuta aidha wenyewe serikalini au nje ya nchi kutusaidia matengenezo. Lakini tusisahau kwamba ile hospitali imejengwa na wenzetu wa Kichina na tumeshawaambia tumewaomba, lakini wamesema kwanza wataanza nyumba zao wanazoishi wao, baadae wataangalia uwezo wa kuifanyia matengenezo hospitali ile, lakini hawakutuahidi wamesema tu.

Kuhusu daktari wa meno tumeambiwa Dk. Juma Rashid yupo sasa hivi ni mzoefu wa muda mrefu na *Red Cross* hawafanyi kazi ya matibabu, wao wanafanya kazi za *orderly*. Kiambatanisho 6.4 Chake Chake mbona wamekufa watu 7, Wete mbona hamna. Nimeambiwa kwa sababu Chake Chake ni kama *referral*, wagonjwa wanachukuliwa *referral* kutoka Wete wanapelekwa Chake Chake. Inawezekana pengine wa Wete wamekufa Chake Chake kwa mujibu wa takwimu hizi ingawa hazijaonesha.

Elimu ya Afya itolewe kupitia maskulini tumepokea na tunafanya hivyo. Afya bandarini, suala la vyoo vichafu melini, mende, uchafu na mambo mengineyo ushauri tumeupokea tutashirikiana na wanaohusika.

Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi imekuwaje bandarini dawa zenye matatizo zinaingia nchini. Tutajitahidi kuzidisha juhudi za ukaguzi. Supu yenye kutia nguvu tumetoa taaluma lakini tumekamata watu wanaotia dawa za kuongeza nguvu, wakiendelea safari hii tutawapandisha Mahakamani mbele ya sheria. Mhe. Spika, nimetajiwa supu ya Mkunazini jirani zangu wamegundua kwamba inatiwa dawa za kuongeza nguvu za kiume, wamegundua maziwa yanayouzwa haya yanayochanganywa na tende na vitu vyengine na wameshawakamata, wameshapima na wameshawapa onyo. Wakiendelea safari hii wakigundua tena watapandishwa Mahakamani.

Mhe. Said Ali Mbarouk pamoja na Mhe. Abubakar Khamis Bakary kuhusu fedha za tiba Unguja na Pemba. Mhe. Spika, ni kweli tumefanya kosa katika kitabu chetu kuna baadhi ya mambo yanayoshughulikiwa na tiba hatukuonesha.

Kwa mfano, Idara ya Tiba Unguja inashughulikia pia fedha zake kusafirisha wagonjwa nje ya nchi. Damu Salama *(Blood Bank)* iko katika tiba ya Unguja. Ununuzi wa madawa ipo katika tiba ya Unguja. Tiba ya Unguja pia inatumia fedha zake katika Chuo cha Udaktari wa Wanafunzi wa Cuba Unguja na Pemba. Wagonjwa wa Pemba wanaokwenda nje ya nchi inabidi mfuko wa tiba Unguja utumike. Kwa hivyo, fedha Unguja zimekuwa nyingi kwa sababu

nyengine zinatumika Pemba. Mhe. Spika, fedha zote safari hii zimepungua kwa kila idara ikiwemo tiba Unguja, tiba Pemba.

Kuhusu mafuta nimeambiwa Unguja milioni 3, Pemba milioni 7.92 ukurasa wa 289 kwa Unguja na 291 kwa Pemba. *Spare part* Unguja laki mbili, Pemba hakuna, lakini nimeambiwa ndio wenyewe walivyotaka Pemba. Mhe. Spika, wenyewe wananisikia pale. Mgao huu wanashirikishwa hata wale wahusika wa Pemba na Unguja. Wa Unguja wanasema safari hii kitengo hichi msitutilie, jana nimeambiwa Unguja wanasema tutilie. Kwa hivyo, Mhe. Abubakar Khamis Bakary ikiwa pametokea matatizo tunaomba samahani na tutayasawazisha kwa bajeti ijayo. Hatuna nia mbaya ya ubaguzi, sote ni wamoja na sote ni ndugu. Tutaendelea kupokea ushauri kwa ustawi wa afya bora za wananchi wetu.

Mhe. Spika, kila tunachokifanya Unguja na Pemba tunakifanya. Masomoni tunawapeleka, fedha tunawapelekea, wakiwa na upungufu wa mahitaji zinatoka Unguja fedha kwenda Pemba. Kila kitu tunawafanyia hakuna ubaguzi. Kwa hivyo, Mhe. Abubakar Khamis Bakary nia yetu sisi tuko safi kabisa.

Mhe. Moh'd Ali Salim shukrani tumezipokea. Hesabu ya Idara ya Ustawi wa Jamii nimeambiwa ni asilimia 76 na sio 20. Pia Hospitali ya Abdulla Mzee ipatiwe mafuta tumelipokea ombi hilo tutawapatia. Wodi ya watoto ijengwe, tutajitahidi kuijenga ingawa siku nyingi. Upungufu wa wafanyakazi tutalishughulikia kwa hospitali ya Abdulla Mzee. *Red Cross* wasitibu, ni hakika wanatakiwa wafanye kazi za *orderly* na hawaruhusiwi hasa kutibu. Ubovu wa hospitali tutaushughulikia. *PHL* (Maabara) ifanye *culture sensitivity* na inafanya hivyo, inafanya *TB*, *cholera* na *typhoid*.

Idara ya Mipango na Sera wauguzi waendelezwe kama wengine. Kwa mfano, wapatiwe *degree*, tumeshawapatia sasa hivi wengine wana *degree*, wana *masters degree* wauguzi hao. Kwa hivyo, kuna taaluma kubwa kubwa tu. Mengine yote Mhe. Moh'd Ali Salim tumeyapokea.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pongezi tumezipokea. Chuo cha Afya kiwe *university*, ushauri tumeupokea na *inshaallah* kitakuwa *university*. *ICU* sasa ni ndogo ijengwe kubwa, ushauri tumeupokea. *Orthopaedic Unit* ni ndogo ijengwe kubwa, tumepokea. Maabara pia haitoshi ijengwe nyengine tutajenga *inshaallah*. *Eye Clinic* ndogo, tumekubali. *PHL* ipatiwe milioni 30 kama tulivyokubaliana na wenyewe Wataliana tutajitahidi tutawapatia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis alisema malaria imepungua lakini darubini zina matatizo, labda zina *virus*. Mhe. Spika, darubini huwa na *fungus*, wakati

mwengine *fungus* wanakula kioo hata matokeo yake unapata pengine matatizo. Tumelichukua na tutalishughulikia.

Kuhusu kichocho mradi pia ushughulikie makonokono. Mwenyewe amekusikia jana na leo tumemwambia alishughulikie jambo hilo. Makonokono yote yafanyiwe kazi. Mkuu wa Kichocho ni Dk. Khalfan, ameniambia kwamba wewe ni mwalimu wake na unakuja mradi maalum wa kushughulikia mambo hayo ya makonokono. Kwa hivyo, *Inshaallah* kwa Unguja na Pemba watafaidika.

Mhe. Spika, kuhusu hospitali ya Konde ipatiwe daktari. Tutawapatia na hospitali itakuwa nzuri ya kisasa. Kuhusu afya Ungi. Je, umepokea barua kutoka kwa Mkuu wa Mkoa. Mhe. Spika, nimepokea barua na tutaifanyia kazi.

Mhe. Salmini Awadh Salmin wa magomeni, pongezi tumezipokea. Uliuliza usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi fedha hizi zipo katika bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii au mfuko mkuu wa serikali. Hizi ni bajeti za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, milioni 371, lakini ni kidogo. Kwa hivyo, wakati mwengine tunahaulisha baadhi ya vifungu kulipa ziada.

Je, wagonjwa wanaorudi wanaofanyiwa matibabu ya figo wapatiwe dawa. Nimeambiwa kwamba dawa zao zinaitwa emuno supresa zinapaatikana Tanzania Bara na tumejitahidi baada ya kufanya mazungumzo na katiba mkuu wetu na *chief pharmacies* wa Tanzania Bara, kuna wagonjwa kama wawili wanapatiwa dawa hizi. Kwa hivyo, na sisi tukipata uwezo tutaziweka hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, ilizungumzwa kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja tujitahidi na usafi. Tutajitahidi na mwenyewe Mkurugenzi ameshasikia na *inshaallah* itazidi kung'ara Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kuhusu Umeme wa *generator* anayewasha awepo. Ushauri tumeupokea. Kuhusu mradi wa uhifadhi ya matengenezo ya nyumba za wazee Sebleni. Mhe. Spika, bajeti safari hii imetenga milioni 100. Lakini tufahamu kati ya milioni 100 ni milioni 50 tu ndio matengenezo ya nyumba za Sebleni na milioni 50 zitakuwa ni hifadhi ya wazee na miradi yao, kama walivyoomba wenyewe wazee walipokutana na Mhe. Rais pale kwenye hoteli ya *ocean View*. Kwa hivyo, matengenezo ya nyumba za Sebleni ni milioni 50.

Wagonjwa wanakatwa miguu ambao ni *diabetic cases.* Kweli wakati *complication* zinapozidi. Kuhusu kiwanja cha Binguni *referral hospital*, hii ni vipi. Hii tunasema ramani tayari lakini bado hatujakuwa na uwezo wala hatujapata mtu wa kuweza kutusaidia katika ujenzi.

Mhe. Salim Abadalla Hamad wa Jimbo la Mtabwe, pongezi tumezipokea na ufafanuzi wa viambatanisho tumezigawa na Uwondwe hamna daktari. Suala hili tumelipokea na tutalishughulikia.

Mhe. Assaa Othman Hamad wa Jimbo la Wete pongezi kwa madaktari wa Wete tumelipokea mheshimiwa. Kuhusu Hospitali ya Wete tutajitahidi kulishughulikia. Juzi tumefanya mazungumzo na mkuu wa WHO wa Tanzania Dk. Shatora ili atupatie daktari maalum wa wazazi katika Hospitali ya Wete, amelichukua ombi letu na atalifanyia kazi.

Vile vile tumezungumza na Balozi mdogo wa Misri kutupatia madaktari wa Hospitali ya Wete, na yeye ombi letu pia amelichukua. Daktari bingwa hasa wa mambo ya wazazi mwakani anarudi masomoni kutoka *Nairobi University*, na wenziwe wote wamesharudi, lakini yeye tu bado anajiendeleza zaidi na taaluma. Kwa hivyo, tumpe nafasi ili amalize elimu yake. nimeshawaambia wenzangu asije tena akahamishiwa Mnazi Mmoja Hospital, huyu awachwe Wete Hospital. Watu wa Wete wamestahamili kwa muda mrefu. Kwa hivyo, waachiwe daktari wao, sasa hivi taaluma yake itakuwa kubwa na akirudi hapa atakuwa ni daktari bingwa *doctor* wa mgongo. Wenziwe wote wamesharudi kama daktari Marijani amesharudi, daktari Ismail amesharudi na wengineo wamesharudi.

Mhe. Ali Abdalla Ali wa Jimbo la Mfenesini kuhusu ushauri, maelekezo na maombi ya hospitali mbili unaomba usaidiwe na sehemu ya maegesho ya magari katika hospitali ya Mwembeladu itengenezwe pale na nyumba zinunuliwe. Yote hayo tumeyapokea na *Inshaallah* tutayafanyia kazi.

Mhe. Zahra Ali Hamad viti maalum ushauri wako wote tumeupokea. Kwa nini vyandarua vimechelewa. Kwa sababu vilichelewa kufika. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman kuhusu ushauri wako wa madawa ya kulevya, usafi wa chakula, usafi wa mabanda ya kuuzia chakula, elimu ya afya maskulini, wafanyakazi kupimwa na malaria. Mhe. Aziza ushauri wako wote tumeupokea na *Inshaallah* tutaufanyia kazi na tunauheshimu.

Professor Ali Denge Makame wa Jimbo la Amani, kuhusu ushauri wako wote ulioutoa mheshimiwa tunauthamini sana na tumeupokea tutaufanyia kazi. Vile vile na Mhe. Najma Khalfan Juma pia ushauri wako wa Wete Hospital tumeusikia na tumeupokea. Lakini uwezo wa kulivunja lile jengo kwa sasa hivi hatuwezi kulivunja lile jengo. Upimaji wa maziwa, hospitali ya wagonjwa wa akili, taaluma ya vidokezo hatari itolewe kwa akina mama wajawazito, chakula, dawa na vipodozi. Mheshimiwa masuala yako yote tumeyapokea na tuliyajadili jana na kila muhusika amesikia.

Mhe. Asha Moh'd Hilal wa Jimbo la Magogoni. Ushauri wa elimu ya madawa ya kulevya, malaria, kisukari, posho za *oncall* na kauli nzuri za ma-*orderly*. Masuala yote tumeyapokea na wahusika wamesikia ulivyosema Mhe. Mjumbe.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary, maelezo yako yote tumeyasikia mheshimiwa. Kuhusu Mnazi Mmoja kwamba baadhi ya madaktari wanakorofisha sekta ya afya na tuwe makini madaktari wetu, wote wenyewe madaktari wako pale, wakubwa wote wa Mnazi Mmoja Hospital wamekusikia wazi wazi na mimi nitazidi kuwaambia maana yake baada ya hapa tutakutana tena na tena, tutawekana sawa sawa.

Pia kuhusu hospitali binafsi, kuna kitengo kinashughulika na hospitali binafsi. Hii hospitali uliyoizungumza ya Kiponda tutaifanyia ukaguzi na wenyewe wamesikia na tutazidi kufuatilia hili jambo. Kwa hivyo, ushauri wako, maelekezo yako yote tumeyapokea na hakuna atakayedharauliwa, tutafuatilia.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi mambo yote uliyoyaeleza ya mbu na mengine yote uliyotuhadithia tumeyapokea mheshimiwa na tutayafanyia kazi wala hatutodharau hata moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki wa Micheweni kuhusu jengo jipya kuwa umeliona lakini unataka madaktari. Mhe. Subeit Khamis tutajitahidi tukupatie. Kuhusu Micheweni kuna upungufu wa vitanda na magodoro. Daktari dhamana amekusikia na mimi nitamwambia upatiwe magodoro tena mapya na mashuka mapya yote na mwenyewe yupo unamuona hapo. Mbali daktari dhamana mwenyewe daktari wa Micheweni.

Kuhusu mishahara iliyoibiwa Micheweni, nimeambiwa hivi ingawa umesema unamngojea Waziri wa Fedha na Uchumi mwenyewe ndio mtu wako. Lakini nimeambiwa tumezungumza na Wizara ya Fedha na Uchumi kuwa *quarter* ya mwanzo katika mwaka huu kwamba wale wafanyakazi 28 tumekubaliana nao Wizara ya Fedha na Uchumi watalipwa ni milioni 4,800,000 kwa hivyo ni matumainio yangu kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi watatupa hizo fedha.

Maradhi ya kisukari chanzo chake inaweza kuwa urithi au *insulin hormones* ziko chini, hali ya maisha yaani *life style* watu wanakula ovyo siku hizi, mafuta kwa wingi, mazoezi hamna, masukari mengi pia yanasababisha. Kuhusu maadaktari wanatutia aibu. Ushauri wake mheshimiwa tumeupokea na hasitutie tena aibu.

Mhe. Omar Ali Jadi wa Jimbo la Kojani, maelezo yako yote mheshimiwa tumeyapokea na yote uliyoomba tumeyachukua na tutakufanyia. Kuhusu madaktari nyumba zisikae hivi hivi, Hospitali ya Kojani huduma ziwe nzuri.

Zitakuwepo za uzazi, za meno, za maabara na kila ulichokizungumza Mhe. Mjumbe tumekisikia na tumekiandika na tumekipokea.

Mhe. Amina Idd Mabrouk, kuhusu mradi wa afya ya akili, pongezi tumezipokea. Kwa wale wagonjwa wengine wanabakwa na wengine wanaranda ovyo. Basi tutashughulikia kwa kushirikiana na wenyewe wahusika. Kwa sababu inavyotakiwa askari polisi wachukuwe hatua za kuwakamata wale na kutuletea au familia yenyewe ya huyo mgonjwa wa akili imlete hospitali ya wagonjwa wa akili na sisi tutamuhudumia. Lakini tutashirikiana nao na tutawafahamisha wale wanaohusika.

Mhe. Spika, kuhusu kujengwa hospitali kuu ya rufaa. Ramadhi tayari, lakini tatizo bado hatujawa na uwezo. Kuhudu upigaji wa dawa za malaria majumbani. Ushauri wako tumeusikia na mengine yote uliyochangia tunayathamini na tutayafanyia kazi.

Mhe. Ali Moh'd Bakar wa Jimbo la Tumbe, alizungumza kuhusu kitengo cha madawa ya kulevya. Kuna sheria mpya sasa hivi inafanyakazi, tume imeshaundwa, tumeshakaa vikao mbali mbali, polisi sasa hivi tumeshawaambia wachukuwe hatua, mahakama tumeshawaambia watumie sheria mpya. Nafikiri imeshaanza, jana kama mmesikia kwenye taarifa ya habari kuna mtu mmoja tayari ameshakamatwa na ameshapigwa faini na keshafungwa.

Mhe. Spika, kuhusu maradhi ya kichocho pia tutalishughulikia. Vile vile kuhusu afya bandarini. Matunda yote tutayashughulikia kuyakagua na mambo ya kilimo. Mhe. Ali Moh'd mambo yote uliyozungumza tumeyapokea na tutayashughulikia, hata moja hatutolidharau.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla wa Jimbo la Chonga. Kuhusu mambo yote uliyosema kuhusu nyumba za madaktari na tukupatie madaktari. Tutakupatia mheshimiwa. Tatizo la saratani na mambo ya kisukari, yota hayo tutayashughulikia. Pia vyakula viwe salama tunavyokula. Kwa hivyo, bodi ya chakula, dawa na vipodozi itayashughulikia mambo hayo na kuhusu wagonjwa wa akili pia tutawashughulikia. Kuhusu vyoo vya jumla jamala sio letu sisi, suala lile ni la Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima mambo yote ya Waheshimiwa Wajumbe tumeyapokea, tumeyasikia, tumeyaandika na tunaahidi kwamba tutayashughulikia. Kwa yale yaliyokuwa tunayaweza basi tutayatekeleza mara moja na mengine ya kuyafanyia kazi basi tutayafanyia.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa majumuisho ambayo umejitahidi kuyafanya kwa muda mchache kidogo. Basi Waheshimiwa Wajumbe niwahoji Wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/11 wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza imeijadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 24 – WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	604,000
Kifungu 06	Idara ya Kinga	6,049,000
Kifungu 07	Idara ya Tiba	6,238,000
	Jumla ya Fungu	**12,891,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu na kamati ya matumizi vimepitishwa bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Waziri nilizungumza suala la *scheme of service* ya wafanyakazi. Wakati alipokuwa anajibu, alijibu kwamba jitihada kubwa imefanywa na wizara yake, nataka niwapongeze kwa hili.

Lakini alisema kwamba suala hili liko kwa Waziri wa Fedha na alikuomba Mhe.Waziri wa Fedha na Uchumi utowe majibu kwa suala hili. Sasa kwa vile Waziri wa Fedha na Uchumi yuko na hakulijibu suala hili, tunaomba kujua kuwa suala hili limefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Nhci (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri

serikali imetangaza kwamba tuna *review scheme of service* na tunaweka miundo mipya ya *scheme of service*. Tunashukuru Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wao walikuwa wa mwanzo, walikamilisha. Nakumbuka tokea mwaka juzi na tuliwarekebishia mishahara yao na baadae mwaka huu tumekamilisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini tunajaribu kwenda na wakati kadiri hali inavyokuwa, tunatoa vivutio zaidi na tunawapandisha hasa wale madaktari bingwa, ili wajisikie kama mnavyosema wasiruke kwenda nje ya nchi.

Kwa hivyo, *scheme of service* Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni ya mwanzo tumeitekeleza na inakwenda vizuri. Vile vile tunatarajiwa kwenda kwenye zile sekta nyengine ambazo bado. Lakini kwa ujumla unajua mambo yanabadilika kadiri hali inavyokwenda na sisi tuko tayari ku-*review* kila hali inavyokwenda. Ahsante.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi, hajajua anajibu nini. Ni kwamba kwa ujumla kuna tatizo la maslahi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, jambo ambalo kwa kweli na nchi inaathirika mno, wataalamu wanakimbia. Sasa wizara inasema kwamba imeshaandaa *scheme of service* iko mezani kwake kwa utekelezaji. Sasa yeye anatujibu ya mwaka juzi. Sisi tunataka ya mwaka huu ambayo iko wizarani kwake tumefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tunazungumza lugha moja tu. Labda Mhe. Said Ali Mbarouk, kwenda Gando yeye anapita huko kulia na mimi napita huku kushoto, nafikiri tunazungumza lugha moja kwamba sote tunataka tuimarishe *scheme of service* ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nilisema kabla ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kweli mimi nilikuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mhe. Said Ali na wewe unajua, na ndio hilo zoezi nililianzisha mimi tukaanza hiyo kazi. Lakini unapoondoka siku zote huyakamilishi, anajuka mwenzako anaendeleza. Kwa hivyo Alhamdulillah tukayaendeleza na wakapata Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nakumbuka vizuri kabisa. Tuli-*review* mtu kwa mtu, lakini hatukukamilisha. Kwa hivyo, akaja mwenzangu Mhe. Salim Juma Othman akalitekeleza, kaja Mhe Mugheiry akaliendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, unajua kama ninavyosema hili suala halikutulia, kila mara maposho hubadilika, mishahara inabadilika. Lakini lengo ni kuwaweka hawa wafanyakazi wetu katika njia nzuri. Sasa hii tuliyosema ya serikali yote, pia zile *scale* zimepitwa na wakati, nayo tunai-*review.* Kwa hivyo, alivyosema yeye kwamba kweli iko sasa mpya na imeshawekwa na tunaikubali kuwa ipo

tayari tumeshaanza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hiyo tutaipitia upya kwa ajili ya kuirekebisha kutokana na hali ilivyo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi na majibu yake. Lakini majibu yake yamenipa hofu kwamba kumbe wataalamu wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii sasa tuwape nafasi ili watukimbie zaidi. Maana yake ni kwamba ndio kwanza wanaitizama, kwa sababu tulitegemea kwamba sasa iwe imetekelezwa, iwe imo katika utekelezwaji, lakini kama inatekelezwa maana yake ni kwamba tujitayarishe kuendelea kuomba kutoka nje na wetu sisi wakimbie wakashughulikie wengine.

Sasa mimi nasema tuendelee, lakini tujuwe kwamba nchi yetu ina matatizo na matatizo makubwa kumbe yako kwa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa sababu hawataki kushughulikia *scheme of service* ya Wizara ya Afya na Uchumi. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe Mwenyekiti, maelezo mazuri kazungumza Mhe. Said Ali Mbarouk. Lakini kauli ya mwisho sio nzuri. Nafikiri sio lengo letu kuikalia *scheme of service* ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Naomba anifahamu Mhe. Said Ali Mbarouk.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurudia tena. Tuli-*review* mara ya mwanzo tukatoa, tuka-*review* mara ya pili na sasa hivi kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii iko tayari tutai-*review* tena. Unajua haya mambo yanapita kwa wakati. *Specialist* tulikuwa tukimlipa nyuma, sivyo anavyolipwa leo. Daktari tulivyokuwa tukimlipa mwenye digrii ya kwanza katika miaka miwili iliyopita sivyo ilivyo leo. Kwa hivyo, hiyo imeshakuwa *review* tena na wataalamu wenyewe na ikija tutaishughulikia, hakuna tatizo lolote Mhe. Mwenyekiti, tunamuahidi na hao wataalamu kukimbia, sisi sio lengo letu na wala hatutaki, tunawaenzi kweli kweli. Lakini sasa tena, lisilobudi tena hatuwezi kumzuia.

Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba suala la watu kutolipwa mshahara wao ulioibiwa katika Hospitali ya Micheweni, na nikamwambia Mhe. Waziri kuwa nitakuwa mkali na ninamsubiri Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwa bahati nzuri Mhe. Afya na Ustawi wa Jamii kajibu vizuri sana kwamba wameshazungumza na Wizara ya Fedha na Uchumi walipwe. Lakini katika kipindi cha bajeti iliyopita nililizungumza suala hili, lakini mpaka

imefika tena katika bajeti ya leo na niliambiwa hivyo hivyo kwamba watalipwa. Sasa naomba kwa sababu yupo Waziri wa Fedha na Uchumi, basi anipe uhakika kama, kwa sababu tusijekusubiri tena bajeti nyengine inayokuja. Shilingi milioni 4,000,000/- mpaka leo hii hawajalipwa watu kwa nini. Kwa hivyo, naomba anipe uhakika watalipwa lini?

Mhe. Waziri wa Nhci (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri Mhe. Subeit Khamis. Mhe. Mwenyekiti, unajua uzito au kidudumizi tunachopata Wizara ya Fedha na Uchumi ni kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi *commitment* yake imeshafanya na ilikwishatoa fedha mpaka afisini zimefika. Sasa ikiwa Muhasibu kafanya uzembe, kasababisha yeye serikali ipoteze, basi tufuate utaratibu. Tufuate utaratibu kwanza tujuwe umefikia wapi utaratibu. Sio kwamba leo pesa zimeibiwa hapa na kesho zimeibiwa pale na serikali tutowe tu. Tutatoa ngapi Mhe. Subeit Khamis.

Kwa hivyo, utaratibu wetu ni kwamba uchunguzi kwanza ufanywe, kesi ifikishwe mahakamani ichunguzwe tuone kuwa yule yuko vipi. Lakini kama kweli, nakubaliana na wewe kuwa tusiwaadhibu hao wengine ambao hawana hatia. Sasa tutazungumza kwa hao wengine, basi nakiri Mhe. Mwenyekiti, tutajitahidi wakati huo uchunguzi unaendelea huko, basi tutaji-*commit*. Sasa hivi nakuomba uniamini mimi nitalishughulikia hili pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili tulimalize hili, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, unajua mimi sio mkaidi wa kuwa nina haja ya kuzuia hiki kifungu au nipige buti tu ili nionekane kuwa nimepiga buti, hapana sio malengo yangu. Lakini sasa huu ni mwaka wa tatu, uchunguzi huo haujakamilika, utakamilika lini na watu wanataka pesa zao ili watumie, wameshafanyakazi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aniambie huko Mahakamani hawajakamilisha huo uchunguzi na kama hawajakamilisha ni lini nataka aniambie ni lini au mwezi gani watapata pesa zao.

Mhe. Waziri wa Nhci (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mwenyewe siku zote unaelekeza kwamba suala likiwa mahakamani sisi tukiwa kama Waheshimiwa Wawakilishi hatuna mkono nalo, tuliwachie mahakama kwa utaratibu. Lakini mimi nakubali wazo lake kwamba hawa watu kuwasaidia wakati kesi inaendelea na imechukua muda mrefu kuwasaidia hawa watu, naomba aniamini. Mhe. Subeit Khamis leo umevaa kofia nzuri sana tuaminiane, kwamba tutajitahidi nitalibeba hilo, tutawatengenezea mambo yao yawe mazuri upesi upesi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waswahili husema ‘mfa maji hukamata chochote’. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alisema kwenye *quarter* ya kwanza jambo hili litashughulikiwa. Wakati huo nadhani alikuwa hajaingia Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi, Dk. Mwinyihaji. Sijui unasemaje kwa suala hili.

Mhe. Waziri wa Nhci (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, unajua *quarter* ya kwanza mara nyingi kifedha huwa ngumu. Tunajaribu sana kuwa wakweli na zile taratibu za fedha zinavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, unajua mara nyingi sasa hivi msimu ule ndio unaanza kuweka vizuri. Kwa hivyo, kuahidi kwa *quarter* kwanza. Lakini kwa mshahara nafikiri haina tatizo tutajitahidi, kwa sababu ile ni *first item.* Kwa hivyo, nakubaliana na yeye Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kama kauli yake alivyotoa, tutajitahidi hili kuliweka sawa ndani ya *quarter* ya kwanza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba

Mhe. Asha Moh’d Hilal: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilizungumzia kuhusu hawa madaktari wa usiku wanaopiga *round*, wanafanyakazi katika mazingira magumu na posho lao hawapewi kwa wakati muafaka. Kwa nini hawawekewi mpaka mwisho wa mwezi. Mhe. Mwenyekiti, ingekuwa wakipokea mshahara wao kungekuwa na kivocha chao kidogo wakapewa zile pesa wao, halafu wakasaidiwa na ule usafiri. Kwa kweli wanafanyakazi kwenye mazingira ya unyonge na ugumu wala hayastahiki. Mhe. Waziri alipokuwa anajibu hakunijibu suala hili. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii anihakikishie kuwa hawa watapatiwa usafiri na kile kiposho chao watapewa wakati muafaka.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu posho za *call*, ni kwamba madaktari wetu wanalipwa. Kuhusu usafiri, sijafahamu Mhe. Mjumbe anataka gari kila mmoja na yake au vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Usafiri wa kumfikisha kazini pale anapohitajika.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, huwa tunafanya hivyo na kama kutakuwa na tatizo basi tutalitatua jambo hilo.

Mhe. Asha Moh’d Hilal: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba 2,676,350,000

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, sina jambo kubwa ni dogo, lakini kiuandishi kwangu mimi hakuna dogo, mimi ni mwalimu. Mhe. Mwenyekiti, unajua katika hiki kitabu kuna kosa moja dogo sana tu ambalo linaleta mchanganyiko. Lakini Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa bahati mbaya hakunifahamu. Lakini kwa bahati nzuri mimi nina utamaduni kwa siku moja moja huenda kwenye nyumba ya kumbukumbu na nyaraka, huwa nasoma Hansard zile za *Legislative Council* kwa sababu najua hii ipo siku itakwenda katika nyumba ya kumbukumbu ya nyaraka. Ndio sababu nikataka tufanye marekebisho, japo kwa kupitia Hansard.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya, kuna sentensi moja inasema,

“Chuo hiki kinabaki kuwa ni taasisi pekee inayotambulika hapa Zanzibar kutoa mafunzo ya afya katika ngazi ya cheti na diploma”,

Inazungumzia cheti na diploma. Sasa katika aya ya pili inayofuatia chini inasema.

“Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya kwa sasa inatoa mafunzo ya Stashahada pekee”.

Inaonekana hapa inatoa Stashahada pekee na kile kifungu cha juu inatoa Stashahada na cheti. Sasa ndio nikasema kuna *contribute* ambayo ilikuwa ni ya kusawazisha. Kwa hivyo, nategemea kuwa waziri atajua namna ya kufanya. Hawezi kuandika kitabu tena upya, lakini namna ya kukifanyia masahihisho hata kupitia kwenye Hansard anajua utaratibu atakaofanya. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, hebu toa ufafanuzi kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Tutasawazisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Labda uhalisia wa mambo ukoje kwanza.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, tunatoa cheti na diploma. Kwa hivyo, tunatoa cheti na Stashahada, ndio Kiswahili nafikiri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nilipokuwa nikichangia Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni, nilihoji malalamiko ya wananchi wa Zanzibar, ambao wana shaka kuwa chuo kile kinaendeshwa kwa upendeleo kwa kuchukuwa wanafunzi wasio na sifa na kuachwa wale wenye sifa. Mhe. Waziri amenipa takwimu, ambazo zinaonesha kuna wanafunzi 440 kama ilivyo kwenye kitabu.

(a) Lakini hoja yangu ni kwamba nataka kujua ni sifa zipi za msingi ambazo wanafunzi anatakiwa kuwa nazo?

(b) Alisema kwamba yupo tayari kuipeleka Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Kwa kweli kuipeleka kamati hii na kutokana na hali ya fedha za Zanzibar ni gharama nyingi. Lakini wajumbe wachache kama mimi pamoja na Mhe. Omar Ali Shehe tunatosha kuchunguza tukipewa *terms of reference* kwa ajili ya kufanyiakazi hiyo. Nadhani atakubalina na mimi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kamati nakuachia wewe ikiwa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, au Baraza lote basi wewe ndio uwawezeshe. *(Makofi)*

Kuhusu sifa za kuingia chuo ni kwamba awe amemaliza *Form IV* au *VI* na kupasi masomo ya sayansi, hicho ndicho kigezo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anakiri mbele ya Baraza kwamba sifa ni kumaliza *Form IV* au *IV* pamoja na kupasi masomo ya sayansi. Wazanzibari wanahoji kuwa kuna watu ambao wamemaliza *Form II* na wako watu ambao waliomaliza *Form IV* pamoja na pasi tatu za C za sayansi na wameachwa.

Sasa hili linahitaji kuchunguzwa na wala tusiwe na wasi wasi wa gharama mimi kama nitateuliwa basi nitasamehe malipo yote, lakini tukachunguze, ili tupate ufafanuzi kwa Wazanzibari na Mhe. Waziri awe katika hali ya salama. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, hapa ninachosema kwamba awe amemaliza *Form IV* au *VI* na kupasi masomo ya sayansi. Sasa bado sijamfahamu Mhe. Mjumbe ametaja *Form II* namna gani, nadhani anifahamishe vizuri. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, unakusudia *Form II* ndio walioruhusika kuingia pale.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wazanzibari ambao wanasema wapo wanafunzi wa *Form II* katika Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni. Kwa hivyo, suala hili linahitaji kuchunguzwa na Baraza. Sasa kama hili ni kweli basi tuchunguze kwa kupitia Baraza ndio hoja yangu.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, ruhusa tumeshaitoa na wafanye uchunguzi. Lakini kuna darasa moja la *PHNB* pale wale ilikuwa ni darasa maalum la wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuwaendeleza *MCHN*. Sasa wale *MCHN* ambapo safari hii ndio wanamaliza ikiwa wamo wale *Form II* basi si kosa.

Lakini kama wapo wanafunzi wanaosomea Uuguzi, *Clinical Officer*, *Diploma* pamoja na mambo mengine kama yupo wa *Form II*, basi itakuwa ameghushi cheti na tutampandisha mahakamani. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hayo ni malalamiko ya wananchi, sasa njia pekee ni uchunguzi na hiyo ndio kazi yako. Kwa hivyo, naomba kama upo uwezekano basi iunde kamati ndogo hata mimi na Mhe. Omar Ali Shehe tunatosha kufanya uchunguzi, kwa ajili ya kupata ufumbuzi juu ya suala hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Mjumbe alipolichangia hili mimi nilichukua jukumu nikamuona Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Afya ndugu yetu Abdalla Ismail Kanduru, ambaye *Deputy Vice Chancellor of SUZA*. Kwa hivyo, nilichukua suala hili na nikampa kwa undani zaidi na nilimuomba hasa kwa kweli atufanyie kazi kidogo Waheshimiwa Wajumbe wamelalamika na wala sitaki chuo chako kianguke hadhi, kwa sababu taifa limekupa kazi hii uisimamie vizuri.

Kwa kweli ameniitikia vizuri na ameniahidi kwamba atalifanyiakazi. Kwa hivyo, nakuomba kwa heshima zote Mhe. Mjumbe na tumuachie kazi *Professor* Kanduru naamini ataifanyakazi na baadaye tutaleta ripoti kamili. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, namuamini *Professor* Kanduru na mwengine yeyote yule. Lakini hawa ambao tumewapa jukumu la kuendesha chuo. Sasa ikiwa kuna mtu ameghushi huyu alikuwepo na Baraza ndilo ambalo litakalosema kwamba ni *right or wrong* ndio ufumbuzi ulipo. Kwa hivyo, kuachiwa huyu mimi siridhiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani tuwaachie waifanye kazi hii na kama hawakuleta taarifa, kwa sababu unasema kuna taarifa na kama ungetuletea ushahidi ingekuwa jambo zuri zaidi na hilo lingekuwa na uhakika.

Lakini ni vyema tuachie kwanza na kama wewe unapata ushahidi wa hayo utatuletea na huku Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wafanye uchunguzi wa malalamiko hayo.

Kwa hivyo, ingekuwa ni vizuri kutupatia jina au majina ya watu hao, basi ingekuwa jambo jema sana kama vile alivyosema Mhe. Abubakar Khamis Bakary kuna mgonjwa alikwenda Hospitali ya Kiponda na kutoa na vitu hapo. Sasa kwa hili nadhani inakuwa vigumu kuweza kuituma kamati yangu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hoja ya mjumbe imelalamikiwa kwa muda mrefu na chombo ambacho kinasaidia sana kuridhisha wajumbe ni Baraza la Wawakilishi.

Kwa hiyo, naona kumtuma tena Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha bado hujawafanyia wajumbe haki, kwa sababu pale wanapokuwa na wasi wasi kwa mujibu wa Kanuni, kidogo kifungu nimekisahau, Baraza ndilo lenye wajibu wa kuondoa hiyo shaka.

Mhe. Mwenyekiti, ukimtuma Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha anaweza kumnong'oneza Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Afya kwamba hawa watoe, itakuwa bado hapajasawazishwa jambo. Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimefahamika. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, ninafikiri wakati unapokwenda kufanya uchunguzi lazima uwe na pahala pakuanzia. Sasa kwenye suala hili tunaanzia kutafuta jina la nani, ndilo jambo ambalo napata tabu kidogo hapa. Kwa hivyo, kama ingekuwa Mhe, Hija Hassan Hija anayo hayo majina au jina, basi ingekuwa ni jambo jepesi kuweza kulifuatilia hata kwenye orodha wenyewe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sikutaka kutaja jina la mtu yeyote, kwa sababu wewe ulikuwa hakimu na nikitaja hapa pengine watu wote wangefukuzwa chuoni. Kweli mimi nilisema ni shaka ya wananchi na ninavyojua kwamba kuna watu ambao wameachwa tena wanazo sifa na kuingizwa watu ambao hawana sifa, hii ni shaka wa wananchi na wala sio ya Hija au mke wa Hija, isipokuwa ni wananchi wa Zanzibar.

Sasa uchunguzi ungefanywa na kupata ufumbuzi ni kweli au uongo. Lakini kumpeleka mtu wa bodi, basi wote wataambiwa ni *degree* ya kwanza wamerudishwa tu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hivi hapa bado tuendelee kuficha haya mambo. Katika hali kama hii suala ambalo ni la wazi tuendelee kulificha kama unalielewa, ndipo kidogo ninapopata tabu hapa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib: Mhe. Mwenyekiti, busara inatakiwa itumike hapa na ninaomba kutoa tanbihi kwa Mhe. Hija Hassan Hija wapo watoto ambao wamemaliza *Form II* na wanabaki kuitwa *Form II*, lakini wanajiendeleza kwa siri na kupata *certificate* za *Form IV*. Sasa isijekuwa yeye amebakia *Form II* kumbe vile mwenzake ameshafika *Form IV* na baadaye sio akajaadhirika, lakini akaonekana ni muongo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hii natoa tanbihi ajue tu, kwamba wasije watu wakamwambia fulani *Form II*, kumbe vile amejiendeleza mpaka *Form IV*. Kwa mfano, watu waliojiendeleza inakuwa siri, anaweza kutoka Kizimkazi na kujiendeleza mjini, lakini kule Kizimkazi anaonekana bado ni *Form II*, kumbe vile amejiendeleza mpaka amefika *Form IV* na amekwenda pale ni *Form IV*. *(Makofi)*

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, labda niseme hivi muda wenyewe nao kidogo umekaa vibaya. Lakini Mhe. Hija Hassan Hija atakaponiletea majina basi nitaituma Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa ajili ya kufanya kazi kwa lengo la kufuatilia suala hili. *(Makofi)*

Nafikiri hayo makofi yanaweza kusaidia kwamba kuonesha tumekubali.

Mhe. Hija Hassan Hija na wewe ulipiga makofi. *(Kicheko)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako pamoja na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib, tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 04 - Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tumepata hoja ngapi, kwani hesabu yake inakuwa tabu kidogo.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, tumepata hoja mbili nafuatilia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuondoa shaka ni vyema tukamsikiliza. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kwenye hotuba hii kwenye Hospitali za Vijiji, kwa bahati nzuri Kamati ya Maendeleoo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ilichukua ahadi ndani ya jimbo langu katika kijiji cha Maziwani kuna Kituo cha Afya, ambacho mimi mwakilishi wao nimeshaanza kukipiga *foundation* na matofali ya kujengea tayari yamo.

Kwa hivyo, kamati ilichukua ahadi kwamba itamuona Mhe. Waziri kwa ajili ya kumalizia sehemu iliyobakia. Mhe. Waziri wakati alipofanya majumuisho sikulisikia hilo. Sasa nataka nifahamu na Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii), lakini Mhe. Waziri ananisikia.

Kwa hiyo, nataka nielewe je, ahadi ile iliyochukua kamati, kwa sababu ulichukulia Baraza na bahati nzuri wananchi leo hii walikuwa wanataka kuja hapa, lakini nauli nikaona itakuwa kubwa nikawazuia mimi. Kwa maana hiyo, nataka jibu la wale wananchi kuhusu hatua gani iliyofikiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kipindi cha miaka miwili na nusu. Katika kutembelea maeneo tofauti tulikuta Hospitali mmoja ya Mtambwe na Mhe. Mjumbe mwenzetu, ambayo kwa bahati nzuri ilikuwa iko kwenye hatua ya mwisho kabisa. Kwa kweli alikuwa na kila sababu za kuomba msaada kwa ajili ya kumaliza ujenzi ule.

Lakini kwa utaratibu tunaambiwa wananchi wajenge mradi kuanzia chini mpaka juu angalau baada ya hapo serikali ndio itie mwega kwa hatua iliyobakia na kuweza kumaliza. Mhe. Mwenyekiti, sisi baada ya kurudi tulimueleza Mhe. Waziri kwamba kuna kituo fulani kiko katika hali kadha, lakini hakijafikia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ushauri tulioutoa kama kamati basi tuliwaomba wananchi wale waongeze bidii na tulimpongeza sana Mhe. Omar Ali Jadi kwa kazi nzuri aliyoifanya na tuliwaambia wananchi wampe kura na wamempa.
Pamoja na hayo, kilichofuatia hapo ilikuwa ni changamoto kwake yeye pamoja na wananchi wake, si vibaya kuendeleza juhudi ile kwa ajili ya kupaweka sawa. Lakini ukweli hasa Mhe. Waziri kwa mtazamo huo hatokuwa na uwezo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Ali Jadi, utaratibu ambao hasa wanatumia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, yaani huwa wanajenga mpaka kufikia kiwango cha linta ikawa imebakia hatua ya kuezeka. Sasa anachosema Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii), kweli aliiona na hospitali ambayo iko kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad imefikia pahala pazuri.

Kwa hivyo, alichokieleza ni kwamba kama ingekuwa juhudi imezidi basi jambo hilo lingekuwa na nguvu kuiomba serikali itoe mchango wake.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, ndio nilipotoa maelezo kwa Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii) kwa sababu ndiye aliyechukua ahadi. Kwa kweli mimi kama mwakilishi wao baada ya kupata ripoti ya kamati walinitaka nichangie basi niliwaambia matofali 1000 na hivi sasa watu wameshafikia hatua kubwa sana, pia niliwaambia kama hayajatosha basi kachukuweni matofali sehemu fulani.

Sasa mimi nilichohoji hapa kwa sababu itakuwa tayari imefikia ile hatua inayotakiwa na serikali ya kuezeka na sio chini tena, yaani tunadai ile hatua ya kuezekwa kama taratibu zinavyoeleza. Kwa hiyo, nijue vipi watasaidiwa kuezeka na sio kujenga tena, kwani tayari tumeshafika juu.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, sisi wizara yetu ni tofauti. Kwa kweli Shirika la *DANIDA* wanatusaidia ikiwa Kituo chako cha Afya kiko katika hali mbaya, sasa wao ndio wanafanya matengenezo upya na wala hawataki mambo ya kumalizia, yaani wanataka kiwe kinainama au kinaanguka ndipo wanapotusaidia.

Kwa hivyo, kifungu cha kumsaidia Mhe. Mjumbe katika bajeti hii hatuna na hilo ndilo tatizo letu. Lakini kama anacho kituo ambacho kiko katika hali mbaya basi kesho tutawatuma watendaji wetu kwa ajili ya kukiangalia na kuweza kukifanyia matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, kituo chake Mhe. Mjumbe kilikuwa katika hali mbaya kimepigwa na upepo na hivi sasa kinajengwa upya kile cha Kojani pamoja na mambo mengine, huu ndio utaratibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, hatuna kifungu cha kuweza kumsaidia Mhe. Mjumbe, kwa sababu yule mwenye kutusaidia sisi *DANIDA* utaratibu wake kituo kiwe kinaanguka.

Mhe. Mwenyekiti: Wahehimiwa Wajumbe, kuna *CDF* inakuja na hayo ni maeneo ambayo unaweza kuingia pamoja na *TASAF*. Sasa nadhani Mhe. Mjumbe ungeangalia kwenye maeneo hayo, kwa sababu Mhe. Waziri ameeleza

kwamba wao hawana utaratibu kama ule wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mimi nimekueleza tu yale maeneo ambayo unaweza kupita. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri alisema vituo viwe katika hali ya kubomoka, kwa sababu tayari nimeshaanza kutiwa matofali basi naweza kwenda kubomoa, ili tupate huo msaada. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu serikali inasikia kilio cha watu wa Maziwani na kituo kiko juu, basi nataka suala hili liangaliwe upya ingawa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina fungu, lakini serikali iangalie pale ambapo wananchi wameshatoa juhudi zao kumalizia. *(Kicheko/Makofi)*

Nadhani Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha ananisikia nitakapopeleka barua yangu atanisikiliza. Tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	6,606,443,000/-
Kifungu 05	-	Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja	174,131,000/-
Kifungu 06	-	Idara ya Kinga	100,079,000/-
Kifungu 07	-	Idara ya Tiba	

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia wizara hii sana nilikwenda kwenye viambatisho. Kwa kweli nashukuru watendaji wa wizara baadhi ya viambatisho nilipata jibu pale pale kwa maandishi kama vile Mhe. Waziri Mkuu anapoulizwa maswali siku ya Alhamis, kwa hilo napongeza.

Lakini kuna kiambatisho 6.1 kwenye ukurasa wa 120 ambacho kinaeleza mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki katika Hospitali za Idara ya Tiba kwa mwaka Julai, 2009 mpaka Machi, 2010.

Sasa maelezo yaliopo juu na taarifa zilizomo ndani ya jaduweli ni tofauti, kwa sababu hapa waliopo ni wagonjwa wa nje tu ndio waliolazwa, lakini waliofariki hawapo. Kwa hivyo, nataka kujua, sijui takwimu zake zitakaa vipi na wala sikupata jibu.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sahihi hawa ni wagonjwa waliolazwa tu na waliofariki kwenye kiambatisho hiki hawapo. Kwa hiyo, nampongeza Mhe. Mwakilishi kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hivi takwimu ya waliofariki unayo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwenye maelezo yamo, lakini kwenye jaduweli hili hamna.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kama kwenye maelezo yamo basi nitaangalia, lakini isijeikatokea vyenginvyo. Tuendelee.

Kifungu 07	-	Idara ya Tiba Unguja	372,200,000/-
Kifungu 08	-	Idara ya Tiba Pemba	

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hivi ni viatu vya kawaida.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ni viatu vya kawaida, kwa sababu baadhi ya mambo yale yote nimeyasamehe. Kwa mfano, yule jamaa yangu aliyefariki, mjukuu wangu ndio mitihani. Lakini ninachopigania sasa kwenye kifungu cha 30003 na 30005 katika Idara ya Tiba Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu chakula cha wagonjwa nilisema ukifanya *calculation* mgonjwa wa Pemba anapewa shilingi 266/- wakati mgonjwa wa Unguja anapewa shilingi 11,267 kwa nini? Suala jengine ambalo nimeuliza ni kuhusu ununuzi wa mapazia na mambo mengine kama hayo.

Mhe. Waziri alisema kuna Daktari Bingwa anakuja ambaye alikwenda kusoma Kenya, ambapo Mhe. Waziri amesema atakwenda Pemba. Hivyo, daktari huyu kweli atakwenda kukaa katika nyumba ambayo kwa Kipemba tunaita koa uchi, yaani ni yule konokono ambaye hana nyumba.

Sasa daktari unampeleka Pemba hata pazia hamna, utie pazia la gunia, haiwezekani, kwa nini Pemba hazikutiwa hata shilingi moja ya mapazia na mambo kama hayo.

Suala jengine ni kuhusu kuendeshaji wa hospitali, kwa upande wa Pemba ni shilingi 700,000/- kwa kila hospitali. Lakini kwa upande wa Unguja hospitali mbili hizo na kila hospitali ni shilingi milioni 5. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana niliposema *are we serious* katika huduma ya Wapemba. Hilo ndilo ambalo ninalotaja jibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa kuhusu daktari ni kwamba anayo nyumba yake Wete, isipokuwa amekwenda masomoni nyumba yake ipo pamoja na familia yake ipo. Kwa hivyo, atakaporudi anarudi kwenye nyumba yake, kwa sababu daktari huyo ameondokea hapo Wete.

Sasa kuhusu mgawanyo wa fedha za chakula. Kwa upande wa Pemba kwa hesabu ya haraka haraka ni shilingi milioni 39 na Unguja ni shilingi milioni 36. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama hili tumefanya kosa kwa sababu Pemba kuna hospitali tano na huku ziko mbili, basi tutasawazisha kwenye bajeti ijayo na wenyewe viongozi wa Pemba wapo na tayari wameshalisikia.

Vile vile kuhusu mgawanyo wa fedha za mapazia pamoja na mambo mengine, hayo ni mapendekezo ya wenyewe Viongozi wa Afya Pemba, pengine wako wanaona sio jambo muhimu na lile lilikuwa muhimu na wenyewe wananisikia nilivyofahamishwa jana, yaani lile jambo ambalo ni muhimu ndilo wanalolipa kipaumbele. Lakini tutalibeba na bajeti ijayo tutaliangalia na kuweza kusawazisha.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani na Mhe. Waziri hata kidogo inamaana safari hii Wapemba wafe, kwa sababu unaposema kwamba *operation* ni shilingi 700,000/- mpaka mwakani ndio tuongeze kwenye bajeti, haiwezekani na wala mtu wa kawaida hawezi kuona hali hiyo.

Kwa kweli nakubali wagonjwa ni shilingi milioni 39 kwa Pemba. Lakini kuna hospitali tano na nimefanya hesabu hapa kila hospitali ni shilingi milioni 700,000/-. Sasa wagonjwa waliolazwa kwa hospitali za Pemba ni 14,000/- kulinganisha na wagonjwa 3,000/- kwa hospitali mbili za Unguja. Kwa upande wa Unguja ni shilingi milioni 36 kwa hospitali mbili, kwa hiyo hospitali moja ni shilingi milioni 18 kwa watu 1,597 kwa sababu ni hospitali mbili ni shilingi 11,000/-.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri anasema kwamba mwakani ndio atasawazisha, inamaana safari hii wale wagonjwa watakaolazwa Pemba wafe kwa shilingi 200, haiwezekani. Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri ataniambia kwamba fedha hizi zitagaiwa, basi atuletee taarifa kuwa fedha hizi zilizokuwa *allocated* kwa wagonjwa wote waliolazwa zitagaiwa sawa sawa, yaani kila mgonjwa anayo haki sawa na mwengine.

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri aseme hapa kuwa fedha hizi zitagaiwa sawa kwa wagonjwa hao au kwa utaratibu huo, ili tuweze kukubaliana. Lakini hawezi kabisa kuniambia wagonjwa wasubiri mpaka mwakani ndio wapewe fedha za chakula na hivi sasa wasile chakula.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimfahamishe Mhe. Mjumbe, kwa kweli sisi hatuna nia ya kuua Wapemba na wala hawatokufa, kwa sababu kiutaratibu tunaofanya sisi na tunavyoiendesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wakati yanapotokezea matatizo Pemba fedha zinatoka Unguja na wala si mara moja. Kwa mfano, kipindupindu au matatizo mengine yoyote, anaposema tu Afisa Mdhamini tu

ninaupungufu wa kitu fulani, basi siku ya pili zinakwenda na huo ndio utaratibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba tutazihudumia hospitali za Pemba kwa kadri ya uwezo wetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kwa hivyo, sisi ni wajumbe wa kamati zako za kudumu na tunafanyakazi kwa maslahi ya Wazanzibari.

Lakini kwa kuwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni mjumbe wa kamati hii, basi ningeomba ile kauli kali aliyosema Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina nia ya kuua Wapemba aifute Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kuweka *Hansard* vizuri. Mhe. Mwenyekiti, ni hilo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, kwanza siifuti kwa sababu kwa hesabu hizi ni dhahiri kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inataka kuua wagonjwa wa Pemba. Kwa kweli haiwezakani shilingi 266 kwa mujibu wa bajeti. Sasa kama ni kusawazisha basi tusawazishe na Mhe. Waziri akubali na aseme kwamba fedha zilizopatikana kwa hospitali zote saba, yaani tano za Pemba na mbili za Unguja fehda hizi sasa zitagaiwa sawa.

Vile vile aseme kwa *operations* kwa sababu wagonjwa wanaolazwa katika hospitali tano za Pemba ni wengi yaani 14,000 ukilinganisha na 3,000. Sasa hawa 3,000 wamepewa fedha za *operations* shilingi milioni 5 kwa kila moja. Kwa mfano, Hospitali moja ya Makunduchi imepewa shilingi milioni 5, lakini *operations* kwa hospitali moja ya Pemba imepewa shilingi 700,000/-. Kwa hivyo, hii ni dhahiri kwamba wanataka kuwaua na wala sifuti kauli hiyo mpaka Mhe. Waziri aseme kuwa fedha hizi zitagaiwa kwa hospitali zote saba sawa kwa mujibu wagonjwa walivyo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo nitazigawa sawa, kwa sababu hatuna nia ya kuua mtu Pemba na wala sina tatizo. *(Kicheko/Makofi)*
Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu fedha zitagaiwa sawa na tutaletewa hapa basi nakubali kwa kauli thabiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tuendelee, lakini tuletewe taarifa ya mgawanyo huo.

Kifungu 08	-	Idara ya Tiba Pemba	89,751,000/-
Kifungu 09	-	Idara ya Kinga Pemba	52,220,000/-
Kifungu 10	-	Idara ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya Unguja	64,928,000/-

Kifungu 11	-	Idara ya Ustawi wa Jamii Pemba	76,000,000/-
Kifungu 12	-	Idara ya Madawa ya Kulevya Pemba	12,746,000/-
Kifungu cha 13	-	Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja	92,966,000
Kifungu cha 14	-	Mchemia Mkuu Unguja	36,926,000
Kifungu cha 15	-	Mnazi Mmoja Hospital	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili nilihoji ubora wa maabara ya Mnazi Mmoja kama Hospitali ya Rufaa na nikatoa ushahidi kwamba kuna wagonjwa ambao walipimwa wingi wa damu nakuonekana wana damu nyingi lakini kumbe walikuwa wana damu ndogo sana.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alikubali kwamba. wataongeza *reagent*, lakini nilitaka nijue kwamba kwa umuhimu wa *reargent* kwa maabara ile

(a) Ni muda gani wataongeza?

(b) Nilitaka nijue kipimo hiki alifanya daktari na daktari ni mwanadamu na keshokutwa tunaingia katika soko huria la Afrika Mashariki leo akimpima mtu wa Matemwe na Tumbatu tutasameheyana lakini kesho kutwa akimpima mtu wa Kenya na Uganda hii itakuwa si kesi ndogo. Sasa ili kuokoa madaktari nini hatua ya haraka ya Wizara ili tusije tukawatia matatizo madaktari wetu kwa sababu ya udhaifu wa maabara zetu?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *Reagent* Hospitali ya Mnazi Mmoja tunaipatia na tutawapatia kama unavyotaka, kama wanavyohitaji kwa sababu moja ya wajibu wetu wa kazi ni kazi nzuri ya maabara ili daktari watibu vizuri.

Na kuhusu *Quality Control* tuifanya tutaihakikishia kwamba *result* zitakuwa nzuri kwa wafanyakazi wetu.

Mhe. Haji Hassan Hija: Mhe. Mwenyeki, unajua kwa maneno matamu Mhe. Waziri anaongoza sana na nampongeza. Lakini nasema kwamba historia hii nah ii hadithi kwamba tutaongeza, tutafanya, halikuanza leo Jumapili ni jambo la miaka tangu mimi naingia humu bajeti ya mwaka 2006/2007 limekuwa ni hadithi.

Ukiangalia kweli matumizi ya maabara ile ni bilioni 5, Wizara inaangalia vipa umbele vyengine lakini inaacha suala hili muhimu. Tuendelee lakini

namuomba kwamba ajue kwamba uchaguzi umemalizika na keshokutwa tunaingia Baraza jipya hili tatizo liondoke haraka kwa maslahi ya nchi hii.

Kifungu cha 15 Mnazi Mmoja Hospital	189,895,000
Kifungu cha 16 Mkemia Mkuu Pemba	15,041,000
Kifungu cha 17 Idara ya Afya ya Jamii Pemba	22,146,000
Kifungu cha 18 Huduma za Afya Wilayani Unguja	40,000,000
Kifungu cha 19 Huduma za Afya Wilayani Pemba	16,178,000
Jumla ya Fungu	**10,638,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	985,806,000
Jumla ya Fungu		**9,085,806,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. WAziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu pamoja na mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kuwa Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Naafiki.

Mhe.Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na makisio hayo pamoja na marekebisho wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilieamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilifikiri kwamba kazi hii ingekuwa nyepesi kidogo lakini kumbe imekuwa ni nzito kiasi cha kwamba muda uliobaki nafikiri hamtoshi Mhe. Waziri akawasilisha hotuba yake kwa uzuri na angalau na Mwenyekiti na Waziri Kivuli wakapata kutoa hotuba zao. Kwa maana hiyo itabidi tuendelee jioni kama tulivyokuwa tumekualiana kabla.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe nahirisha Kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:38 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011
Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji

Mhe. Spika, naomba kwanza kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea na uwasilishaji wa bajeti ya wizara naomba uniruhusu nichukue nafasi hii niwafariji na kuwapa mkono wa tandhia Mhe. Muhiddin Moh'd Muhiddin wa Jimbo la Mtambile ambaye pia ni Waziri Kivuli wa wizara hii kwa kumpoteza mtoto wake mpenzi. Pia nimfariji Mhe. Dadi Faki Dadi Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kumpoteza mama yake mzazi. Kwa hivyo, wote tunasema *ina lilahi wa ina ilayhim rajiun.*

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutuwezesha leo hii kukutana hapa tukiwa na afya njema. Aidha, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake mwema, wenye hekima na busara uliopelekea kuimarika kwa uchumi wetu, kudumisha amani, utulivu na upendo miongoni mwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Aidha, wizara inampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa maridhiano waliyofikia hivi karibuni yaliyoingiza utulivu na amani hapa nchini kwetu. Vile vile tunawashukuru Mhe. Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi kwa miongozo na ushauri wao katika kufanikisha kazi za Wizara hii.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa hotuba yake pamoja na maelezo ya hali na mwelekeo wa uchumi kwa ujumla, mipango na Maendeleo na Malengo ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Tegemeo letu ni kwamba mipango hiyo itakuwa ndiyo dira itakayosaidia kuongeza uzalishaji, na tija katika sekta za uchumi na zenye kutoa huduma, na hatimae kupunguza umasikini miongoni mwa wananchi.

Mhe. Spika, hotuba hii pia imezingatia utekelezaji wa miongozo ya dira 2020, Mpango Mkuu wa Ukuzaji Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar pamoja

na Mpango Mkakati wa wizara, ambayo imelenga kutekeleza malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya miaka mitano 2005 – 2010 ambao umeelezwa katika utekelezaji halisi wa kila sekta.

Mhe. Spika, mtikisiko wa kiuchumi uliokuwa umeikumba dunia mwaka 2008 unaonyesha dalili ya kupungua na hivyo kutoa matumaini ya kuongezeka kwa biashara, uwekezaji na idadi ya watalii watakaotembelea Zanzibar kwa mwaka 2010/2011. Pamoja na mtikisiko wa uchumi kuonyesha kupungua hali ya biashara hasa ile ya usafirishaji kama kawaida inaonesha kupanda na kushuka wakati hali ya uagiziaji (nje ya Tanzania na kutoka Tanzania Bara) kuonesha ongezeko. Kwa mwaka 2009/2010 hali ya biashara ilikuwa kama hivi:-

- Bidhaa zenye thamani ya Tzs 29,744.5 bilioni ziliweza kusafirishwa na kuuzwa nje kwa mwaka 2009, ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Tzs 30,189.2 bilioni kwa mwaka 2008. Usafirishaji huu umepungua kwa asilimia 1.5, iliyosababishwa na upungufu wa usafirishaji katika mazao ya asili ya karafuu na mwani.

- Usafirishaji wa bidhaa kwa upande wa Tanzania Bara ulikuwa Tzs 1,341.1 bilioni mwaka (2009) wakati mwaka 2008 ni T.sh 1,459.6 bilioni.Uagiziaji kutoka Tanzania Bara nao umepungua kutoka thamani ya T.sh 25,936.5 bilioni kwa mwaka (2008) na kufikia Tzs 19,651.0 bilioni mwaka 2009 sawa na upungufu wa asilimia 24.3.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Utalii, katika mwaka 2008, sekta ya utalii ilipatwa na mtikisiko mkubwa baada ya kuanguka kwa soko la sarafu ulimwenguni hali ilipelekea kupungua kwa wageni waliotembelea Zanzibar, kufikia 128,445 ikilinganishwa na wageni 143,265 walioitembelea Zanzibar mwaka 2007. Sura ilirudi kutoa matumaini mwaka 2009 ambapo tulipokea kiasi cha watalii 134,954 sawa na ongezeko la asilimia 5. Kukatika kwa umeme kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo kuanzia Disemba 2009 hadi mwezi Machi 2010, kulipelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa miradi ya utalii na baadhi ya wawekezaji kulazimika kupunguza huduma zao.
Mhe. Spika, wizara kupitia Mamlaka ya Uwekezaji inaendelea na juhudi za kutafuta njia ya kuweza kukamilisha mpango mkuu (*The Master Plan*) wa uwekezaji katika maeneo huru ya uchumi (Amani eneo la Viwanda na Fumba kwa Unguja na Micheweni Pemba) ili kuweza kuweka wazi faida inayoweza kupatikana kutokana na uwekezaji utakaofanyika.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo Serikali imeendelea kuweka mazingira yenye kuvutia uwekezaji na biashara nchini ambayo yamepelekea kuwepo kwa

mtaji binafsi kutoka nje kiasi cha Dola za Kimarekani 2,810.35 milioni, ambapo sekta ya utalii inaongoza kwa asilimia 65.86. Mitaji hiyo imechangia kuongezeka kwa shughuli za biashara, kusogeza huduma za kijamii kwa wananchi, na upatikanaji wa ajira kwa wazalendo wasiopungua 50,000.

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda inayojumuisha uzalishaji viwandani, ujenzi, pamoja na uchimbaji wa mawe, inaonyesha kushuka kwa mchango wake kutoka asilimia 14.3% mwaka 2008 na kufikia asilimia 13.1% mwaka 2009. Kukatika kwa umeme kumepunguza kiwango cha mchango wa viwanda.

Mhe. Spika, mwaka wa fedha 2009/2010 wizara ilitengewa jumla ya Tzs 4,298.5 biilioni kati ya hizo bilioni 2.3 ni kwa kazi za kawaida na bilioni 1.9 ni kwa kazi za maendeleo. Kwa upande wa mapato, lengo lilikuwa kukusanya jumla ya Tzs 839.4 jumla ya Tsh 625.75 milioni zimeweza kukusanywa hadi Machi 2009 ikiwa ni asilimia 74.5 ya lengo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI 2009/2010:

Mhe. Spika, kabla sijaingia katika mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2009-2010 ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe walishapitia vitabu vya hotuba ya bajeti ya wizara yangu na hasa kwa kuwa vitabu hivi viligaiwa mapema. Kwa maana hiyo nitafanya mapitio ya haraka haraka katika utekelezaji na malengo ya mwaka ujao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya mafupi ya utangulizi naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa malengo ya mwaka 2009-2010 kiidara na taasisi zilizo chini ya wizara na kuwasilisha mpango wa kazi na makisio ya mapato na matumizi kisekta kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

IDARA YA MIPANGO NA SERA:

Mhe. Spika, mapitio ya utekelezaji wa malengo ya mwaka 2009/2010 yanaonekana ukurasa 6 hadi 12 na ili kuweza kutekeleza malengo hayo Idara ya Mipango na Sera inaombewa Tsh 1.5 bilioni kwa kazi za kawaida na 1.4 bilioni kwa kazi za maendeleo.

- Kuendelea na kazi za ukarabati wa majengo ya Wizara Unguja na Pemba (Afisi Kuu, Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Idara ya Biashara).

- Usimamizi wa ujenzi wa jengo jipya la Wizara Pemba.

- Kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5), watatu (3)

Unguja na wawili (2) Pemba. Wafanyakazi sita (6), watatu (3) Unguja na watatu (3) Pemba mafunzo ya muda mfupi.

- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi minne (4) ifuatayo:-

  a) Kufanya mapitio ya Sheria na ripoti zinazohusiana na biashara kama ifuatavyo:-

     i) Mapitio ya Sheria Nambari 2 ya mwaka 1995 ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji;
     ii) Mapitio ya Sheria nambari 4 ya mwaka 1983 ya Mizania na Vipimo;
     iii) Mapitio ya Ripoti ya TCFB ya mwaka 2001 (*Tanzania Central Freight Bureau/SUMATRA*) juu ya Kupungua kwa Biashara Zanzibar.

  b) Kuratibu uimarishaji wa viwanda na biashara ndogondogo na za kati *(Integrated Programme).*
  c) Kuratibu uimarishaji wa mazingiara ya biashara.
  d) Kuratibu uimarishaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii.\

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba kazi ya mapitio ya sheria za biashara ilifanyika na utayarishaji wa rasimu za awali za sheria hizo unatazamiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi Julai, 2010. Hatahivyo, kazi ya upitiaji wa ripoti ya *TCFB* iliondolewa na badala yake wizara ilifanya upitiaji wa sheria ya biashara nambari 4 ya mwaka 1989 ambayo nayo rasimu ya awali itakuwa tayari mwishoni mwa mwezi Agosti, 2010.

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji ulioainishwa katika kiambatisho nambari 1, wizara kupitia Idara ya Mipango imewapatia mafunzo ya ndani na nje jumla ya wafanyakazi kumi na tisa (19) kutoka Unguja na Pemba sawa na asilimia 172.73 ya lengo. Kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Mhe. Spika, mbali na malengo tuliyojiwekea, Wizara imeandaa na kukamilisha Mkakati wa Taifa wa Usafirishaji (*Zanzibar National Export Strategy*) pamoja na Mpango Kazi *(Action Plan)* wa utekelezaji wa mkakati huo, ambao kwa pamoja inaelezea utaratibu na hatua za kuchukuliwa ili kuongeza uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Lengo la mkakati huo ni kukabiliana na

nakisi katika biashara hapa Zanzibar. Kati ya hatua zilizoanishwa katika mkakati huo ni:-

- Kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo na viwanda.
- Uongezaji wa thamani wa bidhaa (*Value Addition*).
- Kuanzisha na kuimarisha miundombinu ya kukuza biashara ikiwemo kuunda taasisi ya kuweka viwango, pamoja na kukuza ufanisi wa huduma katika bandari na Viwanja vya ndege.
- Kukuza uwekezaji katika sekta ya viwanda, huduma na kilimo.
- Kuangalia uwezekano wa kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Uchumi (SEZ).
- Kukuza biashara ya Utalii kupitia soko la ndani, kikanda pamoja na soko la nchi zinazoibuka kimasoko *(emerging markets).*

MALENGO YA MWAKA 2010/2011:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 pamoja na mambao memngine yatakayijitokeza, Idara imejipangia

. Kufanya mapitio ya Sera ya Viwanda na Sera ya Biashara (*Review of Industrial Development Policy and Trade Policy*)

- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi minne (4) ifuatayo:-

a) Kukamilisha mapitio ya Sheria za Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji; Sheria ya Mizania na Vipimo; na Sheria ya Biashara.

b) Kuratibu uimarishaji wa viwanda na biashara ndogondogo na za kati (*Integrated Programme*).

c) Kuratibu uimarishaji wa mazingira ya biashara.

d) Kuratibu uimarishaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

- Kuendelea na kazi za ukarabati wa majengo ya Wizara Unguja na Pemba (Afisi kuu, Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Idara ya Biashara).

- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) na wafanyakazi saba (7) mafunzo ya muda mfupi. Pamoja na kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa njia ya semina. Jumla ya semina 4 katika Nyanja za Jinsia, UKIMWI na Utawala zitafanywa.

Ili kuweza kutekeleza Malengo hayo Idara ya Mipango na Sera inaombewa Tzs 1,531.16 milioni kwa kazi za kawaida na Tzs 1,413.55 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, wakati nilipowasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ya mwaka 2009/2010 niliahidi kuufanyia mabadiliko muundo wa Wizara hasa kuangalia upya majukumu ya taasisi zilizoko chini ya Wizara. Kazi hiyo imekamilika katika ngazi ya wizara na sasa muundo huo utawasilishwa katika ngazi husika kwa kutolewa maamuzi. Mapendekezo ya Muundo huo mpya unaonekana katika **kiambatisho nambari 7**.

BARAZA LA BIASHARA LA ZANZIBAR:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Baraza la Biashara la Zanzibar lilijipangia:-

- Kuandaa vikao vitatu (3) vya Baraza, na vikao15 vya Kamati Tendaji, katika mikutano hiyo kero 40 zilizojadiliwa katika Sekta za Kilimo, Miundombinu, Utalii, Mji Mkongwe, kodi pamoja na ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zilitolewa maelekezo na miongozo.

- Kuandaa mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Biashara, Kamati Tendaji, vikundi kazi, Sekretarieti ya Baraza, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Watendaji Wakuu wa Serikali na Sekta Binafsi.

- Ununuzi wa vifaa na vitendea kazi kama kompyuta, photocopy, na vifaa vyengine vya kutendea kazi.

Mhe. Spika, **n**apenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Baraza la Biashara la Zanzibar limefanikiwa kuandaa mikutano mitatu (3) ya Baraza na vikao kumi na tano (15) vya Kamati Tendaji. Katika mikutano hiyo mambo arobaini (40) yaliyokwaza utendaji katika Sekta za Kilimo, Miundombinu, Utalii, Mji Mkongwe, kodi pamoja na ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yalitolewa maelekezo na miongozo. *Kiambatisho Nambari 9.*

i. Lilisimamia utendaji wa vikundi kazi vya sekta za Miundombinu, Uchumi na Fedha, Utalii na Kilimo ambapo kila kikundi kilifanyiakazi maazimio yaliyofikiwa katika vikao vya Baraza na kutafuta ufumbuzi wa kero zilizojitokeza.

ii. Kuandaa kikao cha mafunzo na mashauriano kwa sekta binafsi kujadili kero zinazowakabili zikiwemo ushiriki wao kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

iii. Kununua Kompyuta (*laptop*) moja na fotokopi yenye uwezo mkubwa (*heavy duty*).

iv. Kuandaa makala nne (makala moja kila robo mwaka) na kuchapishwa kwenye majarida kama vile "*Zanzibar Economic Bulletin*".

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Biashara limejipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

a. Kuandaa vikao viwili (2) vya Baraza, vikao vinane (8) vya Kamati Tendaji na kuendelea kusimamia shughuli za vikundi kazi.

b. Kuzindua Mabaraza ya Biashara ya Mikoa (*Regional Business Councils*).

c. Kuendelea kuendesha vikao viwili vya wawekezaji wa ndani na wa nje kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Taifa Tanzania.

d. Kuandaa mafunzo kwa watendaji wa kitengo cha Baraza na Wajumbe wa Baraza.

e. Kuendelea kuandaa makala za kuelimisha Umma juu ya utendaji kazi wa Baraza, mafanikio na changamoto.

f. Kutengeneza tovuti ya Baraza la Biashara.

AFISI KUU PEMBA:

Mhe. Spika,Utekelezaji kwa upande wa Afisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2009/2010 unaendana na mtiririko wa maelezo ya kila idara ambayo yamehusisha na shughuli za Afisi Kuu Pemba. Afisi hii ni kiunganishi katika

kuhakikisha kwamba majukumu, malengo na shabaha zote za wizara kwa upande wa Pemba zinatekelezwa kama zilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Afisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, tunaomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tshs. 163,407,000 kwa kazi za kawaida.

SEKTA YA UTALII:

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Shirika la Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga, kusimamia, kuendeleza utalii, na kuitangaza Zanzibar ili sekta hii iende sambamba na sera na mikakati ya serikali katika kufikia malengo makuu ya kuimarisha uchumi wa taifa na kupunguza umasikini.

MALENGO YA SEKTA YA UTALII KWA MWAKA 2009/2010:

- Kuendelea kuitangaza Zanzíbar na kukuza utalii kwa kushiriki maonesho ya utalii na kualika vikundi vya waandishi wa habari na watembezaji watalii kutoka katika masoko ya asili (*Traditional Markets*) na mapya (*Emerging Markets*), ili kuwataka waandike makala na kupiga picha zenye kuonyesha vivutio vya utalii pamoja na kuwashashiwi watalii watembelee Zanzibar na kuiingiza Zanzibar katika program ya masoko yao.

- Kutafsiri vipeperushi, tovuti na majarida ya útalii katika lugha za masoko ya asili na yenye matumaini ili taarifa ziwafikie walengwa kwa madhumuni ya kutembelea nchini kwetu kwa wingi zaidi.

- Kuendelea kuchapisha vielelezo vya utalii ikiwa ni pamoja na kalenda (*scroll wall calenders*), jarida la Karibu Zanzíbar, vipeperushi cha Kijerumani na mwongozo wa malazi kwa wageni (*accomodation guide*).

- Kuimarisha mitandao *(websites)* za Kamisheni ya Utalii na ile ya Sekta Binafsi ya Jumuia ya Watembezaji Watalii, Zanzibar (ZATO) kwa kuweka matangazo ya utalii kwa lugha tofauti ili taarifa zilizomo zisomwe na watu wengi zaidi duniani.

- Kuandaa tunuku ya Dkt David Livingstone (*Dr. David Livingstone Best Pratice Award*).

- Kuendelea na uandaaji wa mpango kazi wa uendeshaji wa utalii wa baharini (*Marine Tourism Management Plan*) kwa kushirikiana na mradi wa MACEMP.

- Kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii na mali zao.

- Kushajihisha wafanyabiashara wa miradi midogo midogo ya utalii kufanya biashara kwa kujitegemea bila ya kupitia mtu wa kati.

- Kuimarisha kitengo cha utafutaji masoko kilicho ndani ya Kamisheni ya Utalii kwa kukipatia wataalamu zaidi na vitendea kazi.

- Kuandaa mpango wa pamoja na wenye mahoteli ili waweze kuchangia gharama za utafutaji masoko.

- Kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwa kujenga ili kuongeza idadi ya madarasa, afisi pamoja na maktaba na maabara. Kuanzisha kitengo cha kufundisha teknolojia ya habari (*IT*) na biashara, kusomesha na kuajiri walimu wapya pamoja na kujiunga kwa *NTA* level 7 na 8.

- Kuongeza idadi ya wanafunzi, viwango vya elimu pamoja na kuanza maandalizi ya Chuo kutoa shahada ya kwanza *(undergraduate).*

- Kuanzisha kitengo cha utafiti.

- Kuweka vitengo shirikishi Unguja na Pemba.
- Kuwapatia walimu mafunzo nje ya nchi.

- Kuanza utekelezaji wa mpango wa Biashara wa miaka mitano.

- Kuendelea kutafuta wabia kwa ajili ya kushirikiana nao katika uwekezaji wa eneo la Vitongoji.

- Kuwasomesha watendaji watano wa Shirika, wawili kiwango cha digirii ya kwanza, mmoja katika fani ya uchumi, mmoja katika fani ya masoko katika shughuli za biashara ya utalii, na mmoja kiwango cha diploma katika fani ya uandishi wa habari.

- Hoteli ya Bwawani itaendelea kuvifanyia matengenezo vyumba kumi katika ghorofa ya nne, pamoja na ukumbi wa mkutano wa roof top.

- Kuwapatia ujuzi vijana kutoka kituo cha elimu Mbadala kwa kuwapa mafunzo ya vitendo ***(Practical)*** ili kuwatayarisha kwa ajira.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji ulioaniishwa katika *kiambatisho nambari 2, w*izara kupitia sekta ya utalii imekamilisha utungaji wa Sheria mpya ya Kamisheni ya Utalii Nambari 6 ya mwaka 2009, pamoja na uundwaji wa Baraza la Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Mhe. Spika,Kazi ya kuitangaza Zanzíbar na kukuza utalii imefanyika vyema. Jumla ya vikundi saba vya waandishi wa habari kutoka Urusi, Italy, China, Aljazira, Marekani, Israel na Afrika Kusini vimealikwa kwa lengo la kuandika makala yanayohusu Utalii wa Zanzibar. Aidha, tuliendelea kufanya "*Road Show*" katika masoko yanayoendelea na yanayoibuka katika nchi za Scandinanvia, China, Malaysia, Urusi pamoja na kushiriki maonesho ya kiutalii duniani kama *BIT – Italia, ITB – Ujerumani, ATM - Dubai, INDABA - Afrika Kusini, Russian Trade and Tourism Trade Show, WTM – London na China - International Trade Mart.*

Mhe. Spika, Kamisheni imepeleka wafanyakazi wanne (4) masomoni katika ngazi ya cheti, diploma na shahada ya kwanza kwa ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi. Aidha, wafanyakazi sita (6) walisomeshwa kwa ufadhili wa mradi wa MACEMP, na wafanyakazi watatu (3) walipata mafunzo ya muda mfupi nchini India, kama inavyoonekana hapo chini.

1.1 Vile vile, kuliendeshwa Mafunzo ya biashara ya utalii na ujasiriamali kwa wajasiriamali 30 wa vijiji vya Ukanda wa Pwani vya Unguja na Pemba. Vijiji vilivyopatiwa mafunzo hayo ni Nungwi, Uzi, Marumbi, Uroa, Kizimkazi Mkunguni, Matemwe, Pwanimchangani, Bungi, Kiembesamaki, Bumbwini, Ndijani, Kisakasaka, Kidoti, Bububu, Tumbatu, Kipangani Wete, Limbani, Wete, Tumbe, Gando, Maziwang'ombe, Chokocho, Wambaa, Mkoani, Vitongoji, Chakechake, Kilindi na Matale

- Mafunzo ya *"Outreach Program"* yalitolewa na Chuo cha Maendeleo ya Utalii - Maruhubi kwa wanavijiji 69 miongoni mwao (60 wanaume na 9 wanawake) kutoka katika vijiji vya

Matemwe, Pwani Mchangani na Kijini katika fani za Huduma za Vyakula na Vinywaji, Upishi, Mapokezi ya Wageni, Mawasiliano na Huduma kwa Wateja na Utunzaji Nyumba.

- Mafunzo ya ujasiriamali yanayohusiana na masuala ya utalii yalifanywa na Kamisheni ya Utalii kwa vikundi vinne (4) vya Ushirika vya Wanawake vya Pemba ambavyo kila kikundi kilitoa wajumbe kumi (10) kwa jumla ni arubaini (40). Vikundi vilivyopata mafunzo ni:-

  - Kikundi cha Msitusahau – Wambaa.
  - Kikundi cha Umoja ni Nguvu – Wambaa.
  - Kikundi cha Nia Njema – Tondooni.
  - Kikundi cha Tuwe Macho – Makangale.

- Katika kuimarisha usalama wa watalii na mali zao, Kamisheni ya Utalii imekabidhi radio za mawasiliano mbili (2) na *"Walkie Talkie"* kumi (10) kwa wafanyakazi wa kitengo cha Patrol kwa ajili ya kazi za usalama wa watalii.

Mhe. Spika, Kamisheni imefanikiwa kupata tunzo iliyotolewa na *"CTW Chinese Tourist Welcoming Award 2010*", katika maonyesho ya *COTTM* yaliyofanyika Beijing China mwezi Aprili 2010. Tunzo hii imetolewa na taasisi ya utafiti ya soko la nje la utalii ya China *(China Outbound Tourism Research Institute)* kwa kutambua umuhimu na mchango wa Kamisheni ya Utalii katika utafutaji wa masoko ya Utalii. Taasisi hii hutoa tunzo Kwa makampuni ya kimataifa ya utalii na kwa taasisi zinazotoa huduma na bidhaa bora katika kukuza soko la nje la utalii la China. Aidha, ni fakhari kubwa kwetu kulijuilisha Baraza lako yukufu kwamba, *Hoteli za La Gemma Dell Est na The Z Hotel* nazo zimepata tunzo ya Utalii Duniani *(World Travel and Tourism Award).*

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo kwa upande wa Shirika la Utalii na Hoteli ya Bwawani ni kama ifuatavyo:-

- Shirika limeweza kumpatia nafasi ya masomo mfanyakazi mmoja katika ngazi ya Digirii ya kwanza nchini Malaysia katika fani ya Uchumi na Mfanyakazi mwengine tayari amemaliza mafunzo ya Uandishi wa habari katika kiwango cha Diploma.

- Jumla ya vyumba sita (6) vya Hoteli ya Bwawani vimefanyiwa matengenezo sawa na asilimia 60% ya lengo. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kukosekana kwa umeme kwa kipindi

cha miezi mitatu kumechangia kushuka kwa mapato ya Hoteli kwa hiyo kushindwa kufikia malengo.

- Hoteli imeendelea kutumika kama kituo cha elimu kwa vitendo (Practicals) kwa wanafunzi kutoka Chuo cha Utalii.

- Hadi kufikia Machi 2009/2010 Hoteli imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shs. 715.00 milioni sawa na asilimia 88 ya lengo lililowekwa.

Mhe. Spika, kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Kamisheni imejiwekea malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonesho ya kitalii na mikutano ya kimataifa. Mkazo zaidi ni kutangaza katika masoko mapya kama vile Urusi, China na Mashariki ya Mbali. Mbinu za kisasa zitatumika ili kuhakikisha lengo hili linafanikiwa.

- Kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii na mali zao kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

- Kukamilisha kazi ya kuandaa Mpango Kazi wa uendeshaji utalii wa baharini (*Marine Tourism Management Plan*) kwa kushirikiana na Mradi wa MACEMP.

- Uchapishaji wa kalenda za ukutani (*Scroll wall calenders*), kuliendeleza jarida la Karibu Zanzibar na kuchapisha muongozo wa malazi (*Accomodation Guide*), *CD ROM* na *DVD*.

- Kuimarisha vitengo vya mipango na masoko kwa kuvipatia vitendea kazi na utaalamu kwa watendaji wake.

- Kushajihisha uandaaji wa michezo mbalimbali ya utalii ikiwemo Tamasha la Mzanzibari, Mwaka Kogwa, Marathon, Triathlon, Mountain Bike, Tamasha la Nchi za Majahazi, Sauti za Busara na Siku ya Utalii Duniani.

- Kuendelea na utafiti wa uingiaji wageni (*Tourism Sector Survey*) kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Mali Asili na Utalii (Bara) ili kujua mapato halisi ya wageni wanaoingia nchini.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii ilikadiriwa kukusanya mapato Tzs. 813,800,000/= kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Mpaka kufikia mwezi Machi 2010, Kamisheni imefanikiwa kukusanya Tzs 609,750,000/= ambayo ni asilimia sabiini na tano (75%) ya lengo.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Tzs. 737,000,000/= ili Kamisheni ya Utalii iweze kutekeleza kazi zake za kawaida, pamoja na shughuli kubwa ya kuitangaza nchi yetu kiutalii ulimwenguni.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII:

Mhe. Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Chuo kimeweza kufanya kazi zifuatazo:-

- Upimaji wa eneo la Chuo na kupata hati miliki. Eneo la Chuo hicho lilikuwa linamilikiwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale iliyo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ukosefu wa hati ya umiliki wa eneo kwa chuo ulikwamisha taratibu za usanifu wa majengo na matumizi ya ardhi. Upatikanali wa Hati hiyo imekiwezesha Chuo kutayarisha mpango wa matumizi ya eneo na kazi ya kuandaa michoro ya ujenzi inaendelea.

- Chuo kimefanikiwa kuandaa mitaala ambayo imekubaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), na sasa kimo katika hatua ya mwisho kujiunga na *NACTE* katika kiwango cha "National Technical Award – *NTA*" katika ngazi ya 7 na 8. Hatua hii itavifanya vyeti vinavyotolewa na Chuo cha Utalii cha Zanzibar, kutambulika Kitaifa na Kimataifa. Aidha Chuo kimejiunga na Shirika la Kimataifa linalotoa Elimu ya Hoteli na Utalii katika viwango vya kimataifa (*Confederation of Tourism Hospitality*) pamoja na kujisajili na umoja wa vyuo vya hoteli na utalii vya dunia (*Global Confederation of Tourism and Hospitality Accreditation Board*),

- Ukarabati wa Mkahawa kwa ajili ya kufundishia pamoja na vifaa vyake umekamilika.

- Chuo kimefanikiwa kusomesha walimu watano (5) waliohitimu mafunzo ya awali ya msingi (*competence Based education Training*) pia wafanyakazi wengine kumi na saba (17) wako masomoni katika mafunzo mbali mbali kama inavyoonekaka katika *Kiambatisho nambari 5.*

- Chuo kimesajili wanafunzi wapya 701 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 160 ukilinganisha na wanafunzi 541 kwa mwaka 2008/2009, kama inavyoonekana *katika jadweli nambari 5*.

Jadweli Nambari 5: Idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kwa Mujibu wa Viwango vya masomo kwa 2009/2010:

COURSE	FOUNDATION		CERTIFICATE		DIPLOMA		
	MALE	FEMALE	MALE	FEMALE	MALE	FEMALE	TOTAL
HOSPITALITY AND TOURIM MANAGEMENT					34	9	43
ICT AND ACCOUNTING	9	7			24	5	45
FRONT OFFICE	24	9	22	13			68
FOOD PRODUCTION	85	19	39	23			166
FOOD AND BEVERAGE	31	11	22	3			67
HOUSEKEEPING	11	20	5	12			48
OUTREACH PROGRAMMES	128	72					200
TOUR GUIDING			7	-			7
TAILOR MADE COURSES	13	9					22
INCUBATOR WITHOUT WALLS	14	21					35
TOTAL	**315**	**168**	**95**	**51**	**58**	**14**	**701**

- Chuo kimeweza kuanzisha tovuti (*web-site*) yenye anuani www.zito.org. pia zimenunuliwa kompyuta ndogo (*laptops*) 10 kwa ajili ya kitengo cha mafunzo ya teknolojia ya komputa na Uhasibu, generata, projector, vifaa vya kutunzia bustani pamoja na viti, meza na miamvuli.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho, uteuzi wa Baraza la Chuo umekamilika kama inavyoelekeza Sheria namba 7 ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii ya mwaka 2008. Matumaini yetu ni kwamba, kuwepo kwa Baraza la Chuo kutakamilisha mfumo wa usimamizi wa kazi za Chuo na kuongeza ufanisi.

Mhe. Spika, hali ya kifedha ya Chuo hadi kufikia Machi, 2010 inaonyesha kuwa kiliweza kupata jumla ya Tzs 257 milioni. Kati ya fedha hizo Tzs 191

milioni sawa na asilimia 60 ya lengo ni Ruzuku kutoka Serikalini na Tzs 66 milioni ambayo ni sawa na asilimia 55 ya lengo kutokana na ada za masomo *(fees).*

Mhe. Spika, chuo kimeanzisha mpango maalum wa mafunzo kwa wakufunzi (*Training for the Trainers programmes -TOT*) na kinategemea kupata Voluntia watatu (3), mmoja kutoka VSO atakaefundisha fani ya utalii endelevu (*Sustainable tourism*), na wawili kutoka JICA kwa ajili ya mafunzo ya kompyuta na jikoni (*Cook*).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, mbali ya kazi za kawaida za usajili na ufundishaji wa wanafunzi, chuo kitatekeleza kazi zifuatazo;

- Kuyafanyia ukarabati majengo ya Chuo na kukamilisha michoro ya majengo mapya, na hali ikiruhusu kuanza ujenzi.

- Kuendelea kuwasiliana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank - ADB)* ambao wameonyesha nia ya kukijenga upya chuo na kukipatia vifaa kwa gharama inayofikia dola za kimarekeni milioni tatu kuanzia mwaka 2011/2012.

- Kuajiri walimu wapya na wenye taaluma za kisasa ili kuimarisha ubora wa kiwango cha ufundishaji pamoja na kuimarisha mitaala ili iendane na mahitaji halisi.

- Kuandaa mpango wa kitaaluma, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii, ZATO na ZATI, wa kufanya *BRANDING ZANZIBAR.*

- Kuandaa mapendekezo ya Kanuni za Sheria ya Chuo, Kanuni za Utumishi na usimamizi wa fedha.

- Kuandaa mafunzo ya muda mfupi (*Crash programs*) kwa watu au taasisi zenye mahitaji maalum.

- Kufanya tafiti juu ya mabadiliko ya mahitaji katika sekta na kutoa huduma za ushauri kwa watakaohitaji.

- Kuandaa mpango kazi wa chuo wa muda mrefu na muda wa kati.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 chuo kinategemea kutumia jumla ya shilingi 650 (Tzs 500 milioni ruzuku kutoka Serikalini na Tzs 150 milioni kutoka katika vyanzo vya mapato ya Chuo) kwa kazi za kawaida na shilingi 500 milioni zimetengwa kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Shirika la utalii limejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuendelea kutafuta wabia kwa nia ya kushirikiana nao katika uwekezaji wa maeneo ya Shirika huko Kuji na Vitongoji kisiwani Pemba.

- Kuendeleza jitihada za kuwaelimisha wafanyakazi wa Shirika, ikiwamo kuwapeleka masomoni alau wafanyakazi watatu katika ngazi ya Stashahada.

- Kuendeleza juhudi za kutafuta ufadhili wa kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la *LIVINGSTONE HOUSE* na kuliwezesha kutumika kibiashara.

- Kukusanya jumla ya TZS. 253,230,000.00 na kuwa na matumizi yasiyozidi TZS. 211,681,712.00

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Hoteli imejiwekea malengo yafuatayo:-

- Kuinua kiwango cha utendaji wa kazi ambapo Hoteli imelenga kuwajengea uwezo zaidi wafanyakazi wake kama jadweli inavyoonesha hapo chini:-

S/No.	Idadi ya W'kazi	Aina ya Mafunzo	Chuo	Muda wa Mafunzo
1.	2	Diploma ya Uongozi wa Hoteli.	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Miaka miwili
2.	1	Uhasibu	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mwaka mmoja

3.	1	Utawala	Chuo cha Utawala wa Umma – Zanzibar	Mwaka mmoja
4.	1	Kompyuta	Chuo cha Ufundi Karume	Mwaka mmoja

- Kuendelea na mipamgo yake ya matengenezo ya vyumba 10 vya kulala wageni na kumbi tatu za mikutano.

- Kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Hoteli itaendelea kuwapatia mafunzo ya vitendo wanafunzi wa Chuo pamoja na taasisi nyengine katika Nyanja za upishi, utunzaji nyumba, huduma za vyakula na vinywaji na mapokezi.

- Kukusanya kiasi cha Shs. 758 milioni na kufanya matumizi ya Shs. 672.45 milioni ya mapato hayo.

SEKTA YA BIASHARA:

Mhe. Spika, Sekta ya Biashara imeundwa na Idara ya Biashara, Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) na Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*). Biashara ni miongoni mwa sekta zilizopewa umuhimu katika utekelezaji wa MKUZA. Wizara kupitia sekta hii ina majukumu ya kuweka mazingira bora ya kibiashara, kisera, kisheria pamoja na kutoa fursa kwa sekta binafsi kuweza kufanya biashara. Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) lina wajibu wa kutafuta masoko, kununua, kuuza na kusafirisha karafuu pamoja na bidhaa zinazozalishwa na Kiwanda cha mafuta ya Makonyo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Sekta ya Biashara ilijipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Ukaguzi wa mezani 2100 na vipimo, ukaguzi wa madukani 1,233, maghala 171 na *"supermarket 3",* kutoa mafunzo kwa wafanyakazi watano (5), wafanyabiashara na wajasiriamali hamsini (50), kutoa taarifa ya hali ya chakula, biashara na masoko kwa kila mwezi, na kushiriki katika maonesho ya biashara.

  - Kuendeleza mazingira mazuri ya biashara ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya sheria zinazoendana na masuala ya biashara. (Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Na. 2 ya mwaka 1995, Sheria ya biashara

No 4 ya mwaka 1989, na Sheria no 4 ya mwaka 1983 ya mezani na vipimo).

- Kukusanya mapato ya Tsh 26,000,000 yanayotokana na ukaguzi wa mezani (2100), vituo vya mafuta (34) na *"under ground tank (102)",* magari ya mafuta (17), na usajili wa wafanyabiashara, na kuchangia mfuko mkuu wa Serikali

- Kununuliwa kifaa maalum *(prooving tank)* kwa ajili ya ukaguzi wa matangi ya chini katika vituo vya mafuta.

- Kufanya mapitio ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara kupitia mradi utakaofadhiliwa na *BEST.*

- Kwa upande wa shirika la Magari, kuendelea na biashara ya utoaji huduma za karakana, ukodishwaji majengo, udhibiti wa uingizaji wa magari nchini na uwakala wa Bima ya vyombo vya moto, pamoja na kukusanya Tzs 220,585,469.50 ikiwa ni mapato yatokanayo na kazi hizo.

- *ZSTC* ilipanga kununua tani 3,200 za karafuu kwa thamani ya Tzs. 10,240.00 milioni na kuuza tani 3,040 zenye thamani ya Tzs. 15,507.00 milioni ambazo ni sawa na US$. 11,569,000 milioni.

- Kufanya mauzo ya bidhaa zenye thamani ya Tzs 600.00 Milioni katika tawi la *ZSTC* Dar-es-Salaam.

- Kupeleka tani 300 za karafuu katika tawi la Dubai, na kuuza tani 297.0 kwa US$ 1.247 Milioni sawa na Tzs.1,659.042 Milioni

- Kiwanda cha Makonyo kilikadiria kuzalisha idadi ya kilo 29,460 za Mafuta ya viungo, na kuyauza kwa thamani ya Tshs. 313millioni, kama inavyoonekana katika jedwali iliyopo hapo chini.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, katika kuweka mazingira mazuri ya Biashara mbali na kupitia, kutekeleza na kusimamia sheria zinazoendana na biashara, Wizara imefanyia kazi wito wa wajumbe wa Baraza lako wa kuona haja ya kuwepo Uwanja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa hapa Zanzibar. Katika kutekeleza hilo Wizara imefanikiwa kupata eneo lenye urefu wa kilomita 1 na upana wa kilomita 0.6. katika Maeneo Huru ya Kiuchumi yaliyopo kijiji cha Ndaambani,

Shehia ya Dimani. Eneo hilo tayari limeshapimwa na kuwekewa mipaka. Wizara inaendelea kufanya tathmini ya mazao ya wakulima kwa ajili ya matayarisho ya fidia ya vipando vyao. Hatua nyengine zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na Wafanyabiashara wa nchini China katika kufanya michoro na upangaji wa eneo.

Kuhusu kufanya Utafiti kwa ajili ya Kuifanya Zanzibar kuwa eneo huru la kiuchumi, wizara imetayarisha maelezo ya mradi (*Concept paper*), pamoja na hadidu rejea (*TOR*) kwa ajili ya utafiti wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (SEZ). Mradi huu umewasilishwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kupatiwa fedha ili kumtafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti huo.

Mhe. Spika, wizara imetayarisha rasimu ya awali ya sheria ya viwango kwa ajili ya kuwa na udhibiti wa viwango na ubora wa bidhaa hapa Zanzibar. Rasimu ya sheria hiyo hivi sasa inatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi husika za Serikali kwa mujibu wa taratibu zilivyo ili kupitishwa kuwa sheria. Mhe. Spika, maelezo ya utekelezaji malengo na maombi ya fedha kwa mwaka 2010-2011 yanaonekana ukurasa wa 34 – 38.

Mapendekezo ya awali kwa ajili ya mapitio ya mfumo wa utoaji leseni chini ya Taasisi moja tayari yameshaandaliwa. Kazi hii inafanywa kwa mashirikiano na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Mchakato wa kumtafuta mshauri mwelekezi unaendelea ili hatua za mapitio zianze mapema iwezekenavyo. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia *BEST*.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2010, Idara imekusanya jumla ya Tshs. 16,000,000 sawa na asilimia 61.5, ya malengo. Lengo kamili halikufikiwa kwa sababu kazi ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ukaguzi wa matangi ya chini ya ardhi *(underground tank)* katika vituo vya mafuta na magari ya kusambazia mafuta haikufanyika kutokana na sababu za kitaalamu zikiwemo upungufu wa mafuta kwenye vituo.

Mhe. Spika, mbali na maelezo yaliyotolewa hapo juu, Malengo mengine yaliyotekelezwa na Idara ya Biashara yanaonekana katika *Kiambatisho Nambari 8*.

Mhe. Spika, ili Idara ya Biashara iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2010/2011 inaombewa jumla ya Tzs 172,137,000/= kwa kazi za kawaida na Tzs. 1,136,000,000 kwa kazi maendeleo.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi,2010 Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) lilinunua jumla ya tani 2728.954 sawa na asilimia 85.30% ya lengo

zilizogharimu jumla ya Tzs. 8,243,019,250 katika kipindi hicho Shirika liliweza kuuza jumla ya tani 2383 zenye thamani ya Tzs. 10,985,464,351.00 sawa na US$. 8,394,950.

Shirika pia liliweza kukusanya jumla ya Tzs. 301, 767,000.00 kutokana na kodi za majengo yake likiwemo Jengo la Kitega Uchumi liliopo Gulioni Unguja.

Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo - Pemba kiliweza kufanya uzalishaji kilo 15,780 za mafuta ya viungo na kuuza kwa thamani ya Tshs. 184,688,510 kama inavyoonekana katika jedwali zifuatazo:-

Nam.	Aina ya Mafuta	Lengo (KG)	Uzalishaji (KG)
1	Mafuta ya Makonyo	27,000	14,000
2	Mafuta ya Mdalasini	60	40
3	Mafuta ya Mkaratusi Manukato	500	700
4	Mafuta ya Mkaratusi Madawa	800	400
5	Mafuta ya Majani ya Mkarafuu	100	600
6	Mafuta ya Mchaichai	1,000	40

Kiwanda hadi kufikia Machi 2010 kiliuza mafuta ya mimea kama inavyoonesha katika jadweli hapo chini.

Nam.	Aina ya Mafuta	Uzito (KG)	Thamani (Tzs)
1	Mafuta ya Makonyo	14000	157,480,000
2	Mafuta ya Mdalasini	22	900,000
3	Mafuta ya mchaichai	40	2,200,000
4	Mafuta ya majani ya karafuu	600	9,000,000
5	Mafuta ya mrehani	11	732,000
6	Mafuta ya mkaratusi (madawa)	400	5,279,220
7	Mafuta ya mkaratusi (manukato)	700	9,097,290

Mhe. Spika, kwa upande wa Tawi la Shirika la Biashara la Taifa - Dar es Salaam limefanikiwa kufanya biashara ya mauzo ya bidhaa na kukusanya Tzs 916.200 Milioni ambazo ni ongezeko la asilimia 113% ya makadirio.

Tawi la *ZSTC* – Dubai hadi kufikia March, 2010 liliweza kufanya mauzo ya tani 287.05 za karafuu zenye thamani ya US$. 1,113,268.32 sawa na Tzs. 1,730,619,611.50.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2010 Shirika lilitumia jumla ya Tzs 3,077.817 Milioni katika kazi zake za kawaida ikiwa ni gharama za uendeshaji, gharama za kifedha zikiwemo riba na dhamana za mikopo na gharama za masoko.

Kwa mwaka 2009/2010, Shirika la Biashara ya Magari Lilinunua na kuuza bidhaa zenye thamani ya Tzs. 318,310,000/= sawa na asilimia 82.91 ya lengo, kwa robo tatu (3) za kuishia mwaka. Ambapo Shirika limepata mapato ya Tzs. 56,193,900/= kutokana na Biashara hiyo, sawa na asilimia sitini na tisa (69%) ya lengo. Shirika la Biashara ya Magari, mbali na majukumu yake ya kimsingi iliyoainishwa kabla, pia hutoa huduma nyenginezo kwa madhumuni ya kuliongezea mapato Shirika.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010, Shirika limeweza kutoa huduma nyenginezo kama ifuatavyo:

(i)	Ukodishwaji wa Majengo	Tzs. 37,851,040/=
(ii)	Huduma za Workshop	Tzs. 4,927,640/=
(iii)	Ada ya Uingizaji na Usafirishaji vyombo vya moto	Tzs. 172,662,124/=
(iv)	Ujira wa Uwakala wa Bima	Tzs. 539,814/=
	Jumla	**Tzs. 215,930,618/=**

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Uingizaji Magari nchini, katika kusimamia kikamilifu Sheria Nam. 7 ya mwaka 1985, jumla ya vyombo vya moto 3,638 vimeruhusiwa kuingizwa nchini, vyombo vya moto 795 vimeruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi kisheria. Uingizwaji na Usafirishwaji wa vyombo hivyo, umelipatia Shirika jumla ya Tzs. 172,612,124/= kwa mwaka huo wa Fedha. Utekelezaji wa kazi hiyo, umevuka lengo kwa asilimia arobaini na nne (44%).

Aidha, wafanyakazi watatu wamepelekwa masomoni kujifunza fani ya Uhasibu, Kompyuta, Uboharia na Uhakiki wa Hesabu za ndani.

Mhe. Spika, katika mwaka wa Fedha 2009/2010, Shirika la Biashara ya Magari limekusanya jumla ya mapato ya Tzs. 520,680,892/=. Makusanyo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mhe.	Mauzo na ulipwaji madeni	Tzs. 304,750,276.00
	Ujira wa Bima	Tzs. 539,814.00
	Ada ya huduma nyenginezo	Tzs. 172,612,124.00
	Kodi ya Majengo	Tzs. 37,851,040.00
	Semina	Tzs. 4,927,640.00
	Jumla	**Tzs. 520,680,894.00**

Spika, hadi kufikia Machi 2010, Jumla ya Tshs. 453.9 milioni zilitumika kama ifuatavyo:-

Ulipaji wa Ununuzi wa bidhaa	Tzs. 318,310,000.00
Mishahara na Marupurupu	Tzs. 72,472,077.00
masomo	Tzs. 2,220,000.00
Gharama za semina	Tzs. 652,000.00
Safari za kikazi	Tzs. 7,803,000.00
Matumizi ya kuendeshea kazi	Tzs. 29,220,280.00
Halmashauri ya Magari	Tzs. 7,626,000.00
Misaada na Michango	Tzs. 1,561,451.00
Mchango wa ZSSF	Tzs. 6,522,000.00
Mchango wa Hazina	Tzs. 7,521,969.00
Jumla:	**Tzs. 453,908,777.00**

Malengo ya sekta ya biashara kwa 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

Idara ya Biashara

- Kuendeleza mazingira mazuri ya biashara yakiwemo:
  - Kukamilisha matayarisho ya Sheria ya viwango na ubora wa bidhaa;
  - Kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*), na kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi (*Land Use Plan*) kwa ajili ya uwanja wa maonesho ya biashra ya kimataifa ili kupata wafadhili;
  - Kufanya mchakato juu ya mapitio ya mfumo wa utoaji wa leseni na mapitio sheria ya leseni nam 4 mwaka 1983.

- Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuifanya Zanzíbar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi (*Special Economic Zones*);

- Kuanza mchakato wa mapitio ya será ya biashara ili ikidhi matakwa ya Kikanda na kimataifa; na

- Kukusanya mapato ya Tzs 23,000,000 yanayotokana na ukaguzi wa mezani 2500, vituo vya mafuta 38, na usajili wa wafanyabiashara, pamoja na ukaguzi wa madukani 2000, maghala 172 na supermarket 10, na kuingia katika mfuko mkuu wa serikali.

- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi watano (5), wafanyabiashara na wajasiriamali hamsini (50);
- Kuendelea kushiriki katika majadiliano ya Kikanda na ya Kimataifa

Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC*

- Kununua tani za karafuu 3,200.0 kwa Tzs. 10,560.00 Milioni;
- Kuuza tani 2,850 kwa Tzs. 14,183.025 sawa na US$ 10,545,000.
- Kusafirisha tani 300 kupeleka katika Tawi la Dubai;

Mhe. Spika, kiwanda cha Makonyo kinakadiria kuzalisha kilo 27,032 na kuuza kwa thamani ya Tshs. 358,934milioni.

AINA YA MAFUTA	UZITO (KGS)	THAMANI (MILIONI Tzs)
Mafuta ya Makonyo	24,000	311,520,000
Mafuta ya Mkaratusi – Madawa	600	8,510,000
Mafuta ya Mkaratusi – Manukato	800	10,154,000
Mafuta ya Mchaichai	70	3,850,000
Mafuta ya Majani ya Mkarafuu	1,500	22,500,000
Mafuta ya Mdalasini	60	2,400,000

Mhe. Spika,Tawi la *ZSTC* Dar-es-Salaam linatarajiwa kufanya mauzo ya jumla ya Tzs. 990.000 Milioni katika mwaka wa fedha 2010/2011. Kati ya hizo Tzs.

198.000 Milioni ikiwa ni mauzo ya vyakula na vinywaji na Tzs. 792.000 Milioni ni mauzo ya vifaa vya ujenzi na vifaa vya majumbani.

Kwa ujumla Shirika linatarajia kukusanya mapato ya Tzs 397.834 Millioni kwa mpango ufuatao:-

- Kodi ya Jengo la kitega Uchumi (***ZSTC Investment Building***) Tzs. 365.250 Milioni.
- Kodi za maghala Tzs. 21.120 Milioni.
- Mapato ya kiwanda cha mbao, uuzaji wa pishi na kandili. Tzs. 11.464 Milioni

Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yanatarajiwa kufikia jumla ya Tzs. 3,485.025 Milioni ikiwa ni gharama za uendeshaji wa Shirika ikiwemo mishahara, viinua mgongo, maslahi ya wafanyakazi na mafuta.

Mhe. Spika, Shirika la Biashara ya Magari, katika mwaka wa fedha 2010/2011 limepanga kutumia Tzs. 511,840,000.00 kwa kutekeleza malengo iliyojipangia ya ununuzi wa bidhaa na kutoa huduma.

Mhe. Spika, fedha hizo zitatokana na vianzio vifutavyo:

- Kununua na kuuza vyombo vya moto, vyarahani na baiskeli;
- Kuendelea na Uwakala wa Bima ya vipando vya moto;
- Kusimamia Udhibiti wa Uingizaji, Umiliki na Usafirishaji wa vyombo vya moto nchini;
- Ukodishwaji wa Majengo
- Huduma za Karakana
- Ada ya Uingizaji na Usafirishaji Magari
- Ada ya Uwakala wa Bima

Mhe. Spika,kutokana na mapato yaliyoainishwa hapo juu, maeneo ya matumizi ni kama yafuatayo:

- Kulipa Viinua Mgongo kwa wafanyakazi washirika watakaostaafu;
- Kuchangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi wa Shirika;
- Kuwapatia mafunzo wafanyakazi;
- Kuendeleza mpango wa kuyafanyia matengenezo majengo ya Shirika; Kuchangia miradi ya maendeleo na huduma za Ustawi

wa Jamii;

- Kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Shirika linategemea kulipa mafao ya wastaafu watano (5) jumla ya wa Tzs. 62,368,723/=. Aidha, shirika litalipa mchango wake wa ZSSF kama sheria inavyoelekeza.

Kuyafanyia matengenezo Majengo yake ya Unguja na Pemba, ili kuyaweka katika hali nzuri.

Kuchangia jumla ya Tzs. 13,390,506.51 milioni katika mfuko mkuu wa Serikali kutokana na faida itakayopatikana.

SEKTA YA VIWANDA:

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda kwa Zanzibar hujumuisha zaidi viwanda vidogo na vya kati vinavyomilikiwa na watu binafsi. Ukuaji wa Sekta hii hapa Zanzibar si wakuridhisha, kutokana na wawekezaji wetu wa ndani kujikita zaidi katika biashara ya kununua na kuuza pamoja na ile ya utalii ambazo huwapatia mapato ya haraka.

Viwanda vidogo vidogo na vya kati viliopo hapa Zanzibar vinajumuisha usindikaji wa matunda na viungo, utengenezaji wa mafuta ya arki, useremala, utengenezaji wa mikate, utengenezaji wa chokaa, uvunjaji wa kokoto, uzalishaji maji, vinywaji baridi, sukari, matofali na mafuta ya nazi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Maendeleo ya Viwanda ililenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea na matayarisho na kusambaza vijarida elfu tano (5,000) vya sera ya Viwanda / Biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs) iliyotayarishwa kwa lugha nyepesi (*Popular Version*).

- Kutayarisha *"Database"* ya Viwanda (*Industrial Database*) ambayo itasaidia kuweka kumbukumbu zote muhimu za Viwanda viliopo hapa nchini kupitia program ya JP5.

- Kuendelea kutoa mafunzo yakiwemo ya usindikaji wa vyakula kwa Wajasiriamali mia mbili na tano (205) kwa Unguja na Pemba kupitia Programu ya JP5.

- Kuandaa utaratibu maalumu wa kuwatembelea wajasiriamali waliopatiwa mafunzo ya usindikaji wa vyakula, uzalishaji wa

Uyoga, utengenezaji vikoi, huduma za Biashara (BDS) ili kujua maendeleo yao na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

- Kuendeleza mradi wa Nishati mbadala uliopo katika kijiji cha Kisakasaka kwa kushirikiana na *UNIDO*.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Spika, wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda imefanikiwa kutekeleza kazi zilizoanishwa katika ukurasa wa 48 – 50 na malengo na maombi ya fedha kwa mwaka 2010-2011 yanaonekana katika ukurasa wa 51-54.

- Kuchapishwa na kusambazwa vijarida elfu mbili (2000) vya Sera ya Viwanda /Biashara ndogo na za kati (*SMEs*) iliyotayarishwa kwa lugha nyepesi. Idadi hii ni sawa na asilimia arobaini ya lengo (40%).

- Kuanza matayarisho ya awali ya uwekaji wa takwimu sahihi za maendeleo ya viwanda (*industrial database*) ikiwemo ununuzi wa Kompyuta moja (1) na kupata mafunzo ya takwimu kwa maafisa 3 wa Idara yaliyotolewa na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

- Kutoa mafunzo ya usindikaji wa mazao ya kilimo na Bahari kwa walimu wa wanafunzi (*TOT*), Elimu ya ujasiriamali na uendeshaji Biashara, Elimu ya kuongeza thamani kwa zao la mwani kwa Wazalishaji, Wajasiriamali na baadhi ya maafisa wa Idara ya Viwanda. Jumla ya washiriki sabini na moja (71) wa Unguja na Pemba walipata mafunzo hayo kupitia mradi wa *JP5*.

- Kutembelea vikundi vya wazalishaji/wajasiriamali hamsini (50) waliopatiwa mafunzo ya usindikaji wa vyakula, uzalishaji uyoga, utengenezaji Vikoi, Huduma za Biashara (BDS), na Elimu ya ujasiriamali ili kujua maendeleo yao na changamoto zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yao. *Angalia Kiambatisho Nambari 3.*

- Kutembelea Viwanda vidogo na vya kati thalathini na moja (31) vinavyozalisha bidhaa mbali mbali ikiwemo maji, tambi, sukari, vinywaji baridi, samani, matofali, mafuta ya nazi, sabuni, mazulia, chumvi, makubadhi, vyungu, na vyetezo. *Angalia kiambatisho Nambari 4.*

- Kukamilika kwa mradi wa nishati mbadala (*Renewable Energy*) uliopo katika kijiji cha Kisakasaka na kuanza kutumika kwa majaribio.

Mhe. Spika, pamoja na utekelezaji huo wa malengo katika kipindi hicho (2009/2010). Idara ilifanikiwa pia kutekeleza mambo kadhaa ikiwemo:-

- Kushirikiana na taasisi nyengine (Idara ya Biashara, WKMVWW, ZNCCIA, UWAZI n.k) katika kuratibu na kufanikisha ushiriki wa Wajasiriamali kutoka vikundi thelathini na sita (36) vya Zanzibar katika maonesho ya saba - saba katika mwezi wa Julai 2009.

- Kufanya majaribio ya kuongeza thamani kwa zao la mwani (***Value addition***) kwa kutengeneza bidhaa za chakula, juice na sabuni.
- Kukamilisha ujenzi na kuanza kutumika kwa kiwanda cha kukaushia matunda na viungo Pemba, na kurekebisha baadhi ya sehemu ya kiwanda cha kukaushia samaki kilichopo katika kijiji cha Nungwi.

- Kushiriki katika vikao vya kujadili rasimu ya sera ya Maendeleo ya Viwanda na ile ya Viwanda /Biashara ndogo ndogo na za kati za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda, imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuchapisha na kusambaza vijarida elfu mbili (2,000) vya Sera ya Viwanda /Biashara ndogo ndogo na za kati (*SMEs*) iliyotayarishwa kwa lugha nyepesi (*Popular Version*).

- Kukamilisha *"Database"* ya Viwanda (*Industrial Database*) kupitia Programu ya JP5.

- Kutoa mafunzo ya kuongeza thamani (value addition) kwa zao la mwani, "Packaging", Masoko (Marketing technique), udhibiti na Ubora wa bidhaa (Quality Control/Assurance) na ubunifu wa bidhaa (Products design) kwa Wajasiriamali mia moja na ishirini na tano (125) (Unguja – 80, Pemba 45).
- Kukamilisha ukarabati wa kituo cha majaribio ya ukaushaji wa Samaki kilichopo Nungwi.

- Kushirikiana na Idara ya Mipango na Sera na Wadau wengine wa sekta ya Viwanda (Wajasiriamali/Wazalishaji, Wawekezaji katika Sekta ya Viwanda na Washirika wa Maendeleo) kuifanyia mapitio (*Review*) Sera ya Maendeleo ya Viwanda ya mwaka 1998 – 2008.

Mhe. Spika, ili iweza kutekeleza malengo hayo, Idara ya Viwanda inaombewa Tzs 72,196,000/= kwa kazi za kawaida.

SEKTA YA UWEKEZAJI:

Mhe. Spika, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega uchumi ni Taasisi iliyoundwa kwa Sheria Nam.11 ya mwaka 2004 ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji na Vitega Uchumi kutoka mitaji binafsi na kusimamia Maeneo Huru ya Uchumi na Bandari Huru. Utekelezaji wa malengo na malengo ya mwaka 2010-2011 katika kipindi cha 2009-2010 yanaonekana ukurasa wa 54-59.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 Mamlaka ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kutathmini miradi iliyoidhinishwa na kujua hadhi zao za utendaji kazi na kuondosha katika kumbukumbu za Mamlaka miradi ambayo imeshindwa kutekelezwa kutokana na sababu mbali mbali.

- Kuimarisha mahusiano na wawekezaji kwa kuwaenzi wawekezaji waliopo na kuvutia wengine kwa kuweka mkazo wawekezaji kutoka nchi za Ulaya Mashariki, kuwekeza Zanzibar.

- Kuimarisha miundo mbinu katika Maeneo Huru ya Uchumi na Bandari Huru.

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo hayo katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ulikuwa kama ifuatavyo;

- Jumla ya miradi 65 ilifanyiwa tathmini. Miradi mitano 5 kati ya hiyo ilibainika kutoendelezwa kutokana na sababu za kukosa mitaji kutoka vyanzo vilivyotegemewa, na pia kushindwa kutimiza masharti ya uwekezaji kisheria yaliyoainishwa kwenye vyombo vya Serikali. Hali hiyo imepelekea miradi hiyo kufutwa na kuondoshwa katika kumbukumbu za miradi iliyoidhinishwa.

- Hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya miradi mipya 34 iliyokadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Marekani 270.4 milioni iliidhinishwa. Miradi hiyo ni ya sekta za kilimo, utalii, usafiri, biashara na viwanda. Kati ya hiyo 13 ni ya wazalendo sawa na asilimia 38, na 15 ambayo ni asilimia 44 iko katika sekta ya utalii kama jadweli inavyoonekana hapo chini:-

MUHTASARI WA MIRADI ILIYOIDHINISHWA 2009:

S/NO.	ENEO LA UWEKEZAJI	IDADI	MTAJI
1.	Kilimo, usasi na misitu	1	3,900,000.00
2.	Uzalishaji viwandani	3	3,857,671.00
3.	Biashara jumla/rejareja	8	9,508,880.00
4.	Hoteli na Mikahawa	15	110,603,884.70
5.	Usafirishaji na Mawasiliano	1	4,900,000.00
6.	Huduma za kifedha	1	201,226.15
7.	Majengo na nyumba za kibiashara	3	137,017,000.00
8.	Elimu	0	-
9.	Afya	0	-
10.	Huduma za kijamii	2	433,000.00
	Jumla:	**34**	**270,421,661.85**

- Kazi ya uenezi kwa ajili ya kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar zilifanywa kwa kiwango cha kuridhisha kulinganisha na uwezo wa kifedha wa Mamlaka. Mkazo umewekwa katika kuwahamasisha wazalendo kuwekeza. Jumla ya vipeperushi 2000 vimechapishwa na kusambazwa kwa wafanyabiashara. Aidha, kalenda za ukutani, vitabu vya kumbukumbu vya mezani (Diaries) na vifaa vyengine ambavyo vyote vinatangaza fursa za uwekezaji kwa wazalendo vimetayarishwa na kusambazwa.

- Katika kuvutia uwekezaji kutoka nje, Mamlaka imetumia fursa ya ziara za Viongozi wa Kitaifa nchi za nje, katika utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi, na kushiriki kutangaza fursa za uwekezaji na biashara kupitia makongamano katika nchi za Uturuki, Falme za Kiarabu, Malaysia, India na Irani.

- Kupitia Jumuiya ya Mamlaka za Uwekezaji za nchi wanachama wa Afrika Mashariki, ambapo ZIPA ni mwanachama, fursa za

uwekezaji zimetangazwa ndani ya Afrika Mashariki na katika nchi za Canada na Uingereza. Matokeo ya ziara hizo ni kujitokeza kwa wawekezaji walioonyesha nia ambao wengi wanaendelea na tafiti zitazowapelekea kufanya maamuzi ya kuja kuwekeza.

- Huduma kwa wawekezaji zimeendelea kutolewa kwa mashirikiano na taasisi nyengine za Serikali kama vile Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi na Idara ya Ardhi na Usajili. Hata hivyo bado dhana ya kituo kimoja cha uwekezaji

  (One stop facilitation centre) haijaweza kutekelezwa kwa ukamilifu, jambo ambalo Wizara inalifanyia kazi.

  Katika mwaka 2009/2010 jumla ya maombi 310 ya vibali vya kazi na ukaazi yalipokelewa. Kati ya hayo maombi 207 ni mapya, 103 ni ya kuongeza muda. Maombi 45 ya kuongeza muda yamekataliwa na vibali vyake kufutwa kutokana na sababu ya kumalizika kwa makubaliano ya muda wa ajira ya wageni katika nafasi zilizoombewa.

- Ukaguzi wa miradi 72 kwa nia ya kuona inavyofuata masharti ya uwekezaji umefanywa. Aidha, miradi yote mipya imefanyiwa ukaguzi wa maeneo yaliyolengwa kabla ya kuidhinishwa ili kubaini iwapo kuna mzozo wa ardhi au la. Suala hilo limepelekea kupata fursa ya kuwaongoza wawekezaji kufuata Sheria zinazohusiana na mazingira, matumizi ya ardhi, na mahusiano na jamii.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Mamlaka imejiwekea malengo yafuatayo:-

- Kuendeleza kutangaza fursa na kushajiisha wafanyabiashara wa ndani kuwekeza katika sekta ya uzalishaji bidhaa za viwanda kwa kutumia malighafi za kilimo zinazopatikana Zanzibar na Tanzania.

- Kukamilisha utafiti na kutayarisha maelezo ya uwezekano wa uwekezaji katika Uvuvi wa bahari kuu, na pia kuwekeza katika kiwanda cha usindikaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

- Kufanya mchakato wa mapendekezo ya miradi na kuidhinisha miradi mipya 60.

- Kufanya tafiti zinazohusiana na maeneo ya uwekezaji, aina mpya ya fursa za uwekezaji kwa sekta zote, pamoja na fursa za kuendeleza vitega uchumi kwa wananchi wazalendo kwa kutafuta vianzio vya upatikanaji wa mitaji na misaada mengine na hatimae kuwasaidia katika taratibu za kufanya ubia pale wanapohitaji.

- Kushajiisha wawekezaji binafsi ili kuwekeza katika kuendeleza miundo mbinu ya barabara, maji, umeme na majengo katika maeneo huru na bandari huru, ili iwe katika hali ya kuridhisha kwa ajili ya ufanisi wa miradi iliyopo pamoja na kuvutia miradi mipya katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi inaombewa ruzuku ya Tzs. 300,000,000/= kutoka Serikalini.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, pamoja na ufanisi uliopatikana katika utekelezaji wa kazi tulizojipangia, wizara ilikabiliwa na changamoto za; upungufu wa fedha, vyombo vya usafiri kama gari, vespa/pikipiki. na upungufu wa wataalam katika fani za Takwimu, Manunuzi, Uchambuzi wa Sera na Utawala.

Mhe. Spika, sekta ya utalii ilikumbana na changamoto za Uhafifu wa huduma zisizowaridhisha watalii/wageni hasa katika milango ya kuingilia na kutokea nchini (Uwanja wa Ndege na Bandarini).

- Mazingira yasiyoridhisha ya uchafu katika Mji Mkongwe wa Zanzibar pamoja na kero za mapapasi wanaowasumbua wageni.

- Vikwazo vya njiani na usumbufu wa Askari Polisi kudai hongo kwa magari ya kitalii.

- Ufinyu wa bajeti ya kuitanga Zanzibar katika masoko ya kitalii yenye ushindani mkubwa.

- Uhaba wa madarasa na afisi za walimu na kupelekea chuo cha Maendeleo ya Utalii kushindwa kuhimili mahitaji ya wanaotaka kujiendeleza katika fani zinazotolewa hapo chuoni.

- Kutolipwa ada kwa wakati.

- Kubadilika kwa kasi mahitaji ya soko na vifaa vya kutolea huduma ikiwa ni upungufu wa vitabu vya kiada katika maktaba ya Chuo, na mifumo ya kompyuta ya kufundishia ikilinganishwa na uwezo wa chuo wa kufanya mabadiliko katika mitaala, na upatikanaji wa vifaa vinavyoendana na teknologia ya sasa hasa ikizingatiwa uwezo wa kifedha wa chuo katika kugharamia shughuli zake na kuwaendeleza walimu.

Mhe. Spika, pamoja na mchango wa sekta ya viwanda uliotajwa, changamoto zilizopo zinajumuisha na gharama kubwa ya vipuri, mitambo, malighafi, kupanda kwa gharama za uzalishaji, masharti magumu ya mikopo kwa taasisi za fedha,ushindani wa biashara kwa bidhaa za viwandani pamoja na uhaba wa wataalamu katika fani ya uhandisi.

TAARIFA ZA JUMUIYA ZA MAENDELEO ZA KIKANDA:

A: **Jumuiya ya Afrika Mashariki** (***East African Community***):

Mhe. Spika, naomba nieleze kwa muhtasari juu ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa makubaliano ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, baada ya kukamilika kwa Itifaki ya Umoja wa Forodha miaka mitano (5) iliyopita ulianza mchakato wa Itifaki ya uanzishwaji wa Soko la Pamoja, ambayo imekamilika na kutiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama mwezi Novemba 2009. Itifaki hiyo inatarijiwa kuanza kutumika mwezi Julai 2010 baada ya kuridhiwa na Mabunge ya nchi wanachama. Katika Itifaki ya Soko la Pamoja maeneo yaliyojadiliwa ni pamoja na uhuru wa kuingia na kutoka nchi moja kwenda nyengine kwa bidhaa, watu, wafanyakazi, biashara ya huduma na mitaji.

Katika majadiliano hayo imekubaliwa kuwa masuala ya kumiliki ardhi na majengo pamoja na ukaazi wa kudumu yatasimamiwa na sheria husika za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, imekubaliwa kuwa hati ya kusafiria (*passport*) ndiyo itakayotumika kwa ajili ya kusafiri kutoka nchi moja kwenda nchi nyengine. Hata hivyo, imekubaliwa kuwa nchi zitakazokubaliana kutumia vitambulisho kama hati ya kusafiria baina ya nchi hizo zinaweza kuendelea na utaratibu huo. Kwa upande wa Tanzania bado hati ya kusafiria (*passport*) ndiyo itakayotumika kama hati sahihi ya kusafiria ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, Majadiliano ya Uanzishwaji wa Mashirikiano ya Ubia ya Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya

(*Economic Partnership Agreement – EAC –EC EPA*) yanaendelea. Majadiliano hayo yanaongozwa na vifungu vya 3 (2) na 37 vya mkataba wa makubaliano ya Ushirikiano wa Kiuchumi (*Framework of Economic Partnership Agreement – FEPA*). Maeneo yanayoendelea kujadiliwa kwa ajili ya mashirikiano ni Upatikanaji wa Masoko (Market Access), na mashirikiano ya maendeleo na Kiuchumi (Develepment and Economic Cooperation).

B: **Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*):**

Mhe. Spika, Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) zina lengo la kuanzisha Eneo huru la Biashara 2008, Umoja wa Forodha 2010, Soko la pamoja 2015, Umoja wa fedha 2016 na Sarafu ya aina moja ifikapo mwaka 2018 katika nchi wanachama wa Jumuiya hiyo.

Mhe. Spika, eneo huru la biashara katika nchi za *SADC* limeshaanza kutumika ambapo wazalishaji na watumiaji kutoka nchi wanachama hawatolipa ushuru wa Forodha kwa bidhaa zinazozalishwa katika Jumuiya hiyo baada ya kukidhi mahitaji, yakiwemo ya uhalisia wa bidhaa *(Rules of Origin).*

Mhe. Spika, nchi wanachama wa *SADC* zimo katika mchakato wa kuanzisha Itifaki ya Umoja wa Forodha ambapo bado majadiliano yake yanaendelea. Ili kufanikisha azma hiyo Jumuiya inazingatia pamoja na mambo mengine masuala ya viwango vya ushuru wa Pamoja **(***Common External Tariff),* mpangilio wa kisheria na kitaasisi (*Legal and Institutional Arrangements*), ukusanyaji na ugawanaji wa mapato (*Revenue collection, sharing and Distribution Mechanism Including a Compensatory funds*) na ulingano wa sera (*Policy Harmonization*).

Mhe. Spika, kukamilika kwa majadiliano ya Jumuiya hizi yanatarajiwa kuiwezesha nchi yetu kuuza na kununua bidhaa nyingi kutoka nchi wanachama wa Jumuiya hizo. Hivyo naomba kutoa wito kwa wajasiriamali, wazalishaji pamoja na wawekezaji kuendelea na juhudi za kuzalisha kwa wingi zaidi bidhaa kwa ajili ya masoko ya Afrika ya Mashariki, Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Ulaya, kwani tusipozalisha na kuuza, siku zote tutabakia kuwa soko la bidhaa kutoka katika Jumuiya hizo na kuathiri maendeleo ya biashara na Uchumi kwa Jumla kutokana na kuwa na nakisi katika urari wa biashara na nchi hizo.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI:

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2009/2010 na matarajio kwa mwaka

2010/2011 naomba sasa uniruhusu nitoe muhtasari wa mapato na matumizi kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kupitia Idara ya Biashara na Kamisheni ya Utalii ilikadiria kukusanya mapato ya Tzs. 839.8 milioni (Tzs. 26.0 milioni – Idara ya Biashara na Tzs. 813.8 milioni – Kamisheni ya Utalii) kutokana na vianzio vyake vya mapato. Hadi kufikia Mwezi Machi 2010 Wizara ilikusanya Tzs. 625.75 milion. (Tzs. 16.0 milioni – Idara ya Biashara na Tzs. 609.75 – Kamisheni ya Utalii) sawa na asilimia sabiini na tano (75%)

Mhe. Spika, jumla ya Tzs 2,357 milioni ziliidhinishwa na Baraza lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo fungu 21 (Wizara) ni Tzs. 1,661 milioni na Tzs 696 milioni kwa fungu 31 (Kamisheni ya Utalii). Hadi kufikia mwezi Machi 2010, fedha zilizopatikana ni Tzs. 1,649.4 milioni sawa na asilimia sabini (70%) ya makisio. Kati ya fedha hizo Tzs. 1,180.3 milioni kwa fungu 21 na Tzs. 469.11 milioni kwa fungu 31.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara hii pia iliidhinishiwa jumla ya Tzs. 1,941.5 milioni kwa kazi za maendeleo kwa ajili ya miradi inayosimamiwa na Wizara. Hadi kufikia Machi, 2010 fedha iliyopatikana ni Tzs. 950 milioni sawa na asilimia arobaini na tisa (49%) ya makadirio.

SHUKURANI:

Mhe. Spika, mafanikio tuliyopata ni matunda ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na Wajumbe mmoja mmoja kwa ushauri na changamoto mlizotupa katika kipindi cha utekelezaji. Ushauri wenu ulituonesha njia pale ambapo sisi peke yetu tulikwama.

Mhe. Spika, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ilipata michango kutoka kwa Taasisi, Jumuiya za hapa nchini, Kimataifa na nchi rafiki. Tunaomba kutoa shukurani zetu za dhati kwa *ZNCCIA*, *ZATO*, *ZATI*, *TNBC*, taasisi ya *"TRADECOM", EU, UNIDO, UNDP, World Bank*, *Common Wealth*, *WTO na ILO*. Pia tunazishukuru nchi marafiki zikiwemo China, Uingereza, Nchi za Nordic, Qatar, Urusi, Italy, Dubai, kwa misaada na mashirikiano waliyotoa kwa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Idara, na Wakuu wa Taasisi za Wizara kwa michango yao katika kufanikisha hotuba hii. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wa taasisi zote za Wizara, kwanza kwa mashirikiano waliyotoa, na pili kwa kutimiza wajibu wao vyema katika utekelezaji wa kazi zetu, na hivyo kunipa nguvu ya kusimama hapa na kuwasilisha hotuba hii ya bajeti. Pia naomba nimshukuru Mkurugenzi na Wafanyakazi wa Idara ya Upigaji Chapa kwa kazi nzuri ya uchapaji wa hotuba hii.

Mhe. Spika, utekelezaji wa kazi za wizara zilichangiwa na wengi. Naomba kupitia Baraza lako Tukufu nizishukuru kwa dhati taasisi za kiserikali, makampuni binafsi, Jumuiya za Kibiashara, wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano ya namna tofauti waliyotoa ili kufanikisha malengo ya wizara.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, ili Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji iweze kutekeleza malengo yake niliyoyataja kwa mwaka 2010/2011 nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waitafakari, waichangie hotuba hii na baadae watoe miongozo itakayotuwezesha kutekeleza kwa ufanisi mkubwa malengo ya Wizara kama tulivyoainisha. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Tzs 2,676 milioni kwa kazi za kawaida za Wizara. Kati ya fedha hizo Tzs 1,939 milioni ni za fungu 21 na Tzs 737 milioni kwa fungu 31. Kwa upande wa fedha za fungu 21, Tzs 300 milioni ni ruzuku kwa Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*), Tzs 400 milioni ni ruzuku kwa Chuo cha Maendeleo ya Hoteli na Utalii na Tzs 200 milioni ni ruzuku kwa Baraza la Biashara. Pia naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tzs 2,549.55 milioni kwa kazi za maendeleo, na kukusanya jumla ya Tzs 829,325,000 (Tzs 805,800,000 Kamisheni ya Utalii na Tzs 23,525,000 - Idara ya Biashara).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kama ni mashindano Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji ameshinda kwa kutumia dakika ishirini kuliko mawaziri wengine wote ambao wamewahi kutoa hotuba zao. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) Mhe. Spika, kwanza naomba kutumia nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia sote tukiwa hai na wazima kwa afya siku hii ya leo. Aidha, nitumie nafasi hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe maoni kwa niaba ya

Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa uwezo wake mkubwa wa kiutendaji kama ambavyo ametuwasilishia hotuba yake hii leo. Pongezi hizi na shukurani ziwaendee pia watendaji wake wote wanaongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Pemba, Wakuu wa Vitengo mbali mbali vya wizara tunawapongeza kwa juhudi zao wanazozitumia katika kuhakikisha kuwa majukumu ya kazi walizopangiwa zinakwenda vyema. Ingawa kumekuwa na changamoto nyingi zinazowakabili katika utendaji wao wa kazi ila juhudi zao zimekuwa zikionekana.

Mhe. Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango mawazo na hata ushauri pale ilipobidi wakati kamati ilipokuwa ikifanya kazi zake za kawaida kwenye taasisi mbali mbali za mawizara. Mashirikiano makubwa waliyoonesha pamoja na juhudi zao kwa hakika ni hizo zimepelekea kufikiwa kwa mafanikio haya. Mpaka hii leo tukiwa tunahitimisha awamu ya pili ya muda wa kamati vile vile na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti.
2. Mhe. Ali Abdalla Ali	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asaa Othman Hamad	Mjumbe
4. Mhe. Ashura Abedi Faraji	Mjumbe
5. Mhe. Said Khelef Ali	Mjumbe
6. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	Mjumbe
7. Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	Mjumbe
8. Mhe. Juma Duni Haji	Mjumbe
9. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
10. Mhe. Rashid Seif Suleiman	Mjumbe
11. Ndg. Amour Moh'd Amour	Katibu
12. Ndg. Mariam Hussein Rajab	Katibu

Mhe. Spika, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ina majukumu makubwa ambayo yanagusa mwenendo mzima wa uchumi. Mhe. Spika, kwa mazingira ya nchi yetu ambayo kwa maumbile yake ni visiwa basi ili tuwe na uchumi imara suala la kuimarisha Sekta ya Uwekezaji, Utalii na Biashara ni muhimu sana. Hilo ni jukumu kubwa tulilolikabidhi wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba uniruhusu nitoe maoni ya kamati kupitia sekta hizo kama ifuatavyo:-

Baraza la Biashara la Zanzibar

Mhe. Spika, Baraza la Biashara la Zanzibar ni chombo muhimu sana ambacho kwa njia moja ama nyengine kimesaidia kutatua kero nyingi za wafanyabiashara wetu. Kwa mfano, wafanyabiashara walio wengi wamekuwa wakiamini kuwa utonzwaji wa kodi kubwa unawanyonya sana, hivyo, kuchelea kupata faida. Kupitia Baraza la Biashara wafanyabiashara hukutana na kujadili masuala mbali mbali yanayowakabili ili mustakbali wa malengo yao wende sawa. Tunaamini kuwa kuwepo kwa utaratibu huu wa kuwakutanisha wafanyabiashara uendelee ili kuwasaidia wafanyabiashara wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia kuwa katika mwaka wa fedha 2010-2011 wizara imejipangia kuzindua Mabaraza ya Biashara ya Mkoa yaani *(Regional Business Council*) tunaamini kuwa kupitia Mabaraza haya ya Mkoa yatasaidia kuwahamasisha hata wale wafanyabiashara ndogo ndogo.

Mhe. Spika, tukiwa tunaelekea katika itifaki ya uanzishwaji wa soko la pamoja la Afrika Mashariki ni vyema wafanyabiashara wetu wakafahamu kinagaubaga kuwa jambo hili ili lisijelikaleta utata kwa siku za usoni kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewasaidia wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kutokuathirika na taratibu hizo mpya.

Sekta ya Utalii

Mhe. Spika, sekta hii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Shirika la Utalii pamoja na Hoteli ya Bwawani. Sekta ya Utalii Zanzibar kwa muda mrefu sasa ukiacha suala zima la kusaidia ongezeko la mapato la taifa letu imekuwa pia ikitoa ajira mbali mbali kwa wananchi. Lakini kumekuwa na malalamiko mengi ya wazalendo juu ya ajira kwenye sehemu za mahoteli. Wazalendo wamekuwa wakilalamika kukosa ajira katika mahoteli na hata wakiajiriwa basi ni nafasi za watu wa chini kama vile wafyagiaji au watunza bustani.

Mhe. Spika, nchi yetu imejaaliwa kuwa na vivutio mbali mbali ambapo kupitia watalii pamoja na wageni mbali mbali tumekuwa tukipata mapato mengi kupitia vyanzo hivyo. Haina budi sasa wizara kwa kushirikiana na taasisi husika kuweka taratibu ambazo zitasaidia kutuongezea mapato zaidi. Mhe. Spika, tunamaanisha kwamba pamoja na kuwa na vivutio asilia ni muda muafaka sasa kuwa na vivutio *artificial*, vivutio hivi ukiacha suala zima la

uongezaji wa mapato bali huchangia katika kuweka miji yetu safi. Mfano, mzuri ni eneo la Forodhani ambapo mandhari sasa imekuwa ya kuvutia zaidi.

Mhe. Spika, eneo kama lile la bustani ya Jamhuri ambayo ni vyema likaimarishwa zaidi pamoja na eneo la wazi lililopo Michenzani karibu na Kisonge ni maeneo ambayo yakitiliwa mkazo zaidi yatasaidia kubadilisha mandhari ya mji wetu.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kwamba biashara ni matangazo hatuna budi kujitangaza zaidi ili tuwe na mustakbal mzuri wa maisha ya wananchi wetu. Kwa kuwa jitihada kubwa zimechukuliwa katika kuitangaza Zanzibar ndani ya Tanzania na hata nje ya nchi kupitia maonesho mbali mbali kamati inaiomba serikali kupanua wigo zaidi hususan katika masoko mapya kupitia maoneshe mbali mbali ya kitaliii na mikutano ya kimataifa.

Mhe. Spika, Zanzibar imekuwa ikifahamika kwa sifa zake za ukarimu, busara, utulivu na amani ina amini kuwa sifa hizi ndizo zinazowavutia zaidi watalii na wageni wengine kuja nchi kwetu. Suala la ulinzi na usalama wa watalii pamoja na mali zao lazima liangaliwe kwa umakini ili kuhakikisha wale wabaya wachache hawatuharibii sifa hiyo iliyodumu na watalii hawapati usumbufu.

Mhe. Spika, michezo imekuwa ikihamasisha utamaduni wetu wa kizanzibari na hivyo kuwa kivutio hasa kwa watalii wanaokuja nchini. Michezo ya utamaduni ikiwemo Tamasha la Nchi za Majahazi, Tamasha la Mzanzibari, Mwaka Kogwa au Sauti za Busara imekuwa kivutio kikubwa cha kuimarisha utamaduni wetu na pia kuwakutanisha watu wa rika au sehemu mbali mbali. Aidha, si vibaya tukarudisha yale mashindano ya '*marathon'* na '*trithon'* ambayo yameitangaza sana Zanzibar kiutalii.

Chuo cha Utalii Maruhubi

Mhe. Spika, elimu ndiyo dira ya maendeleo na elimu iliyo bora ni mwelekeo mzuri wa maisha. Kwa muda mrefu sasa Chuo cha Utalii kimekuwa kikikabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo zilipelekea kuzorotesha huduma za elimu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua chuo iliyofikia hivi sasa. Chuo kipo katika mchakato wa kutambulika zaidi. Hivyo tunakiomba chuo kiendelee na taratibu zilizobakia ili wakufunzi wapate hadhi ya kutambulika kitaifa na kimataifa.

Hakika pia, mazingira mazuri huchangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa elimu bora. Uhaba wa madarasa, uchakavu wa majengo pamoja na ufinyu wa vitendea kazi unatia dosari sifa ya chuo. Mhe. Spika, umefika wakati sasa tutambue nini tunafanya na nini tunatekeleza. Kwa upande wa Tanzania visiwani ni Chuo cha Utalii Maruhubi pekee ambacho kinatoa mitaala tofauti

katika mambo ya utalii. Kwanini chuo hichi tusikipe kipaumbele ili kisaidie kutoa wakufunzi walio bora ambao watatambulika kitaifa na kimataifa. Tunaiomba serikali itambue umuhimu wa chuo hichi.

Mhe. Spika, ijapokuwa tunafahamu ya kwamba, Benki ya Maendeleo ya Afrika imeonyesha nia ya kukijenga upya chuo hiki kuanzia mwaka 2011/2012. Kwa hali hiyo, ni vyema nasi tukafanyia matengenezo japo yale madogo madogo.

Hoteli ya Bwawani

Mhe. Spika, serikali kuwa na vitega uchumi vyake ni jambo la busara sana, hususan kwa nchi changa na zile zinazoendelea kama hii yetu. Hoteli ya Bwawani kimtazamo imekosa hadhi ya hoteli, hivyo kupoteza mapato mengi ambayo yangepatikana kama hoteli ingekuwa katika hali nzuri. Mhe. Spika, tunaamini kuwa maendeleo hayaji kwa siku moja, ila tukumbuke kuwa haba na haba hujaza kibaba. Ukarabati wa hoteli unahitajika ili kukidhi haja za wadau mbali mbali. Kama tumeweza kuanza na ukarabati wa vyumba sita mwaka wa fedha 2009/2010 kwa nini tushindwe kuendeleza lile tulilolianza kwa siku za usoni.

Kwa kuwa tunaamini kwamba tukiwezeshwa tunaweza, kamati inaiomba serikali iidhinishe matumizi ya hoteli ya kiasi cha Shilingi 717,450 milioni ya mapato ili nasi tuwe tuna hoteli yetu yenye hadhi inayostahili.

1. **Sekta ya Biashara**

Mhe. Spika, Sekta hii ya Biashara inajumuisha Idara ya Biashara, Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) na Shirika la Biashara la Magari (*MTC*)

- **Idara ya Biashara**

Mhe. Spika, suala la kuwa na uwanja wa maonyesho ya biashara ya kimataifa hapa Zanzibar ni jambo muhimu sana. Serikali itambue haja ya kuwa na uwanja wa maonyesho ya biashara na ilichukulie jambo hili kwa umakini zaidi. Mhe. Waziri amezungumzia maeneo huru ya kiuchumi yaliyopo kijiji cha Ndambaani, Shehia ya Dimani yaliyotengwa kwa ajili ya maonyesho. Ni vyema sasa tukalitilia mkazo suala hili ili yasije yakatokea kama yale yaliotokea kwa maeneo ya Mwanakwerekwe na Tunguu.

Mhe. Spika, kamati ilipata muda wa kwenda kuangalia maeneo huru haya na kuridhishwa na hali yake. Hivyo basi, tunaiomba serikali iharakishe suala hili kwani tukiwa na uwanja wa maonyesho tutatumia fursa hiyo kujitangaza zaidi kibiashara na hata kukua kiuchumi.

Mhe. Spika, ni vyema tukaangalia zaidi sheria zetu za biashara ili tutakapokuwa tayari kufanya maonyesho hayo tuweze kukabiliana na ushindani uliopo wa biashara. Mhe. Waziri ametuhakikishia kuwa, rasimu ya awali ya sheria ya viwango kwa ajili ya kuwa na ubora na udhibiti wa viwango vya bidhaa imeshatayarishwa. Tunaamini sheria hiyo italeta mabadiliko makubwa katika ulimwengu huu wa bidhaa.

- ***ZSTC***

Mhe. Spika, utaratibu wa kujitangaza kibiashara huinua chachu ya maendeleo kwa sehemu ya biashara kama ilivyo. Kwa Kiwanda cha Makonyo Pemba matangazo huhitajika ili kusaidia kukitangaza kiwanda pamoja na kuwashajihisha watu mbali mbali kutumia bidhaa zinazotengenezwa kiwandani hapo. Mhe. Spika kuna umuhimu mkubwa kwa kiwanda kushajiisha matumizi ya bidhaa wanazozizalisha ndani na hata nje ya nchi ili kuwa na soko la uhakika.

Pamoja na juhudi zinazofanywa na Shirika la Biashara (*ZSTC*) Dar es salaam, bado sehemu hii ya shirika inakabiliwa na changamoto ya jengo wanalolitumia. Shirika limekuwa likitumia mapato mengi wanayoyapata katika kulipia kodi ya jengo. Utumiaji wa jengo hilo umekuwa ukigharimu kiasi cha shilingi milioni 33 kwa mwaka. Kamati kupitia hotuba zake mbali mbali ilishauri na inaendelea kushauri ufumbuzi wa suala hili upatikane ili shirika liendelee kujiendesha kwa faida zaidi.

2. Sekta ya Viwanda

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Japokuwa Sekta ya Viwanda Zanzibar haiwezi kuwa na viwanda vikubwa kutokana na kutokuwa na maeneo makubwa kama yale ya wenzetu wa Tanzania Bara, kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda hivyo. Hata hivyo, kuna haja ya kuendelea kuwa na viwanda vidogo vidogo pamoja na vile vya kati.

Viwanda hivi vina faida kubwa sana kwa nchi kama vile kutoa ajira kwa wananchi hivyo husaidia kupunguza umaskini, lakini pia huleta na unafuu wa bei za bidhaa zinazozalishwa.

Mhe. Spika, kamati inaamini kuwa tukijipanga tunaweza kufanikisha na kuisaidia sekta hii kuwa moja ya sekta ambazo zitakuwa zinasaidia ongezeko la pato la taifa. Mazingira mazuri ya uwekezaji yanahitajika hususan kwenye sekta hii ili wawekezaji waondokane na dhana ya kuwa Zanzibar ni nchi yenye uchumi wa kisiwa.

3. Sekta ya Uwekezaji

Mhe. Spika, Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) ni chombo muhimu sana katika kuleta maendeleo ikiwa kitatumiwa vizuri. Utekelezaji wa chombo hiki una changamoto nyingi ambapo kwa njia moja ama nyengine umepelekea kusua sua kwa utekelezaji wa majukumu yake. Mhe. Spika, lengo kuu la *ZIPA* ni kuifikisha nchi yetu katika mustakabali mzuri wa dhana ya kituo kimoja cha Uwekezaji yaani *"one stop center"*. Tutumie muda mfupi katika kukamilisha taratibu za uekezaji lakini maamuzi hayo yafanywe kwa busara na umakini, lakini endapo vyombo vyetu vya maamuzi havitakuwa na wajumbe wenye kauli ya mwisho basi migongano haitasaidia kufikiwa kwa lengo hilo.

Aidha, tunapoamua kuteua maeneo huru basi tuwe makini na maamuzi hayo. Haipendezi hata kidogo kufanya maamuzi hayo lakini tukashindwa kuyaendeleza. Hivi leo maeneo ya Micheweni hakuna lolote lililotekelezwa. Inaonesha serikali haijipangi kujenga miundo mbinu ambayo pengine tungeyagawa malengo hayo kwa awamu basi leo Micheweni kungekuwa na sura ya kivutio na waekezaji wangeamua kuwekeza. Lakini kwa mazingira yaliyokuwepo katu tusitegemee lolote pale.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema sasa ufike wakati tuwe tunazungumzia ufumbuzi wa matatizo kuliko kuendelea kujadili changamoto mbalimbali zinazozikabili taasisi zetu. Mhe. Spika, tumekuwa tukitolea mfano kwa nchi ya kama vile Dubai jinsi ilivyoweza kufanikiwa baada ya kufungua milango ya uwekezaji. Mara nyingi nimekuwa nikisisitiza kuwa kwanini wao waweze na sisi tushindwe kufikia hayo malengo au hata nusu yake.

Mhe. Spika, tunafahamu kuwa, Mamlaka ya Vitega Uchumi ina jukumu kubwa la kuitangaza nchi yetu katika suala zima la uwekezaji. Aidha, mamlaka inajitahidi sana katika kutekeleza majukumu yake na kama tulivyozoeya kusikia kuwa uwekezaji kwenye Sekta ya Utalii pekee. Ni vyema sasa, mamlaka ishajihishe uwekezaji katika maeneo mengine kama vile uwekezaji katika ujenzi wa nyumba, kilimo na katika uvuvi.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya kamati, niwaombe sasa wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato yatakayokusanywa kwa mwaka 2010/2011 ya jumla ya Shilingi 2,352,000,000/-, wakati Shilingi 1,939,000,000/= kwa ajli ya matumizi ya kazi za kawaida za wizara na Shilingi 1,790,000,000/= kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi tunaunga mkono hoja hiyo na vile vile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni nasema pia,

naunga mkono hoja. Pia nawataka wajumbe wenzangu wamuunge mkono Mhe. Waziri ili wizara itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza naomba kuwasilisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin) (Waziri Kivuli, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji): Mhe. Spika, kwa niaba ya waziri kivuli naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Hotuba ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 kama yalivyotolewa na Mhe. Waziri Kivuli Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin.

Mhe. Spika, kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu, nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kwa kuendelea kunipa mimi pamoja na nyinyi neema zake za uhai na uzima na kuniwezesha leo hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kutoa maoni ya kambi mahiri ya upinzani juu ya hotuba iliopo mbele yetu, ikiwa ni mara ya mwisho kwa awamu hii ya sita ya uongozi mahiri wa Dr. Amani Abeid Karume. Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu ampe Dr. Amani mapumziko ya amani, utulivu na salama pamoja na maisha marefu.

Mhe. Spika, pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa maoni machache ya Kambi ya Upinzani juu ya bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Mwenyezi Mungu aendelee kukupa busara na hekma na akuvushe salama katika mchakato ujao ili uweze kuliongoza Baraza hili zaidi. Amin.

Mhe. Spika, sina budi pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji (Mhe. Samia Suluhu Hassan) kwa mashirikiano makubwa alionipa wakati wote nikiwa waziri kivuli wa wizara yake, yeye pamoja na watendaji wake, nasema ahsante sana. Ninamuomba Mwenyezi Mungu amvuushe afike pale alipokusudia ili atumie nguvu zake na ujuzi wake kulisaidia taifa, Amin.

Mhe. Spika, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ina matabaka matatu ambayo kila moja lina umuhimu wa pekee katika kujenga na kukuza uchumi. Mhe. Spika, moja kati ya matabaka haya au yote kwa pamoja yakiterereka huleta athari kubwa kwa uchumi wa nchi husika pamoja na wananchi wake.

Katika muhula huu tunaokwenda nao dunia imekubwa na mtikisiko wa kiuchumi ambao kwa vyovyote vile umeathiri matabaka ya wizara kama hii ulimwenguni kote. Kwa vile Zanzibar ni sehemu ya ulimwengu haiwezi kuepuka na hilo.

Tukiitazama Wizara, tutaona imeundwa na idara na taasisi mbali mbali ili kuleta ufanisi wa utendaji. Mhe. Spika, idara na taasisi za Wizara hii ni kama ifuatavyo:-

- Idara ya Mipango na Sera
- Idara ya Biashara
- Idara ya Vwanda na
- Idara ya Uwekezaji na Vitega Uchumi.

Mhe. Spika, taasisi ambazo ziko chini ya wizara hii ni:-

- Shirika la Taifa la Biashara *ZSTC*
- Shirika la Magari
- Shirika la Utalii
- Kamisheni ya Utalii
- Hoteli ya Bwawani

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, jukumu kubwa la idara hii ni kuandaa na kusimamia mipango na sera za wizara pamoja na shughuli zote za utawala. Kwa upande mwengine ni kuratibu mipango ya idara na taasisi nyengine na kuwa kiungo muhimu kati ya wizara, idara na taasisi zilizo chini ya wizara hii.

Mhe. Spika, idara, katika mwaka uliopita wa fedha ilijipangia malengo kadhaa kuyatekeleza. Kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, imefanikiwa kutekeleza malengo yote iliyojiwekea, isipokuwa lengo moja la kupitia ripoti ya *TCFB* liliondolewa. Ni sababu zipi zilizopelekea kuondolewa lengo hilo, kwani kwa maoni yangu suala hilo lilikuwa na umuhimu wa pekee wa kuweza kutujuvya ni sababu zipi zinazopelekea biashara ya Zanzibar kushuka. Jambo ambalo lingetuwezesha kujua tatizo na tukaweza kuchukua hatua muafaka kukabiliana na tatizo lenyewe na tukaweza kuandaa mikakati na mipango madhubuti ya kuliondoa ili kunyanyua biashara yetu.

Mhe. Spika, ukiangalia maelezo ya Mhe. Waziri juu wa utekelezaji wa malengo ya mwaka uliopita na malengo yanayokusudiwa kutekelezwa na idara hii, kuna kujirudia rudia. Kwani tumeelezwa kwamba sheria namba 2 na namba 4 mapitio ya rasimu zake umekamilika, sasa iweje tuelezwe tena kwamba malengo ya mwaka huu wa fedha pia yamepangwa kutekelezwa tena.

Utaratibu wa uimarishaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni muhimu sana hasa kwa vile tumeamua kuingia kwenye biashara ya utalii. Masikitiko yangu ni kwamba bado hatujakuwa makini juu ya suala hili, kwani pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na menejimenti ya chuo bado serikali haijatoa msukumo unaostahiki na kuridhisha kukiimarisha chuo hicho. Hivi karibuni

chuo kimepokea msaada wa vifaa mbali mbali vya jikoni, lakini la kusikitisha vifaa hivyo hata pa kuwekwa hapana. Nimuulize Mhe. Waziri ni lini upanuzi wa chuo kimajengo utaanza ili kupata nafasi ya kutosha ya kufundishia na kuweka vifaa.

Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Rais kutoa agizo la kutengenezwa barabara iendayo chuoni, hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Mhe. Spika, chuo kinawapatia mafunzo ya juu waalimu na wafanyakazi wengine. Ni muhimu maslahi yao yakaangaliwa ili baadae wasije kuondoka kwa kufata maslahi mazuri nje.

IDARA YA BIASHARA

Mhe. Spika, majukumu makubwa ya idara hii ni pamoja na kuangalia hali ya chakula, kusimamia vipimo na mezani, kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji, ukaguzi wa maduka na maghala, ufuatiliaji wa masoko, kuandaa maonyesho ya biashara, kutoa taarifa za biashara na kushiriki katika majadiliano ya kikanda na kimataifa yahusianayo na biashara.

Majukumu yanayosimamiwa na idara hii ni mazito na muhimu sana, ambayo utekelezaji wake utaweka mazingira mazuri ya biashara. Ili ufanisi wa utendaji upatikane na kuonekana, ni budi watendaji wapatiwe nyenzo na vifaa vya kutendea kazi na utaalamu wa kazi yao.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba wafanyakazi wa kitengo cha mezani, vipimo na kumlinda mtumiaji hasa Pemba hakuna usafiri wa kufuatilia kazi zao, kwani kazi zao si za afisini moja kwa moja tu, bali ni za nje ya afisi. Wafanyakazi hao wanategemea gari za kuazima na gari ya Afisa Mdhamini wao. Hivyo katika hali hii tija, ufanisi na lile lengo la kumlinda mtumiaji litapatikana?.

Katika maelezo ya Bajeti ya Mhe. Waziri nimefarijika sana kwa kuona kwamba miongoni mwa mambo mengi ambayo nimekuwa nikimshauri, Mhe. Waziri ameanza kuonesha dalili ya kuyachukulia hatua. Moja ni lile la kuanzisha sheria ya viwango kwa ajili ya kuwa na ubora na udhibiti wa viwango vya bidhaa hapa nchini Zanzibar, kwa hilo nampongeza sana. Pili ni lile la kuanzisha Kiwanja cha Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Zanzibar.

Mhe. Spika, ninamuomba sana na kwa heshima zote Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi aupe mradi huu umuhimu unaostahiki na kuupatia fedha haraka, kwani mafanikio ya mradi huu utaiongezea mapato serikali.

Mhe. Spika, bado hali ya biashara kati ya Zanzibar na nchi za nje pamoja na ile ya Zanzibar na Tanzania Bara hairidhishi, kwani bado nakisi katika urari wa biashara ni mkubwa. Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya kuongeza uzalishaji katika sekta mbali mbali kwa matumizi ya ndani na usafirishaji.

Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa bidhaa zinazozalishwa kuongezwa viwango na ubora ili ziweze kukabili ushindani katika masoko ya ndani na ya nje. Ule mradi unaojihusisha na hilo ni budi usimamiwe ipasavyo na kupewa uwezo.

Tatizo jengine ambalo linazikabili bidhaa zetu ni namna ya ufungaji na zana za kufungia bidhaa hizo, yaani "*Packing and Packing Materials*". Kwa hivyo, na eneo hili nalo linafaa kusimamiwa na kushughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Waziri ametueleza kwamba lengo la ukusanyaji wa mapato halikukamilika kutokana na sababu alizozieleza ambazo mimi kwa mawazo yangu naziona si za msingi. Kwani utaalamu ni juu yake kuusimamia na kuona kwamba wafanyakazi wa kitengo hicho wanapatiwa utaalamu unaostahiki ili waweze kumudu majukumu yao. Kwa muda wa miaka mitano (5) tokea Mhe. Waziri kuwepo wizarani, ingetosha kukipatia kitengo taaluma muwafaka kwa maslahi ya nchi.

IDARA YA VIWANDA

Mhe. Spika, ni jambo lisilo na ubishani kwamba Sekta ya Viwanda ni muhimu sana katika kukuza pato la taifa na kupunguza umasikini. Sekta hii hapa kwetu bado inasuwasuwa na mchango wake katika pato la taifa bado ni mdogo sana. Zanzibar kama kisiwa uwezo wake wa kuanzisha viwanda vikubwa ni mdogo sana. Kwa hiyo, kuna haja na umuhimu wa pekee kuangalia sera ya viwanda vidogo vidogo na kuirekebisha ili iweze kutoa muelekeo na msukumo wa uanzishwaji wa viwanda hivyo. Ziko nchi nyingi duniani zimefanikiwa na kupiga hatua kubwa za uchumi wao kutokana na uanzishwaji na uimarishaji wa viwanda hivyo. Mfano, Malaysia na Singapore.

IDA RA YA UWEKEZAJI NA VITEGA UCHUMI

Mhe.Spika, mamlaka hii ina umuhimu wa pekee katika kuvutia uwekezaji nchini. Uwekezaji huo ima uwe wa wazalendo au wageni kutoka nje. Jukumu la kuitangaza Zanzibar kwa wawekezaji ni lenye gharama na linahitaji utaalamu. Jambo la kusikitisha ni kwamba, Mamlaka haiwezeshwi ipasavyo kufanya shughuli zake. Mhe Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 mamlaka imeandaa na kutekeleza makongamano mangapi ya kushajiisha wawekezaji (*Investment Forum*) ndani na nje ya nchi?

Mhe. Spika, njia zinazotumiwa na Mamlaka ya kusambaza vijarida, makabrasha na kalenda hazina mafanikio makubwa ya kuitangaza Zanzibar kuwa ni kituo bora cha uwekezaji. Mhe. Spika, naishauri serikali iipatie fedha Mamlaka, angalau iweze kutayarisha "*Investment Forum*" mbili za nje, moja upande wa Magharibi na moja upande wa Mashariki na moja ndani ya nchi kwa kuwaalika wawekezaji kutoka pande zote za dunia kuja hapa Zanzibar. Mhe. Spika, hili kongamano la ndani litakuwa na faida kubwa zaidi, kwani wawekezaji watakapokuja ndani watajionea wenyewe hali halisi ya uzuri, utulivu na ukarimu wa Wazanzibari.

Mhe. Spika, nimezungumza mara nyingi juu ya kuimarisha maeneo huru ya Fumba na Micheweni kwa kuyawekea miundombinu muwafaka ambayo itawavutia wawekezaj. Lakini kinachodhihirika ni serikali kupatwa na kigugumizi juu ya hilo. Kwa hivyo, tusitegemee hata siku moja kuwa kutakuwa na muwekezaji atakaejitokeza kuwekeza katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Mamlaka ilijipangia kuidhinisha miradi 50 na mpaka Machi, imeidhinisha miradi 26 sawa na asilimia 52 ya lengo. Mwaka 2010/2011 imepanga kufanya mchakato wa mapendekezo ya miradi mipya 60. Nimulize Mhe. Waziri. Jee, Mamlaka itaandaa miujiza gani hata ifikie lengo hilo?

SHIRIKA LA TAIFA LA BIASHARA

Mhe. Spika, shirika hili ndilo lenye kuhodhi ununuzi wa karafuu kutoka kwa wakulima kwa bei duni na kusafirisha nje zao hilo. Pamoja na kupewa msukumo mkubwa utalii, lakini bado karafuu ni tegemeo kubwa katika uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba bei za karafuu ulimwenguni ni za kupanda na kushuka, bado shirika linajilimbikizia faida kubwa na kuendelea kudumaza mkulima wa karafuu na hatimae kumfanya ashindwe kuyahudumikia mashamba yake, matokeo yake ni kupotea mikarafuu na kushuka uzalishaji wa karafuu kutoka wastani wa tani 10,000 mnamo miaka ya 60 hadi kufikia tani 3000 mnamo miaka ya hivi karibuni. Hali hii ya kushuka uzalishaji wa karafuu bado itaendelea kwani hiyo mikarafuu kidogo iliyobakia bado inaendelea kufa na kukatwa wala hakuna hatua muafaka inayochukuliwa kukabiliana na hali hiyo.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo cha mikarafuu kutengewa shilingi milioni themanini ni dhihaka wanayofanyiwa wakulima wa karafuu na serikali yao. Serikali kama kweli ingekuwa makini basi ingaliandaa mpango madhubuti wa uhamasishaji, upandaji na ushughulikiaji mikafuu. Kwa mfano, mkulima kama amechukua miche 100 ya mikarafuu, baada ya miezi 6 atembelewe na mabwana shamba kuangalia maendeleo ya mikarafuu hiyo.

Ikiwa baada ya muda huo itaonekana miche hiyo inaendelea vizuri basi apongezwe na kupewa motisha na maelekezo ya utunzaji zaidi. Ziara hizo za mabwana shamba zifanywe kila baada ya kipindi fulani mpaka mikarafuu hiyo ifikie kiwango cha kuzaa. Wakati huo ikiwa miongoni mwa mikarafuu 100 aliyochukuwa mkulima angalau asilimia 90 au 80 imefikia kiwango cha kuzaa basi apewe zawadi maalumu na kutangazwa kwa wengine, ili na wao wahamasike kupanda mikarafuu na kuitunza.

SHIRIKA LA BIASHARA LA MAGARI

Mhe. Spika, shirika hili lilianzishwa kwa mintarafu ya kununua magari ya serikali na magari mengine kwa ajili ya kuwauzia wananchi. Mtaji ulioanzishiwa shirika ulikuwa mdogo sana. Lakini kwa bei za wakati huo ulikidhi haja. Hivi sasa kwa bahati mbaya sana serikali imebadili mwelekeo, kwani badala ya magari ya serikali kununuliwa kupitia shirika hili, sasa yananunuliwa kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi. Mimi sielewi kuna mantiki gani juu ya hili, labla Mhe. Waziri anieleweshe kwa manufaa ya baraza.

Mhe. Spika, baada ya uongozi wa shirika kuona kuwa shirika hili limeachwa mkono, umebuni mbinu mbadala kwa kuliendeleza shirika, nawapongeza kwa hilo. Mhe. Spika, kila mwaka tunapoelezwa juu ya shirika hili tunaambiwa kwamba limeweza kufanya faida na hata mwaka huu maelezo ni hayo hayo.

Mhe. Spika, jambo linalosikitisha ni kwa shirika kukataa kata kata kulipa gharama za mkaguzi wa mahesabu yake kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Fedha ambazo zinaingia katika Mfuko wa Serikali. Ninamuomba Mhe. Waziri alieleze Baraza hili sababu za msingi zinazopelekea shirika lake kufanya hivyo pamoja na kwamba linafanya faida, vyengingevyo sitaondoa shilingi katika Bajeti yake.

SHIRIKA LA UTALII NA HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Spika, pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na uongozi pamoja na wafanyakazi wa shirika, bado utendaji wa shirika hili ni wa kusuasua. Hii inatokana na kwamba rasilimali nyingi za shirika zimechukuliwa na serikali kuu bila kufidiwa au kuongezewa mtaji. Shirika kila mwaka linashindwa

kuliendeleza eneo lake lilioko Vitongoji Pemba (lenyewe au kwa kumpata mbiya). Shirika limeandaa mikakati gani madhubuti hata ikawa linashindwa kupata ufumbuzi juu ya eneo hilo? Na hali hiyo itaendelea hadi lini na wizara kama msimamizi wa taasisi zilizochini yake imetoa na itatoa msaada gani.

Hoteli ya Bwawani ni rasilimali muhimu ya serikali. Kwa hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kutunzwa na kuendelezwa. Malengo ya serikali ni ama kuifanya hoteli kuwa ni shirika linalojitegemea au kuingia ubia na mwekezaji ama wa ndani au wa nje kwa ajili ya kuendesha na kuitangaza hoteli hiyo. Malengo hayo yote hadi sasa yamegonga mwamba. Ninamuomba Mhe. Waziri, alieleze Baraza lako tukufu nini hasa hatma ya hoteli hiyo.

Mhe. Spika, kwa sasa shughuli kubwa ya hoteli ni kukodisha kumbi zake kwa shughuli mbali mbali, kupiga disko na kukodisha vyumba kwa wageni wanaotembelea hapo, pamoja na kukodisha baadhi ya vyumba kwa taasisi nyengine kwa shughuli za kiofisi. Ninamuomba Mhe. Waziri alipatie Baraza lako tukufu mchanganuo wa makusanyo wa mapato yanayokusanywa na hoteli kwa mwaka. Kwa mfano, ukodishaji wa kumbi na kadhalika.

Mhe. Spika, kazi yoyote inayofanywa huwa ina mpango maalum na muda wa kumalizika pamoja na gharama zake. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri anieleze utengenezaji wa vyumba vya hoteli unategemewa kumalizika lini na utagharimu kiasi gani?

KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii ni chombo kinachosimamia sekta tunayoambiwa ni sekta kiongozi katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Sasa kama hivyo ndivyo, kwa nini kamisheni haijawezeshwa ipasavyo ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa upeo mkubwa? Mhe. Spika, Kamisheni itawezaje kuitangaza Zanzibar kiutalii katika masoko yanayotanuka duniani kwa kupangiwa kupatiwa asilimia 0.2 ya bajeti ya serikali kwa kutekeleza kazi zake?

Mhe. Spika, uanzishwaji wa utalii pamoja na kuwa na lengo na madhumuni ya kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa pia ilikuwa na lengo la kumsaidia mwananchi mmoja mmoja kuongeza kipato chake na kupunguza umasikini. Mhe. Spika, lengo kwa upande wa wananchi bado halijafikiwa kwani kuna matatizo kadhaa kwa mfano wawekezaji wenyeji hawapewi misamaha ya kodi, wageni wanaruhusiwa kuwa na *tour operators* kama wananchi, halikadhalika na mahoteli yanayofungua *tour operators* mfano *Breeze Beach Club* na kadhalika.

Mhe. Spika, *tours* zinazofunguliwa na wageni zinakuwa na mitaji mikubwa, kwa hivyo *tours* za wenyeji haziwezi kuhimili ushindani na hatimaye hutetereka au kufa kabisa.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo linawakabili wenyeji ni la biashara ambazo zilikuwa zinaendeshwa na wenyeji mfano biashara za kanga na vikoi sasa zinaendeshwa na wazungu. Baadhi ya watembezaji watalii ni wageni na wafanyakazi mahotelini kuanzia ngazi za juu na hata wafyagizi, wengi wao ni wageni.

Mhe. Spika, yapo matatizo mengi ambayo yanaikabili sekta ya utalii ambayo mengine hupelekea serikali kupoteza mapato mengi. Kwa mfano, wenye mahoteli huyauza mahoteli yao au kuyabadili majina baada ya kuona kwamba muda wa msamaha wa kodi unakaribia kwisha.
Mhe. Spika, Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza lako tukufu ni hoteli ngapi zilizofanya hivyo na serikali imepoteza kiasi gani.

Mhe. Spika, wako baadhi ya watu huja nchini kwa kazi ya *volunteers* baadae hujiingiza katika biashara ya utalii. Je, Mhe. Waziri hili halioni kuwa ni tatizo?

Mhe. Spika, pia kuna tofauti ya bei wanazopangiwa *Local Tour Operators* na *Foreign Tour Operators.* Pia baadhi ya hoteli huzuia matangazo ya *Local Tour Operators* kuwekwa mahotelini na badala yake wanaweka ya kwao.

Mhe. Spika, hivi sasa kidogo kidogo kumeanza kujitokeza Utalii wa Ngono *(Sex Tourism)* sijui hili Mhe. Waziri analielewa? Kama analielewa amechukua hatua gani kuzuia balaa hilo. Kama halielewi namuomba afuatilie kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya sekta hii ya utalii nashauri yafuatayo:-

a) Wizara itafute vijana kutoka vyuo vikuu wafanye utafiti kwenye sekta ya utalii kuona ni kiasi gani wananchi na sehemu zenye utalii zimenufaika na ni kwa kiasi gani zimeathirika kimazingira, kimila na kiutamaduni. Halikadhalika, wewekezaji wenyeji wamenufaika na kufilisika kiasi gani.
b) Kutengwe maeneo maalum ya fukwe kwa ajili ya wananchi nao waweze kupumzika.
c) Hoteli zinazofungua *Tour Operation* ziadhibiwe kwa kutozwa faini isiyopungua dola 1000.

d) Utafutaji masoko ya utalii – *Tourism Marketing* ifanyiwe mapitio kwani kuna baadhi ya taasisi kama vile *Serena Tours* na *Explore Zanzibar* wanajiingiza katika kazi hiyo ambayo ni shughuli ya Kamisheni ya Utalii.

e) Mawasiliano ndani ya mahoteli kati ya wageni yasidhibitiwe na wawekezaji yaachiwe *Tour Operators.*

f) *Ground handling* zisifanywe na makampuni ziachiwe wenyeji, mfano wa makampuni hayo ni *Aba Kombin kent* na *Ocean Tours.*

Mhe. Spika, kama hiyo asilimia mbili ya bajeti ya serikali inayotengwa ingelikuwa inatolewa yote basi japo kuwa haitoshi ingekuwa afadhali. Kutokana na hali hiyo, ndio utaona malengo yanayopangwa kuwa yanarudiwa kila mwaka wa bajeti. Changamoto hii si kwa Kamisheni ya Utalii peke yake lakini takriban ni kwa taasisi zote zilizoko chini ya wizara hii. Sasa unaweza kujiuliza Mhe. Waziri anafanya nini? Je, hawawajibiki yeye pamoja na watendaji wake? Hapana waziri na watendaji wake wanawajibika ipasavyo lakini wanarudishwa nyuma na utaratibu mbaya wa upangaji na utoaji kasma.

Mhe. Spika, hili ni tatizo. Kama tunataka kuikwamua Zanzibar kiuchumi ni budi tubadilike katika mipango yetu, hasa tukizingatia kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu kwani hali ikiwa itaendelea hivi kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza nafasi.

TAARIFA YA JUMUIYA ZA MAENDELEO ZA KIKANDA

Mhe. Spika, Zanzibar kama nchi huru haiwezi kubaki nyuma na kutoshiriki katika jumuiya kama hizo kwa manufaa ya Wazanzibari. Mhe. Spika, ushiriki wa Zanzibar katika jumuiya hizi chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna matatizo makubwa kwa Zanzibar hasa kwa vile wenzetu hawana nia njema na Zanzibar. Mhe. Spika, sijui wanaoshiriki kwenye vikao vya jumuiya hizo wanakuwa makini kiasi gani kwani mara nyingi maamuzi yanapotolewa huwa yanaiathiri Zanzibar ambayo huwa katika upande wa kupoteza. Mhe. Spika, tujitahidi kama inavyowezekana washiriki wetu kwenye jumuiya hizo wawe ni wataalam wenye kuwajibika badala ya wanasiasa wanaogopa kupoteza nafasi zao kwa kusimama kidete kuitetea Zanzibar.

Mhe. Spika, hivi sasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Protokali ya Soko la Pamoja imeshasainiwa, halikadhalika na ile ya Umoja wa Forodha. Sasa la kujiuliza ni vipi Zanzibar itanufaika kiuchumi katika hali hizo? Wakati

uwekezaji katika kilimo ni asilimia 0.4 ya bajeti na ni asilimia 0.3 ya bajeti katika sekta ya uzalishaji viwandani.

Katika miaka 10 ya awamu ya 6 kuna mradi mmoja wa uwekezaji katika kilimo na hakuna hata mradi mmoja wa uwekezaji katika uvuvi pamoja na kwamba tuna utajiri mkubwa uliotuzunguka.

Mhe. Spika, njia pekee ambayo inaweza kuikwamua Zanzibar kiuchumi ni kuifanya Zanzibar kuwa ni eneo tengefu la kiuchumi *(Free Economic Zone).*

Mhe. Spika, nimesikia kwamba suala hili la kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi limejadiliwa katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi zote za jumuiya waliafiki, isipokuwa Tanzania Bara wao wakataka suala hilo lifanyike Mwanza katika Ziwa Victoria. Je, Mhe. Spika, ndugu zetu wapenzi wanaitakia mema Zanzibar?

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba Mhe. Waziri anieleze juu ya haya yafuatayo:-

- Kuna kiwanda cha maji kinachomilikiwa na wazalendo huko Kikungwi Pemba. Zaidi ya miaka 2 sasa wamiliki hao hawajapatiwa hati miliki ya eneo hilo. Ni kwa sababu gani na wizara imechukua hatua gani kuwasaidia wawekezaji hao?
- Jengo linalotumiwa na Benki ya *Barclays* Chake Chake Pemba linamilikiwa na nani sasa na je, wamekodishwa, wameuziwa au wamepewa huba? Serikali inanufaika vipi na jengo hilo?
- Muwekezaji Carlos aliyeko Chokocho anafanya shughuli gani na serikali inanufaika vipi na muwekezaji huyo? Serikali imepata mapato kiasi gani tokea kuwepo kwake hapo.
- Maeneo huru ya Fumba, Micheweni na Amani yanaendelezwa vipi ili kuwavutia wawekezaji?
- Vinu vya kusindika mafuta ya majani ya mikarafuu na kadhalika vilivyogaiwa kwa wananchi na *ZSTC*,
- Vinazalisha kiasi gani kwa mwaka?
- Serikali inanufaika vipi?
- Wananchi nao wamenufaika vipi?
- Je, lengo la MKUZA la kupunguza umasikini wa kipato limefanikiwa kiasi gani kupitia vinu hivyo?
- Je, ni lini na hatua zipi zitachukuliwa kubinafsisha zao la karafuu?

HITIMISHO

Mhe. Spika, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji inasimamia taasisi muhimu katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini wa kipato kwa

wananchi. Kwa hivyo, ni muhimu kwa serikali kuelewa hilo na katika kugawa rasilimali chache ni vyema wizara ikatengewa fungu muafaka kwa ajili ya kukamilisha malengo iliyojiwekea.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha na kuvunja moyo kuona kwamba inayoitwa sekta kiongozi ya utalii inayosimamiwa na Kamisheni ya Utalii ambayo imepewa jukumu la kuitangaza Zanzibar kiutalii na kukuza utalii inapangiwa asilimia 0.17 ya bajeti ya serikali na bahati mbaya hata kiasi kama hicho wakati mwengine hakipatikani chote. Kama kweli tunakusudia kukuza utalii ni lazima hilo lionekane na kuchukua hatua muafaka.

Mhe. Spika, msisitizo wa kuiwezesha sekta binafsi ni kufanya utaratibu wa kuipatia mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo. Hili ni jambo la msingi na lenye umuhimu.

Mhe. Spika, ninamaliza kwa kukushukuru tena kwa kunivumilia kutoa maoni ya kambi ya upinzani na pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa makini. Ninamuomba Mwenyezi Mungu mtukufu awape wajumbe wako mafanikio katika michakato inayowakabili ili waweze kujumuika pamoja baada ya Uchaguzi Mkuu kwa kuendelea kuisaidia nchi yetu kwa kazi zao nzuri walizozionesha katika kipindi kinachomalizika.

Mhe. Spika, mwisho ninamuomba tena Mwenyezi Mungu mtukufu awape *tawfiq* viongozi walioko madarakani kwa kutembea juu ya maneno yao kwamba tufanye uchaguzi ulio huru na wa haki bila ya vurugu. Amin.
Mhe. Spika, kwa heshima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie bajeti hii kwa makini na mumuelekeze Mhe. Waziri kwa faida ya wote. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri Kivuli kabla hujaondoka hebu angalia ukurasa wa 7, para ya 3, mstari mmoja kabla ya mwisho wa para hiyo, pale ulipoandika labda nianzie juu "Mhe. Waziri alieleze Baraza hili sababu za msingi zinazopelekea shirika lake kufanya hivyo pamoja na kwamba linafanya faida vyenginevyo sitaondoa shilingi katika bajeti".

Kwa kuweka rekodi safi sijui ndio umekusudia?

Mhe. Salim Abdulla Hamad (Kaimu Waziri Kivuli wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji) Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kuwa makini sana wakati nilipokuwa nikisoma hotuba hii refu. Lakini kama nilivyosema mimi ni kwa niaba ndio sina mamlaka ya kubadilisha chochote. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Tunamshukuru sana Mhe. Kaimu Waziri Kivuli anajua kutumwa. *(Kicheko)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri ambazo tunaamini kwamba biashara ni uti wa mgongo wa nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia machache katika sekta nitakazozigusa, lakini kabla ya hapo niseme tu kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja sina matatizo.

Mhe. Spika, sekta ya utalii ni sekta mama naweza kusema kwa sasa hivi kwa hapa nchini kwetu. Tukiangalia kwa hali yoyote ile sehemu hii imeajiri vijana wengi katika kujitafutia riziki zao lakini pia kulisaidia taifa letu katika kuleta maendeleo ya hali za wananchi wetu.

Mhe. Spika, utalii tukitaka tusitake ni vyema tukawasomesha vijana wetu vizuri, tukawaendeleza vizuri, Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii kutoa taaluma mbali mbali katika kuendeleza harakati za kuleta maendeleo ya watu wetu.

Mhe. Spika, kwa asilimia kubwa tunaamini kwamba vijana wetu wengi wako katika vijiji mbali mbali, ukianzia mahoteli ya mjini hata vijijini. Mhe. Spika, wakati wa utalii vijana wengi utawatafuta mjini huwaoni, lakini tunaposema kwamba ikifika leo *season* vijana wengi utawakuta wako mijini wamekaa hawajui waende wapi. Kwa hivyo, niseme tu kwamba sekta hii muhimu hasa tukizingatia kwamba vijana wetu wana mambo mengi amabyo wanajipatia riziki zao kwa njia ya halali ya kuendesha zile kazi za utalii.

Kwa mfano Mhe. Spika, kuna vijana wetu wanaojituma katika sehemu za udereva, usafirishaji wa kuwapeleka watalii baharini na kutembelea sehemu mbali mbali. Lakini pia kuna vijana wetu wanaouza vitu mbali mbali vya utalii vya asili vya nchi yetu na wale wenye nyumba zao ambazo wamewekeza vizuri kwenye maduka yao wanapata faida.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri taaluma itolewe zaidi kwa wananchi wetu wanaoishi katika sehemu hizi wanazofikia watalii ili uimarike uhusiano mwema baina ya watalii na wananchi wazalendo.

Mhe. Spika, mimi nilipata bahati ya kutembelea nchi ya Uganda katika utalii wao. Mhe. Spika, Uganda iko sehemu wanakwenda watalii wengi sana. Huko bahati nzuri wenzetu kutokana na uendelezaji wa viwanda vyao katika nchi yao wamejaribu hata sabuni zinatoka pale pale nchini kwao, ukiacha maji na mambo mengine. Mhe. Spika, biashara hii inakwenda sambamba na sehemu ya viwanda na biashara nyenginezo. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri akatilia mkazo sana sekta ya viwanda katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kama vitapatikana viwanda vitatu vikubwa katika nchi yetu Unguja na Pemba tunaweza kuwahakikishia wananchi wetu wengi wa nchi hii hasa vijana wetu na kinamama wakapata ajira kubwa sana.

Mhe. Spika, mfano tulipotembelea Arusha katika sekta ya viwanda, yaani nakusudia katika viwanda mbali mbali ambacho kiwanda kile cha vyandarua. Mhe. Spika, tuliwakuta vijana wanafika hata elfu tano zinakwenda shifti sijui mara ngapi maana kutwa kucha. Lakini harakati zilizokuwepo pale zinaonesha dhahiri kwamba kama na sisi ukiacha chochote ukatafuta kitu ambacho kina mahusiano kama hayo, basi vijana wetu katika nchi yetu watapata changamoto ya kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tuendelee katika wawekezaji wazuri lakini wawekezaji ambao wanaweza kutoa tija kwa jamii yetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri viwanda ni sehemu ya uti wa mgongo wa nchi yetu vile vile, lakini viwanda ni sehemu ya kupatikana ajira kubwa kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, katika kuendesha biashara pia ningemshauri Mhe. Waziri na namuomba sana anisikilize kwa hili. Mhe. Spika, biashara ya magari inaletwa na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kupitia Shirika la Magari, hata kama kuna makampuni mengine lazima yapitie pale kulipa ada ya watu inayokubalika. Hivyo tuseme Mhe. Spika, kwa kuwa wizara inataka kukuza biashara na wizara hii zimegusana wizara mbili, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto inahusika na Wizara ya Biashara yenyewe inahusika.

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa suala la biashara linakwenda katika pande mbili, tuangalie tuna gari ngapi kama daladala zetu za wananchi wetu zinazotembea katika miji yetu Unguja na Pemba na vijana wangapi wamepata ajira katika sehemu ile. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri hii naisema kwa sababu biashara ni sehemu moja ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu na zile ajira ambazo Chama cha Mapinduzi kiliahidi katika ilani yake kwamba tutatoa ajira milioni moja, basi mojawapo katika vijana wetu ambapo naamini kama tutazihesabu daladala zetu watafika vijana elfu nne au elfu tano.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kama kuna milki za kuingiza gari katika nchi yeye ndio anayeingiza kupitia Shirika lake la Magari au chombo kinachohusika. Kama zinatakiwa kuzuiliwa daladala hizi paelezwe sababu za msingi ambazo zitaturidhisha sisi tuliokuwemo humu ndani kwa niaba ya wananchi wetu ambao wanatutegemea.

Mhe. Spika, umetembea nchi nyingi na Waheshimiwa Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliokuwemo humu wametembea nchi mbali mbali. Hebu tuelezwe na Mhe. Waziri huko zinakotoka zile daladala za dungu ninazosemea mimi za wenzetu hawa zina kasoro gani na zina tatizo gani. Kwa sababu tunasema kwamba kutakuwa na zogo katika mji wetu labda kuna magari mengi mimi siamini.

Zamani Mhe. Spika, kulikuwa na magari makubwa sana ya *Austin* au *Boris* kama zitakaa hapa Darajani gari tano tu nyinyi pakupita mtapatafuta. Lakini leo kuna vigari vyetu *luxury*, kuna dungu, vibasi vya kawaida vidogo vidogo, *dyna*, zikikaa hata 40 hapana matatizo. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri yeye ndio anayeleta magari katika nchi akae na Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi walijadili hili suala.

Mhe. Spika, nazungumza hili kwa dhati kabisa na kiukweli kwamba wananchi wametutuma wanasikitika. Tumesema tunawatafutia ajira, leo ajira inataka kuwaendea puta, yaani iwatoke si vyema. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anataka mapato lakini pia Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto yeye ndio mwenye kutafuta hizo ajira zenyewe kwa vijana wetu. Kwa hivyo, hili nasema liangaliwe ili kuleta manufaa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kazungumza katika hotuba yake kwamba anaandaa hivi sasa sehemu moja kubwa ya kuwekwa eneo la maonesho ya biashara. Mhe. Spika, mimi namuunga mkono sana Mhe. Waziri lakini pia niseme tumechelewa. Kwa sababu sisi tunaanza halafu tunaondoa hii mara ya tatu, sasa anatafuta watu labda wa kuwekeza ili kuweka hayo maonesho ya biashara.

Mhe. Spika, hilo ni suala zuri, lakini niombe tu kama alivyosema Waziri Kivuli na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwamba anaomba haya maeneo yakishapatikana yasiwe tena wanapewa wahisani tuachane na hayo. Mimi naunga mkono moja kwa moja kwamba linalofanywa pale kama hapa kwetu Mwanakwerekwe palikuwa pameshazoea, tukatoka pale pakenda Tunguu pazuri zaidi. Mhe. Spika, kijiji kingekuwa kama tuko *Kilwa Road* kule kwenye maonesho ya Saba Saba maana pameshazungukwa lakini yanayofanywa nayo si mabaya kwa sababu kutafuta elimu ni sehemu moja ya kukuza maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mhe. Spika, hivi sasa tumo katika soko la Afrika Mashariki na soko la pamoja limeanza rasmi kuanzia tarehe mosi mwezi huu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri Zanzibar hatuna kitu, Zanzibar tunategemea kupokea kitu. Yaani sisi hatuna cha kusafirisha tunategemea kitoke nje kiingie kwetu. Lakini sasa hivi umefika wakati Mhe. Spika, ni vyema basi wananchi wetu wafanyabiashara mbali mbali wa kada mbali mbali wakaelimishwa wakatafuta bidhaa nzuri, bidhaa madhubuti tukasafirisha.

Lakini mimi niseme tu Mhe. Spika, kama tutakuwa makini kwa mfano tuna maeneo mazuri ya uvuvi. Kwa sababu kama hukupanga huwezi kupanga, upange utekeleze upate. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa nchi nyingi hazina samaki watamu kama wa Zanzibar, maana Zanzibar samaki ni watamu kuliko Afrika ya Mashariki yote naweza kusema hivyo, bahari kali, samaki wake watamu. Ukenda huko ukanda wa Kiwengwa na kwengineko utampenda samaki wa kule kuliko wa maji ya huko.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri haya ayaangalie hivi sasa umefika wakati kwamba tutafute kila nyanja wawekezaji wazuri wazuri ambao wana uwezo wa kusafiri mbali kuvua samaki na kuleta katika nchi yetu, ili nchi ipate maendeleo lakini pia tupate bidhaa ya kusafirisha katika soko la pamoja.

Mhe. Spika, hivi sasa tumo katika harakati za utalii wameshaanza kuja, lakini nimuombe sana Mhe. Waziri mimi bado nasema pamoja na kutafuta walinzi, *radio call*, tutafute walinzi wanaoweza kulinda katika mahoteli yetu. Mhe. Spika, sikubaliani hata siku moja mimi kuona kabila lipo pale na marembo yake akawa mlinzi, yule si mlinzi kwa sababu akisikia kwii anakwenda mbio wala humwoni.

Mhe. Spika, nasema kwamba sehemu moja ya kulinda usalama wa watalii uko mikononi mwetu. Kwa hivyo, namuomba kwa dhati Mhe. Waziri kwa nia njema kabisa tuamini kwamba pamoja na juhudi zinazoendelea katika maeneo yetu na ukanda huu ambao tunautegemea sana katika sehemu ya utalii, basi tutafute walinzi na wenye mahoteli wapewe masharti mazuri ambayo lazima wayafuate. Kwa sababu wakati wa ulinzi ule wa magongo umekwisha na asilimia 90 ya mahoteli yetu ukitembelea yako wazi.
Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa usalama wa wageni wetu kwa sababu mgeni anapokuja nyumbani kwako akiondoka salama atakusifu, ikitokea hitilafu Mwenyezi Mungu asitujaalie itokee patakuwa na matatizo kidogo.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nampongeza Mhe. Waziri na naikubali hotuba hii kwa asilimia mia moja sina matatizo.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia bado jioni hii akatupa uzima wa kuweza kuendelea na shughuli zetu. Lakini pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa pili katika wachangiaji hawa wa kawaida ukimuacha Mhe. Waziri, Mwenyekiti na Waziri Kivuli.

Mhe. Spika, tatu nimpongeze Kaimu Waziri Kivuli kwa kuweza kujibu ile hoja uliyomwambia utaondoa shilingi au kwa niaba. Kwa hivyo, nafikiri suala lile kalifikiria wakati gani.

Mhe. Spika, nne nimpongeze Mhe. Waziri kumbe na yeye kuchukua fomu ya urais angeweza kuifanyia kazi lakini kafanya wasi wasi. Lakini yote haya yamekuja kutokana na watendaji wake walivyo mahiri katika wizara hii. Watendaji kwa kweli wamejitahidi na inshaallah Mwenyezi Mungu awape upeo zaidi wa kuona na kumulika yale ambayo yatatuletea faida katika nchi yetu ili wananchi waneemeke.

Mhe. Spika, nianze kuingia katika bajeti kwenye Mipango na Sera. Mwaka 2009/2010 Mhe. Waziri kaeleza, katika malengo aliyojipangia ni viwanda na biashara ndogo ndogo. Mwaka 2010/2011 malengo yale bado yapo. Sasa Mhe. Spika, mimi nataka Mhe. Waziri aje anieleze mwaka 2009/2010 hatukuyafikia au hayakukamilika au yamekuaje.
Mhe. Spika, nikiondoka hapo, niende kwenye uimarishaji wa biashara ndogo ndogo. Suala hili limekuwa ni kilio kwa wananchi wetu katika suala hili katika kutaka kujinyanyua kiuchumi. Hivi karibuni kwenye maswali na jibu Mhe. Asha Moh'd Hilal kaweza kugusia kwamba wananchi wetu bado wanakerwa au wanapata usumbufu kwa biashara ambazo wanazitoa Zanzibar na zikifika Tanzania Bara zinalipiwa tena. Mawaziri wakajibu wakasema suala hili tayari katika kero limeshaondoka na haliko.

Mhe. Spika, mimi nataka nimfahamu Mhe. Waziri biashara ndogo ndogo ni kuanzia zipi na ambazo kuwa zinatupelekea usumbufu kwa watu wetu ni zipi. Kwa sababu mimi juzi nilikuwepo Dar es Salaam kwa bahati nzuri wale wanaochukua biashara hapa Zanzibar kupeleka Bara kuanzia boksi moja mpaka mawili, basi nikawaona wamezuiwa na wakaambiwa ingieni chumba hicho na walipotoka tayari wanarisiti ambazo wamepewa kwa malipo.

Sasa Mhe. Spika, waziri aje kuniambia ni biashara zipi ambazo kuwa tayari wamekubaliana kuwa zisilipiwe ushuru mara mbili. Au ni utaratibu gani ambao

unataka ufuatwe ili wafanyabiashara wetu wasipate usumbufu. Lakini vile ni kuinyima Zanzibar mapato kwa sababu mfanyabiashara wa Shs. 100,000/= amejipangia malengo yake ameshatoa nauli yake ya Shs. 10,000/= au Shs.15,000/= haizidi hapo anakwenda kula na watoto, hatimayake ukamwambia alipe tena Shs. 10,000/= au Shs.15,000/= kwa hivyo itakuwa umempangia asifanye kazi tena mtu huyo.

Kwa hivyo, nikitaka Mhe. Spika, Mhe. Waziri aje kunieleza kuwa ni biashara zipi ambazo kuwa wamekubaliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili mfanyabiashara yule asisumbuliwe na biashara hizo. Lakini katika jibu (c) Mhe. Spika, ni mazingira ya biashara, kwa kweli linaleta masikitiko.

Juzi vile vile wakati wa maswali na majibu au Mhe. Waziri Kivuli wa Habari, Utamaduni na Michezo kasema zile biashara zinazouziwa pale mfano Darajani, mafuta, dawa za mswaki na vitu vyenginevyo, huwa vimeshamaliza muda. Lakini kwa utaalamu kabisa wanaondoa nambari ile ya kwenye vile vitu ya kuonesha muda wa utumiaji, halafu ikarudi ikauzwa kwa mlaji.
Sasa mazingira ya kibiashara Mhe. Spika, tunataka tuelewe ni yapi sasa, ili kama hayajazibitiwa yale, si kweli. Kitu kinachouzwa dukani kilichokuwa hakijamaliza muda ni Shs. 10,000/=, lakini ukienda pale wanapouza mikononi ukakipata kwa Shs. 3,000/= na mwananchi anasema labda kiko hai, hatima yake keshokutwa kinamletea matatizo. Kwa hivyo, mazingira ya kibiashara ningemuomba Mhe. Waziri kwa jitihada zake pamoja na watendaji basi aongeze juhudi. Wauza biashara ni sisi, ingawa tukisema hivyo wananchi wataona tunawakosesha uhondo wao, maana vile kumbe ndio nafuu yao ya kupata kula, lakini vina athari.
Mhe. Spika, mfano mdogo tu tumesema tulinde mazingira Mhe. Spika, ya mifuko ili nchi yetu iwe nzuri. Lakini hivyo inavyomiminika bora vile zamani ilikuwa haipo kuliko hivi sasa. Sasa Mhe. Rais ambaye alikuwa ni wa awamu ya nne Mwenyezi Mungu amrehemu, wakati zinatoka zile kanga za mitaani, alipeleka jina lake moja akasema ‘kiumbe mzito’ na ikaja kanga hiyo, na kweli kiumbe ni mzito hata ukamsarifu vipi. Maana hata ukimtetea ili kulinda afya yake na usalama wake basi hakubali yeye.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi. Kila mmoja na majukumu yake ajitahidi kuwaelekeza watendaji wake na kuwasimamia vyema katika biashara ili isilete athari kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika ukurasa wa 10 sehemu inayosema changamoto ambalo kuwa pia limekuja, ambalokuwa Mhe. Waziri kalikusudia. Ukiingia kwenye ukurasa wa 11, pia na malengo yake ni viwanda. Mhe. Spika, viwanda japokuwa Mhe. Waziri kavitaja kwenye hotuba yake kavitaja viwanda vidogo vidogo vya makonyo, vya marashi ya mchai chai na vyengine. Ni

vyema kwa vile tunayo matunda mengine Mhe. Spika, yakiingia msimu wake basi huamini, kama hivi sasa yameingia machungwa basi ukifika pale Darajani basi machungwa 20 kwa Shs. 500 na hatimayeka machungwa yanarudi yanaoza maskini.

Mhe. Spika, ni vyema kama kweli tunawashajihisha wawekezaji, basi wakaja wakatuwekea viwanda kwa yale matunda ambayo tunayo kama machungwa, maembe na mabungo basi Mhe. Spika, tusingepata shida watu wetu wangepata kazi na nchi yetu ingeneemeka. Lakini cha ajabu tunayasafirisha maembe hapa kwenda Oman, halafu maembe yale yale yanarudi kwetu tena kwa bei kubwa zaidi, ni mambo ya kusikitisha. Japokuwa ardhi ni ndogo, lakini bado tuna uhai na nguvu ya kuweza kutenda yale yaliyopo tunayaweza. Mhe. Spika, viwanda vikubwa bado hatujaviweza, lakini hivi vidogo vidogo vya matunda basi wawekezaji wangeshajihishwa ili wakaja Zanzibar wakaweka.

Mhe. Spika, ukiingia msimu wa mabungo basi kocha moja ni Shs. 200/=, lakini yakiadimika moja ni Shs. 500 basi hulipati. Kwa hivyo, ingekuwa ni faida kwa wakulima pia ni faida kwa nchi yetu. Mhe. Spika, juisi ya bungo wazungu wanavyoipenda hatari. Lakini Mhe. Spika, kubwa zaidi ni viwanda vya samaki, japokuwa hatujavua bahari kuu. Hizi bahari zetu ndogo ndogo tunazovua basi wakati ikiingia msimu wa madagaa hapa hatari.

Nafikiri Mhe. Najma Khalfan kazungumza hivi karibuni kwamba kule kwao Mkanjuni hutembezwa kwa magari ya ng'ombe, basi ingekuwa ni vyema Mhe. Spika, waziri akashajihisha serikali ili wakatafutwa wawekezaji wa viwanda vya samaki, tusitafute madini ambayo hatuna, lakini yale tuliyokuwa tunayo basi tuyaendeleze.

Cha ajabu Mhe. Spika, Oman hakuna wavuvi, lakini samaki wanaletwa kwenye makopo kuja hapa Zanzibar kutoka Oman. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri wangelizingatia hili ili wakawashajihishwa wawekezaji wakatuwekea viwanda vidogo vidogo kwa yale ambayo tunayo. Kwa sababu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira juzi alitoa mwangaza mwema, kwamba tayari anahamasisha wananchi waanze kufuga samaki, licha ya kuvua baharini, samaki watakuja kutufukuza baadae. Lakini kama tutakuwa na viwanda vya kusindikia samaki basi tutapata kuuza sehemu nyengine na nchi yetu itaingiza mapato.

Mhe. Spika, niende katika Chuo cha Utalii. Kwa kweli hiki ni chuo ambacho vijana wetu Wazanzibari wengi wanakilengea jicho sasa hivi na wengi ajira zao wanazitegemea zitoke pale. Lakini vijana wale wakishakusoma na wakishayajua mazingira ya pale chuoni, kwa sababu wao wanakua wameshajiingiza kama ni watalii wenyewe wanayoyafanya mitaani basi ni

makubwa zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeiomba wizara pamoja na kuwasomesha vijana katika mambo ya utalii, lakini pia na desturi na mila ya nchi yetu wasiache, ili tusipoteze haiba ya nchi yetu Mhe. Spika. Kwa kweli vijana wanaipotezea nchi yetu malengo yake, wanaipotezea ile heshima ya Zanzibar.

Unaweza ukamkuta mtoto wa Kiafrika, mtoto wa Kimakunduchi au Kojani ana vidani shingoni vimempuputika basi kina mama hawasubutu kuvivaa, sasa sijui yale ndio masomo wanayosomeshwa katika chuo au ni mazingira gani ya kiajabu ajabu. Kwa hivyo, pamoja na kusomesha lakini wapewe na taaluma za Kizanzibari kwamba haya ndio maadili yetu na kazi ni hii.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kulinda muda wako ndio nimetazama saa na mimi. Nina imani kuwa unajikamata kidevu kwa kuona muda umeshakwisha. Mhe. Spika, ningeendelea kusema nimshukuru Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kunipa ushauri wa kuweza kujua kipi nifanye na kipi nisifanye. Naomba *Inshaallah* Mwenyezi Mungu pia chifupi wake awape uhai na nguvu mpya za kufanyia kazi. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awape uwezo zaidi warudi tena Barazani kuja kushirikiana na wenzao pamoja na mimi nikiwemo, ili kutekeleza majukumu yetu ya kazi hizi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Samia Suluhu Hassan asichoke kuwashawishi watendaji wake kuendelea na juhudi zao. Wasijekuona sifa zote tunazowapelekea ni kwa sababu ya maneno ya Mhe. Aman Karume na Mhe. Seif Sharif, hapana, na imani zao ambazo wanakwenda nazo na utendaji wao. Lakini vyenginevyo katika kipindi kinachofuata, tukiona mazingira hayaruhusu basi kwa kweli japokuwa serikali itakuwa ni ya pamoja, lakini tutakuwa ni wakali kwa kuwalindia wananchi heshima zao. Nasisitiza biashara za Darajani Mhe. Waziri watume watendaji wako ziangaliwe kwa vyema na akijulikana mtu anafanya huo ulaghai basi asipate msamaha, kwa sababu maradhi yamekuwa mengi na wataalamu wanatuambia kuwa vyakula ndio vinasababisha maradhi haya.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, naunga mkono hoja niseme kwa asilimia mia juu ya mia, lakini bora nitampa asilimia 90 kwa sababu asilimia 10 nilimwambia akienda safari za nje aniite kama *guard* wake hakuniita kwa hivyo nampa asilimia 90.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, na mimi naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii tukaweza kuhudhuria kikao hiki muhimu. Lakini pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii, ambapo kwa kweli kama ulivyosema aliwasilisha chini ya muda ambao umepangwa.

Lakini vile vile naomba niungane na rafiki yangu katika kumlaumu kidogo Mhe. Waziri kutokana na kwamba yeye hakujitokeza kugombea. Tunasema hivi kwa sababu dunia ya leo ni dunia ambayo inakwenda katika *gender equality*, kati ya wagombea 11 waliojitoza, kwa vyovyote *figure* ambazo tulikuwa tunaziangalia sana ni *figure* za Mhe. Samia Suluhu pamoja na Mhe. Asha Abdalla Juma. Lakini kuwaachia wagombea 11 wote wanaume, basi ile ni kuendeleza mfumo dume. Kwa hivyo, naomba mara nyengine kwa kweli hilo lisije likatoke, kwa sababu ni kuwarudisha nyuma wanawake.

Mhe. Spika: Hivi hizo fomu kwa upande huu wa upinzani huwa hazipo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar iko katika harakati kubwa sana ya kukuza uchumi, ndio ajenda yetu ya msingi ilioko mbele yetu. Vile vile tuko katika mpango maalum wa kupunguza umaskini kwa wananchi wetu chini ya programu ya MKUZA.

Mhe. Spika, mazingira ya nchi yetu ambayo ni visiwa, basi tunaweza tu kukuza uchumi kwa kutegemea sekta kwanza ya biashara, tunaweza kuimarisha uchumi wetu kwa kutegemea sera ya viwanda pamoja na biashara ya utalii. Sasa katika sekta hizi tatu ambazo ndizo tunazodhani zinaweza zikaimarisha uchumi wetu, viwanda na biashara sekta hizo zote zimejumuishwa katika wizara ya Mhe. Samia Suluhu Hassan.
Kwa hivyo, hii ndio kusema kwamba biashara ya biashara na viwanda tunayoizungumza sasa hivi ni wizara muhimu sana katika kukuza uchumi wetu. Kwa hivyo, msingi wa kukuza uchumi wetu ni kwa kupitia wizara hii.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu nadhani katika harakati zetu za kuelekea kukuza uchumi na suala zima la kupunguza umasikini bado safari ilioko mbele yetu ni kubwa sana. Kadiri tunavyo panga, kadiri tunavyopiga hatua lakini inaonekana kuwa safari ilioko mbele yetu ni kubwa. Kwa sababu tunahitaji utalii, utalii ambao kwa namna yoyote ile unaweza ukaingiza fedha nyingi katika nchi yetu. Bado hadi sasa utalii wetu haujawa na ile tija iliyokusudiwa bado hatujafikia katika lengo ambalo kama tukilitumia vizuri basi linaweza likaleta tija ambayo tuliikusudia.

Vile vile sekta ya biashara nayo haiendi mbele kwa Zanzibar, sekta ya biashara inarudi nyuma. Kwa sababu maana ya biashara ni kuuza pamoja na kununua. Ili tuseme kuwa tuna biashara maana yake ni lazima urari katika uuzaji na

ununuaji uwe unalingana. Lakini inavyoonesha kwamba nguvu za uagizaji ni kubwa zaidi kuliko nguvu za uuzaji katika nchi yetu.

Vile vile sekta ya viwanda kwa kweli imerudi nyuma. Katika miaka ya 1970 tuliona ni jinsi gani tulivyokuwa angalau na sisi tuna viwanda vinavyotambulika na vinavyojulikana katika eneo zima la Afrika ya Mashariki. Kwa sasa hivi viwanda vyetu vyote ambavyo tulikuwa navyo vimekufa.

Mhe. Spika, tunapozungumzia viwanda tunadhani ni vile ambavyo vinatoa bidhaa ambazo tunaweza tukauza katika soko. Mimi sidhani kama tunaweza tukaorodhesha kiwanda cha tambi, ama kiwanda cha chapati ukasema kwamba hicho ni kiwanda. Mhe. Spika, bado nadhani hiyo hatuwezi tukasema kuwa ni kiwanda.

Mhe. Spika, kwa sababu muda ni mdogo, kwa hivyo naomba nitumie fursa hii kwa kuchangia mchango wangu kwa kuuliza maswali. Swali langu la kwanza ambalo namuuliza Mhe. Waziri, naomba tu anieleze kwamba sasa hivi kuna maonesho ya kimataifa yanayoendelea pale Dar es Salaam. Maonesho ambayo yalianza juzi tarehe 01/07/2010, kwa sababu mataifa mengi yapo pale na mataifa yaliopo pale lengo la maonesho yale ni kujitangaza.

Je, Zanzibar sisi kwa upande wetu tumewakilishwa na makampuni gani, ama tumewakilishwa na kitu gani ambacho tunaweza tukasema kwamba na wenzetu nao watuone ili waje wavutike katika kufanya biashara katika nchi yetu. Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, Mhe. Spika, biashara siku hizi ni ya kidiplomasia. Mabalozi wanatumika sana katika kujenga diplomasia za kiuchumi. Sasa naomba tu anieleze ni namna gani mabalozi wetu tulionao katika nchi za nje, tunawatumilia vipi na wao wanatumika vipi katika kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza Zanzibar.

Mhe. Spika, hivi karibuni tulikuwepo Malaysia na kamati yako na kule Malaysia tulionana na balozi aliyeko kule. Lakini alitueleza kwamba tuna tatizo na salamu hizi zipelekeni, kuna deni la mchele sijui la Thailand. Deni hili kwa kweli halinipi fursa ya kwenda kumuona yeyote kwa sababu, bado Zanzibar inadaiwa. Sasa hiyo tulikuwa tunaeleza ni namna gani ambavyo mabalozi wetu tunaweza tukawatumilia katika kutuvutia wawekezaji, licha ya kikwazo alichokipata Balozi wa Malaysia, yaani Balozi wa Tanzania aliyeko Malaysia.

Mhe. Spika, swali langu la tata, ni kuhusu utekelezaji wa itifani ya soko la pamoja ambalo lilianza juzi tarehe 01/07/2010. Soko hili la Afrika ya Mashariki ambalo lina *consumer* zaidi ya 100, bila shaka ni soko kubwa sana.

Sasa sisi Zanzibar tumejiandaa vipi kulitumia soko hili, kuzitumia fursa zilizomo katika soko hili. Kinyume chake kama ikiwa hatukijiandaa ni kusema kwamba Zanzibar hilo soko la watu 100, basi litaendelea kuivamia Zanzibar na Zanzibar itatumika kama soko tu. Lakini vipi sisi Zanzibar tunaweza tukalitumia soko hilo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika: Unakusudia milioni 100.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ndio, milioni 100, *consumer* hawa walioko katika soko.

Mhe Spika, swali langu la nne ni kwamba katika kulitumia hili soko la Afrika ya Mashariki, nchi mbali mbali zimeanza sera maalum za kuwawezesha wananchi wao. Juzi nilimsikia Mhe. Uhuru Kenyata Waziri wa Fedha wa Kenya akizungumza namna gani Kenya inajiandaa katika kuwawezesha wananchi wake kimitaji. Sasa ikiwa nchi mbali mbali zinazungumzia katika sera za kuwawezesha wananchi wao kimitaji ili kuwekeza katika soko hili.

Je, kwetu sisi Zanzibar na kwa sababu serikali ipo hapa kwa kupitia Dk. Mwinyihaji Waziri wa Fedha, anaweza na yeye akatueleza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetuandaa vipi Wazanzibari, ama imewaandaa vipi wafanyabiashara wa Zanzibar katika kuwawezesha, hususan katika suala la mikopo ili na wao waweze ku-*compete* katika biashara hii ya Afrika ya Mashariki.

Swali la tano Mhe. Spika, katika ukurasa huu wa tatu kwenye kitabu chake Mhe. Waziri ametuambia kwamba kuna bidhaa zenye thamani ya Shs. 29,744,000, zilisafirishwa na kuuzwa nje. Naomba Mhe. Waziri atuambie kwa faida yetu na kwa faida ya wananchi, ili tupate tuelewe ni kiasi gani na sisi katika hiyo hatua ndogo basi ni bidhaa gani ambazo na sisi tumetoa.

La mwisho kabisa. Mhe. Spika, katika miaka ya hivi karibuni Zanzibar ilikuwa inafanya biashara nzuri sana na nchi ya Comoro. Biashara baina ya Zanzibar na Comoro ilikuwa ni kubwa sana na ni pahala pekee ukiwacha mbali sehemu ya Tanzania Bara, Kenya na nchi nyengine. Sasa lakini kwa kiasi fulani naona biashara ile baina ya Zanzibar na Comoro kwa kweli imefifia.

Je, serikali haioni umuhimu wa kuandaa mazingira maalumu ya kurejesha biashara baina ya Zanzibar na Comoro. Mhe Spika, mchango wangu huu umeishia hapa, ambao umekuja kwa mfumo wa maswali. Naomba nikushukuru na naomba nimpongeze waziri kwa mara ya pili. Lakini naomba niishie kwa kuunga mkono hoja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia machache sana katika hotuba ya Mhe. Waziri. Kwanza nimpongeze sana kwa jitihada anayoifanya kuendeleza hii wizara na kwa namna anavyojitahidi.

Pia niwapongeze sana watendaji wake Katibu Mkuu, msaidizi wake na mkurugenzi pamoja na Afisa Mdhamini Pemba kwa namna wanavyojitahidi katika hali ngumu sana, ili kuona kwamba majukumu waliyojipangia katika wizara yake yanakwenda vizuri. Naomba apokee sana pongezi zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando.

Mhe. Spika, mimi naomba nianze na ukurasa wa 78, kuna *organization chart* ya wizara. Katika *organization chart* ile naomba niulize maswali na nishauri kitu chengine kimoja. Kwanza chini ya MTTI. Labda ni Ministry Trade Tourism and Investment. Pale kuna mashirika manne. Kuna *ZSTC*, kuna *Zanzibar Institute for Tourism Development*, upande huu kuna *Zanzibar Commission for Tourism* na kuna *ZIPA*.

Lakini Mhe. Spika, sikuona pahala ambapo Shirika la Magari limewekwa pamoja na Shirika la Utalii wapi lipo. Sasa naomba kujua haya mashirika yapo katika eneo gani la wizara. Kwa hivyo, naomba kujibiwa hilo.

Pia ni vizuri afisi ya *Internal Audit* iwe chini ya *management* na zaidi Katibu Mkuu. Mhe. Spika, juzi nilipokuja hapa *organization chart* ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilionesha kwamba Afisi ya *Internal Audit* iko chini ya uangalizi wa Katibu Mkuu. Madhumuni makubwa ya kuiweka hapa ni kwamba huyu anakuwa na nafasi ya kupiga kengele, mfano kama ameona jambo lolote katika eneo lolote la wizara, kama kuna jambo ambalo linakwenda kinyume na udhibiti wa fedha na matumizi yake. sasa hakuna eneo ambalo katika *organization* hii Afisi ya *Internal Audit* imewekwa. Kwa hivyo, pia ningeomba jibu au kama halipo basi ningeshauri iwekwe hapa.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi naomba nianze na Shirika la ZSTC. Karibu kila mwaka huwa najaribu kuchangia kidogo katika suala hili. Mhe. Spika, tukiangalia *trend* ya ununuzi wa karafuu unapungua kila mwaka. Kwa nchi makini haiwezi kuangalia tu ikatumua macho kwamba kuna upungufu wa uzalishaji kila mwaka, lazima kuwe na mikakati inayoonekana kwamba tunageuza hiyo hali. Sasa haionekani isipokuwa tunachokiona ni kutoa miche. Sasa utoaji wa miche sio kuongeza uzalishaji wala kustawisha karafuu. Hapa Mhe. Spika, Mhe. Waziri ni lazima atuambie hasa kuna mpango gani, *vision* ya serikali na wizara yake kuhusiana na suala hili la ZSTC ni lazima tuipate.

Mwaka 2003/2004 aliyekuwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji wakati ule nakumbuka alikuwa Mhe. Moh'd Aboud, alituambia Baraza hili kwamba serikali ina mpango wa kulibinafsisha zao la karafuu. Imepita miaka hiyo hadi leo serikali inaonekana ina kigugumizi. Sasa sio vizuri serikali kuahidi Baraza na halafu inaonekana hakuna utekelezaji na tuliambiwa kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa na tukaambiwa kila kitu tayari.

Mhe. Spika, suala hili juzi tumeambiwa limekaliwa na Wizara ya Fedha na Uchumi, sasa kama ni kweli basi ni vizuri tukaambiwa kinaga ubaga nini hasa kilichomo kwenye suala hili. Kwa hivyo, lazima tufike pahala *ZSTC* imegeuzwa kuwa Mamlaka ya Karafuu Zanzibar na kuendelea kuwa shirika ni tatizo kubwa kwa maoni yangu.

Suala jengine ni kuhusu bajeti ndogo ya Kamisheni ya Utalii. Kwa kweli kama tunakusudia hasa kama Utalii ndio Sekta Kiongozi, basi huwezi kuipangia Kamisheni ya Utalii bajeti ile kwani haiwezi kufanya kitu. Matokeo yake kila siku itakuwa inapiga mbio hapa penuni, lakini haiwezi kufanya *Promotion* ya Utalii katika masoko.

Kwa hivyo, sioni sababu labda Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze tatizo nini kuifanya Kamisheni ya Utalii kuifunga mikono kiasi hiki, kwa kweli haiwezi kufanyakazi katika hali iliyonayo.

Mhe. Spika, bajeti ile ambayo Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin Waziri Kivuli wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji), asilimia ile ni ndogo na wala hatuonekani kama tuko makini kwenye suala hili. Kwa hiyo, naomba jibu katika suala hilo.

Lakini eneo jengine ambalo kama sikupata maelezo mazuri nakusudia kuzuia shilingi ni Idara ya Viwanda. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anatuomba tuidhinishe shilingi milioni 72 kwa ajili ya shughuli za Idara ya Viwanda. Sasa bajeti hii inaonesha nia ya wizara yake kutokuwa tayari kuona kwamba Zanzibar inakuwa na viwanda vya uzalishaji.

Hizi shilingi 72 milioni kwa kweli zitufanye nini katika masuala ya *Promotion* ya *Industrial Manufacturing*. Nadhani hakuna nia, labda tumeweka watu wapate riziki zao za mishahara au vyenginevyo sawa. Lakini kama wafanyekazi kwa lengo la kuisaidia Zanzibar hapa naona hakuna jambo la maana hata kidogo. Kutokana na hali hiyo, naomba maelezo kwa nini zikatengwa kiasi hicho kidogo.

Pamoja na hayo, Mhe. Spika kwa kweli tunayo hali ngumu sana hata Kiwanda cha Mshumaha, hii ni aibu kubwa tukiachia mbali Kiwanda cha *Biscuit* na

mambo mengine. Kwa mfano, siku hizi kwenye hitima watu wameacha kula visheti na mambo mengine, isipokuwa wamejikita sana kwenye *biscuit*, kwa sababu wanawake labda hawana muda wa kushughulikia mambo. Sasa hata ku-*promote* uzalishaji wa *biscuit* hapa Zanzibar tunalo tatizo kubwa.

Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Waziri bado hajawa tayari na uzalishaji wa ndani. Kwa kweli nilishawahi kusema kwenye bajeti hizi, kwamba Singapore ilipoona uchumi wake unayumba basi waliweka sera madhubuti ya uzalishaji viwandani.

Hata hivyo, Singapore ni nchi ndogo sana kuliko Zanzibar, yaani Pemba ni kubwa karibu mara mbili kuliko Singapore, lakini wao walikusudia kuzalisha viwandani na kweli wamezalisha na uchumi wao umekua mkubwa. Sasa sisi tunaambiwa viwanda vikubwa haviwezekani imekuwaje Singapore inawezekana nchi ndogo kuliko yetu sisi na tunasema haiwezekani au vipi.

Mhe. Spika, nadhani kuna tatizo la sera na kama kuna tatizo hilo basi Mhe. Waziri atuambie tufanye nini ili tuweze kubadilisha sera, hatimaye Zanzibar iwe ni eneo la uzalishaji wa viwandani, kwa ajili ya kupata ajira ya watu wetu pamoja na kuuza nje.

Kutokana na hali hiyo, hatuwezi kuendelea kuwa *recipient* wa bidhaa kutoka nje, wakati mwengine bidhaa nyengine hazina kiwango inakuwa ni mtihani mkubwa. Hivi kweli hata Kiwanda cha Mshumaha, kwa sababu tulikuwa na tatizo la umeme hapa.
Kwa kweli hili ni tatizo ambalo Mhe. Spika serikali kupitia Mhe. Waziri alieleze Baraza hili mikakati ambayo ameiweka.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, katika ukurasa wa 73 Orodha ya Viwanda Vidogo na Kati vilivyotembelewa ukiviangalia viwanda vyenyewe ni mtihani mkubwa. Kwa mfano, kuna *Hafidh Traders* Viwanda vya Matofali, basi Mhe. Waziri anatuambia anavyo viwanda vya matofali au Viwanda vya Tambi, Viwanda vya Viatu vya Makubadhi vilioko Tumbe, yaani ukienda kutizama hicho kiwanda, nadhani tumefanya mas-hara.

Vile vile visusu na vikapu *are we serious* Mhe. Spika, yaani pale baharini kuna mtu anafanya visusu vya muwale navyo ni viwanda. Kwa kweli nafikiri tusifanye mas-hara katika suala hili au pale Msuka kuna vijana wanafanya mikoba na mikeka navyo ni viwanda. Mhe. Spika, nadhani kuna mambo mengine bora tusiyaingize kwenye vitabu vya bajeti, kwa sababu hivi vinasomwa na watu wengi na watatudharau.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilizungumze kidogo ni kuhusu Jumuia ya Afrika ya Mashariki. Kwa kweli lazima serikali iwe makini sana juu ya suala hili, vyenginevyo hadhi ya Zanzibar itakuwa inapungua kidogo kidogo na tukitahamaki ile dhana ya wengine ya serikali mbili kuelekea moja *this is the gateway* ninavyoiona mimi.

Kwa hiyo, hatuonekani Zanzibar tunaoudhibiti wa suala hili, nilikuwa nikiangalia je labda Mhe. Waziri anaweza kutueleza uanzishwaji wa hili linaloitwa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kwa hali ya Zanzibar ilivyo, ama kuna mazungumzo ya kuanzisha *Common Currency*.

Sasa tukiendelea sisi huku tunao mgogoro na wenzetu kuhusiana na suala letu la kero la *East Africa Currency Board* bado hatujapata ufumbuzi tunaingizwa kwenye sarafu moja. Mhe. Spika, sisi itakuwa *portion* yetu ipi, lakini baya zaidi kuna mazungumzo ya *East African Federation*. Kwa kweli tunapata giza Mhe. Spika, Zanzibar inawekwa kwenye *angle* ipi katika suala hili. Hivi *East African Federation* Zanzibar itaingia kama nchi au bado tutaburuzwa kwenye mgongo wa Tanganyika.

Kwa hivyo, mambo haya kama Mhe. Waziri amejipa jukumu la kusimamia masuala ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki, basi awe na majibu maridhawa ambayo sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi tuweze kuwajibu wananchi. Lakini kuendelea kama ilivyo nadhani hatuwezi kunyamaza na tunapata wasi wasi mkubwa wapi Zanzibar inakwenda.

Kwa maana hiyo, tunataka majibu maridhawa, kwa sababu yeye ndiye amejipa jukumu hilo, ili wananchi wakituuliza basi tuwajibu Zanzibar katika *East Africa Federation* iko pahala gani.

Mhe. Spika, katika ukurasa 9 Mhe. Waziri anasema kuangalia uwezekano wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengevu la uchumi. Kwa kweli jambo hili ni zuri, lakini sijui uwezekano huu tunauangalia kwa nani na tunauomba kwa nini, ni jambo la kutupa jibu, kwa sababu ikifika pahala kama sisi wenyewe hatuna mamlaka kama iwe ni sehemu ya *Special Economic Zone*.

Nadhani hapo tunalo tatizo ndipo pale Mhe. Waziri Kivuli alipozungumza kwamba kaka zetu au wenzetu wa Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda wao walikuwa hawana tatizo na Zanzibar kuwa *Special Economic Zone*. Lakini kaka zetu wa damu, wapenzi wazuri, wao ndio waliotoa *objection* na kama hilo ni kweli Mhe. Spika, basi tunalo tatizo kubwa. Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kutujibu suala hili kama ni kweli basi tujue tunaondoka na hali gani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu *ZIPA*. Kwa kweli nimesikitishwa namna *ZIPA* inavyofanyakazi na hasa kutokuwa na uwezo wa *One Stop Center* kama tulivyokubalina, kwa sababu tulikubaliana kwamba *ZIPA* iwe *One Stop Center*. Kwa hivyo, ikiwa mpaka leo kama suala hili bado tokea *ZIPA* tulipoiunda hapa na tukavunja zile taasisi nyengine na kuifanya iwe moja, kwa ajili ya kutusaidia mambo yetu, basi kama hili halijawezekana. Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo linanipa mashaka sana.

Mhe. Waziri Kivuli alizungumza kuhusu Kiwanda cha Maji kule Pemba ambacho mpaka leo bado hakijapata Hati Miliki. Kwa kweli hili ni tatizo la kwamba *One Stop Center* katika *ZIPA* haikuwezekana, kwa sababu wanaotoa Hati Miliki ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na mtu wao ambaye yupo pale twabaani atapelekwa mtu wa chini ambaye hana maamuzi. Kutokana na hali hii, *ZIPA* tuseme imeshindwa, kwa sababu kama inaidhinisha miradi kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, wale vijana walinijia na kuniambia kweli wanasikitika na hii hali na wao walikuwa watu wengi kwa ajili ya kuanzisha kiwanda. Kwa hivyo, kutokana na kukaa kwa muda mrefu hawajapata Hati Miliki wameamua kila mmoja kugawana walichonacho na wamebakia kidogo ambao wanaendelea kusubiri.

Kwa hiyo, isifike pahala utaratibu huu wa *ZIPA* ukakwamisha maendeleo ya wananchi na hili si jambo zuri hata kidogo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umemalizika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimalize kwa kukipongeza Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kwa shughuli zao wanazozifanya. Kwa kweli wanafanyakazi ngumu katika hali ngumu ambapo fedha kidogo, hata hivyo wanajitahidi na waendelea kupokea pongezi zangu na waendelee kucheza japo gamba gumu ndio hali ya mambo.

Pamoja na hayo, nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jitihada wanayofanya na akinijibu vizuri basi nitaunga mkono hoja.

Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Kwanza awali ya yote nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa juhudi pamoja na kazi nzuri, ambazo wanazifanya katika wizara hii.

Kweli Waswahili wanasema “kinamama wakiwezeshwa wanaweza”. Mhe. Spika, nampongeza Waziri kwa kukaa muda mrefu katika wizara hii na jinsi anavyozitekeleza kazi zake kwa mujibu wa utaratibu. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya katika kipindi chote ambacho anaiongoza wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 15 kuhusu Sekta ya Utalii, yaani kuwepo kwa Sekta ya Utalii ni jambo muhimu sana katika wizara hii. Kwa kweli kama inavyofahamika kwamba baadhi ya nchi huwa zinaendeshwa na Sekta hii ya Utalii, pindipo ikiimarishwa vizuri inakuwa ni mchango mkubwa katika nchi.

Kwa hviyo, nimpongeze Mhe. Waziri anajitahdi sana katika sekta hii kwa kuihamasisha na kuipangia mipango mbali mbali, kwa ajili ya kupata matumaini na kuwa kivutio kwa wageni pamoja watalii kutoka nchi tofauti kuja hapa nchini kwetu.

Kwa maana hiyo, namshukuru kwa juhudi yake, isipokuwa jambo la msingi wazidishe mikakati zaidi, kwa sababu kama inavyofahamika nchi yetu inapendwa na wageni au watalii wengi kuja kutembelea hapa visiwani. Kwa hivyo, naomba wazidishe mikakati kwa ajili ya kuimarisha sekta hii katika uzalishaji na kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ingawa kuna vitengo vyengine ndani ya wizara yake vinavyohusu biashara, uwekezaji, lakini kwa sasa imepewa kipaumbele Sekta ya Utalii kwa kushirikiana na kilimo, kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi yetu.

Nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 48 kuhusu Sekta ya Viwanda. Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda hujumuisha zaidi Viwanda Vidogo Vidogo vya Kati vinavyomilikiwa na watu binafsi. Kwa kweli kama tunavyofahamu kwamba faida ya kuwa na viwanda katika nchi ni kubwa sana. Kwa mfano, ndugu zetu ama vijana wetu wanapata ajira kwa ajili ya kuweza kujikimu kimaisha.

Mhe. Spika, tatizo kubwa la viwanda na hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wanapotaka kuja wawekezaji kuwekeza kwa ajili ya viwanda, kwa kuwa mji wetu mdogo na tunayo maeneo makubwa ya uwanda. Kwa hiyo, ni vyema kuwapatia sehemu hizo za uwanda, kwa sababu kujenga viwanda ndani ya miji nadhani itakuwa mtihani.

Nadhani kuna kipindi fulani India kulikuwa na kiwanda karibu na mji. Sasa baada ya kutokea matatizo ya gesi kwenye kiwanda kile ambayo iliathiri binadamu katika maeneo yale. Kwa hivyo, hivi sasa kuna haja wakati

wanapokuja wawekezaji ni vizuri kupewa maeneo ya uwanda, kwani hayaoti vipando vya aina tofauti pamoja na kuwa mbali na makaazi ya wananchi.

Kwa mfano, hivi sasa mji wetu umekua na katika maeneo ya Mombasa kuna kiwanda ambacho kinaitwa *Zanzibar Kool*, kiwanda hiki kimezungukwa na majumba. Kwa hiyo, inaweza kuwa ni mashaka baada ya kutokea matatizo yoyote, ingawa cha maji hakina matatizo sana. Lakini baadhi ya viwanda kujengwa kama mule kwa hivi sasa inaweza kuwa mtihani.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, hawa wanaokuja kuwekeza katika masuala ya viwanda, hivi sasa zaidi waelekezwe kwenye maeneo yetu ya uwanda, kwa ajili ya kuepusha matatizo ambayo yanaweza kutokezea.

Vile vile kuhusu suala la kuzidisha kasi kwa Wawekezaji wa Viwanda vya Vyakula. Kwa mfano, kama ilivyoelezwa hapa *juice*, maji na mambo mengine. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuangalia zaidi vile viwanda ambavyo uzalishaji wake ni mkubwa pamoja na nafasi za ajira na hata biashara yake inakuwa na wateja wengi.

Kwa mfano, Kiwanda vya Peremende. *Biscuit, Chocolate*, sasa hivi kama tutakuwa navyo nadhani vitasaidia sana kwa ajira za ndugu zetu, kwa sababu kwanza watumiaji wake wengine na utaona kama hii biashara ni ndogo tu, lakini zile tani za peremende, *biscuit* zinazoingia hapa ni nyingi sana. Kwa kweli bidhaa zile zinamouzwa utakuta wateja wake ni wengi, ambao ni watoto ndio wateja wakubwa lakini faida yake ni kubwa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili nalo aliangalie la kuwapata wawekezaji kama hawa na kuweza kushauriana pamoja na kuzungumza nao, nadhani vikiwepo viwanda kama hivi vinaweza kusaidia. Kwa mfano, nafasi za ajira zinaweza kuwa nyingi, kama kiwanda hiki kiwekwe kwenye uwanda wa kiasi meli kumi au kumi na tano.

Kwa hivyo, vijana wengi watapata ajira zikiwemo usafiri wa magari, akinamama lishe, yaani mbali ya ile bidhaa au biashara zitakazozalishwa na baadaye kupelekwa mitaani itakuwa imesaidia kwa kiwango kikubwa wananchi wetu kupunguza ukali wa maisha.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili akaliangalia sana kwa ajili ya kuweza kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi wetu.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 34 kwenye kifungu cha 6 kuhusu Sekta ya Biashara, imeundwa Idara ya Biashara na hiki ni chombo muhimu sana. Mhe.

Spika, kama inavyofahamika katika kipindi cha nyuma hapa palikuwa na biashara ambazo ni kubwa, yaani Awamu ya Tatu na likatoka tamko rasmi kubwa Biashara Huria zimeruhusiwa na kila mwenye biashara yake anakaribisha, “Zanzibar ni Njema Atakaye Aje”. Kwa kweli kipindi kile tulifaidika sana kutokana na ule mfumo mzuri uliokuwepo pamoja na biashara zilikua vizuri sana.

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba mfumo ule unaendelea au umekwisha. Kwa hiyo, atakapokuja kufanya majumuisho anieleze, ili nijue unaendelea au haupo tena.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ukurasa wa 26 kifungu 5 kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Kwa kweli kuna haja ya kukiimarisha zaidi chuo hiki, kwa sababu kuwa na chuo hiki ni muhimu sana kama walivyosema wenzangu. Chuo hiki kinawapatia taaluma ndugu pamoja na vijana wetu kuhusiana na masuala ya utalii na kupata wataalamu, ili kuweza kuimarisha Sekta ya Utalii kwa lengo la kupata neema zaidi katika nchi yetu.

Pamoja na hayo, jambo kubwa ambalo ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuwa ashirikiane zaidi na watu wa utamaduni katika kusomesha kwenye chuo hiki na kuweza kuonesha yale mambo ya utamaduni katika nchi yetu.

Kwa mfano, kwenye kipeperushi ambacho kuna mama amekaa juu ya kobe na amejitanda kanga, kwa kweli picha ile inapendeza au Mzanzibari ukimuona amevaa baibui la kiasili. Sasa hali kama ile inavutia sana kwa watu au wageni tofauti wanaokuja katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri katika usomeshaji wa chuo hiki ajaribu sana kutoa taaluma za masuala ya utamaduni, ili kupata kivutio kwa wageni wetu wanaokuja nchini hapa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii ya kuchangia wizara ya swahiba wangu mkubwa ambayo ni Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa kutusomea hotuba hii kwa muda mfupi sana na

yale mambo muhimu hakuyasahau kuyataja na hivyo kutufanyia kazi rahisi ya kuweza kuchangia.

Aidha nawapongeza sana wafanyakazi wote wa wizara hii kwa majukumu makubwa waliyotwikwa na jinsi wanavyoziendsha.

Mhe. Spika, nataka nifahamishwe kwa sababu Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ni muhimu sana katika nchi kama ya Zanzibar. Zanzibar ni kisiwa na tuna-*deal* na uchumi wa kisiwa, kwani ardhi yetu ni ndogo na tumezungukwa na bahari. Kwa hivyo, sisi kazi yetu ni biashara katika kutoa huduma.

Sasa kama wizara hii ndio muhimu sana kulinganisha wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa bahati mbaya suala hili halifahamiki na wala halipewi uzito unaostahiki. Kwa kweli wizara hii inaweza kuzalisha na kutoa mapato ya zaidi ya asilimia 70 ya nchi hii. Kutokana na umuhimu wake wizara hii na pia ni wizara ambayo inahitajika kupewa kila aina ya kipaumbele. Lakini jambo la kusikitisha ni wizara ya mwisho ambayo imetupwa kabisa na wala haipewi thamani yake inayostahiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huwezi kwenda baharini na kutaka kuvua nyangumi kwa mshipi wa kawaida na kidau na wala huwezi kwenda kuvua papa kwa chambo cha kuvua changu. Kwa mfano, Wajapani wanakwenda kuvua nyangumi ambacho ni kitoweo chao kikubwa na chenye thamani kubwa, wanakuwa na meli maalum za kuvulia nyangumi, zana nzito pamoja na watu wenye ujuzi wa hali ya juu. Kwa hivyo, huwezi kutia chambo cha kibua na kwenda kuvua nguru na wala haiwezekani.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, ili serikali iweze kufahamu umuhimu au matunda ya wizara, basi ni vyema wizara hii iwezeshwe ipasavyo. Kwa kweli wizara hii kwa muda wote wa miaka kumi ambayo ninayoiona biashara imeshuka kwa kiwango kikubwa sana, viwanda havikui na *ZIPA* huduma zake za chini kabisa.

Kwa hivyo, hilo sioni ajabu na wala simlaumu Mhe. Waziri na hata wafanyakazi wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, isipokuwa nailaumu serikali nzima kwamba imeshindwa kutambua umuhimu wa wizara hii.

Mhe. Spika, huwezi kuwaambia *ZIPA* leo kwa mwaka mzima wafanyekazi ya kuleta hapa matajiri kwa ajili ya kuja kuwekeza kwa bajeti ya shilingi milioni 300 haiwezekani. Kwa kweli shilingi milioni 300 ni hoteli au kampuni ndogo ndio itakuwa na bajeti ya shilingi milioni 300, lakini si kwa *ZIPA*.

Vile vile kwa upande wa Idara ya Viwanda shilingi milioni 72 haiwezekani kabisa, pia Kamisheni ya Utalii shilingi milioni 37 haiwezekani. Kwa mfano, tukiangalia Malaysia kuna *incredible* India wanatangaza katika *CNN* pia Indonesia na wao wanatangaza. Kwa kweli tangazo moja katika *CNN* linafika dola milioni moja, lakini sisi kweli tunatangaza utalii kwa shilingi milioni 37, nafikiri tunafanya mas-hara na kwa hali hii hatufahamu kabisa kama Utalii ndio Sekta Kiongozi, yaani haiwezekani.

Mhe. Spika, nasema kwamba kama kweli *we are very serious* na tunataka tuvue samaki mnene ambaye mwenye mnofu, basi lazima tutie chambo madhubuti chenye thamani kubwa, mshipi madhubuti pamoja na chombo madhubuti kwa ajili ya kuvulia, basi nina hakika tutavua na Zanzibar itaondokana na umasikini mara moja.

Kwa mfano, Dubai hawana mafuta, isipokuwa wanaendesha biashara zao ndizo zinazoendsha uchumi wao *recession* iliyotokea Dubai imeyumba sana. Lakini wanasema hata ikiyumba hivi kwa muda wa miaka 20 maendeleo Dubai wameshapata, yaani hapa wakae kitako tu basi maendeleo yanakidhi haja. Kwa mfano, hospitali, viwanda pamoja na huduma nyengine mbali mbali *with high technology*, kwa hivyo naamini kwamba wako *very much at advance.*

Kwa hivyo, wizara hii lazima ipewe nafasi yake katika serikali yetu. Mhe. Spika, tunakokwenda mbele wizara hii inakosa kitu kimoja ambacho ni muhimu sana ni Idara ya Ushirikiano. Kwa kweli wizara hii haiwezi kufanyakazi zake kama haikuweza kushirikiana na wizara zote na ndio maana kule *ZIPA One Stop Center* ikashindikana, kwa sababu bado mawizara yote haya hawajaamini na wala haijatambua Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ndio Wizara Kiongozi (Mama), yaani wizara zote.

Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Masuala ya nje na ndani ya Muungano, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, yaani wizara zote zifanyekazi bega kwa bega na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, lakini bado haijatambua suala hilo. Kwa hiyo, Zanzibar itaendelea kuwa masikini tu.

Mhe. Spika, mkombozi wa Zanzibar na wala tusidanganyane nchi yetu ni visiwa na visiwa ni *services* au *trade* na wala si chengine na kama hatuna ndoto nyengine za madini na mambo mengine ya kutoa chini ya ardhi ni biashara na huduma. Kwa hivyo, tukishindwa kujua umuhimu wake, basi Wizara hii ya Utalii, Biashara na Uwekezaji itashindwa kufanyakazi zake na kwa hali hiyo tunaidhoofisha nchi pamoja na sisi wenyewe.

Sasa kama tunataka kuleta maendeleo katika nchi hii Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ipewe bajeti kubwa kabisa, ili watu waweze kufanyakazi tena wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu wawekwe katika wizara hii kwa ajili ya kufanyakazi na wizara yetu ipate kufanyakazi vizuri na kuleta matarajio mazuri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea baada ya kusisitiza hayo ninamuomba Mhe. Waziri anifahamishe kidogo kwenye ukurasa wa 4 wa kitabu cha Mhe. Waziri anaeleza kwamba kuna ajira ya watu wasiopungua 50,000 ambao wameajiriwa katika Sekta ya Utalii.

Kwa kweli hii inapingana moja kwa moja na Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, katika ukurasa wa 35 Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 35 kuhusu Ajira Rasmi Nchini inasema hivi:-

> "Mhe. Spika, idadi ya waajiriwa imekuwa ikiongezeka ndani ya Sekta ya Umma na ile Binafsi, ambapo idadi ya waajiriwa imefikia watu 47,551 mwaka 2009 kutoka waajiriwa 41,608 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 13.7.
>
> Kati ya waajiriwa hawa jumla ya wafanyakazi 31,378 sawa na asilimia 75.5 wamo katika Sekta ya Umma, ambapo asilimia 40.0 kati yao wamo katika Sekta ya Elimu. Aidha wafanyakazi wa Sekta Binafsi wamefikia jumla ya 10,230 sawa na asilimia 24.5 ya waajiriwa wote. Kati ya hao asilimia 12.8 wafanyakazi katika shughuli mbali mbali katika Sekta ya Utalii".

Kwa hivyo, hii inapingana moja kwa moja na *speech* ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha. Mhe. Spika, naomba nipate ufafanuzi, kwa sababu takwimu hizi ikiwa haioani zinatuletea matatizo katika ukusanyaji wa hizi taarifa.

Mhe. Spika, nikizungumzia suala la viwanda sisi Zanzibar ni kisiwa ambacho kina bahati kubwa sana kwa sababu tuko masafa mafupi tu kutoka Bara la Afika, Mauritius wanalia sana kwamba wao wako mbali sana na Bara la Afrika, yaani hawako India wala Afrika.

Kwa hivyo, wangeomba sana wapate hii *advantage* ya kuwa karibu na Bara la Afrika, lakini sisi tunayo *geographical advantage* ambayo mpaka sasa tumeshindwa kuitumia. Kwa kweli *geographical advantage* hii ingetusaidia

sana kama tungewezakuitumia sisi kwenye Muungano wetu wa Tanzania, Muungano wa *East Africa Community* na hata Muungano wa *SADC*.

Lakini tumeshindwa hata kuutumia huu Muungano wa Tanzania, kwa sababu fursa hii tungeitumia vizuri, baada ya sisi kulia kuhusu kero za Muungano, basi Tanzania Bara wangelia kuhusu kero za Muungano, sasa tumeshindwa kutumia fursa hiyo na tunanung'unika sisi, wao ndio walikuwa wanung'unike.

Kwa hivyo, tutumie fursa hii ya *geographical* kwa ajili ya kujenga uchumi wa Zanzibar. Kwa mfano, Singapore *raw materials* zinatoka Malaysia na viwanda vya kufanya *process* viko Singapore. Kwa hivyo hakuna tatizo mali kutoka Tanzania Bara vikawa *process* in Zanzibar na zikauzwa nje, tukatumia ile fursa ya muungano. Tunashindwa kutumia fursa za muungano tunapiga kelele.

Mhe. Spika, viwanda ni suala muhimu sana katika suala hili la Masoko ya Afrika Mashariki na Masoko ya SADC. Mhe. Waziri kaorodhesha viwanda 31 katika *list* yake, viwanda vyenyewe ni vidogo vidogo. Sisi wafanyabiasha tunasema hivi ni viwanda na viwanda vyote vinaanza udogo vikenda kukubwa. Mfano kiwanda cha tambi, kwenye tambi sasa hivi wanaanika tambi nje hawa-*pack.*
Mhe. Abdalla Mwinyi anakumbuka zamani sisi tulivyokuwa wadogo tulikuwa tunaona kuna tambi katika *packet* kabila lake nishazisahau ni nzuri sana.
Sasa wale hivi ni kuboresha bidhaa zenu ziweze kuanikwa katika mtambo na ziweze kuwa *packed* katika *very good packing* na ziwe na *expire date* baada ya kutia katika vipolo tambi mbichi zikatoka Dar-es-Salaam, acheni mtindo huu fanyeni mtindo huu na huu hizo ndio *systerm* za kufanya sio unatoa tambi zinatoka moshi, fangus. Kule china kwenye mashine za tambi kunamtambo mzima wa kukausha tambi ambao tambi zikishakutolewa inakaushwa halafu inakuwa *packed* na inatiwa *expire date* na kila kitu. Mtambo wenyewe wote huo ni dola elfu 35. Kwa hivyo nahisi kwamba wafanyabiashara wanao uwezo huo lakini elimu hawana. Kwa hivyo Wizara ya Biashara inajukumu kubwa sana la kuweza kuwasomesha watoto wetu.

Bekari hiyo unayoidharau weye kila mwaka mimi napata karatasi napata keki ya Krismas inatoka Marekani inakuja Unguja, napata keki nyengine inatoka Italiy, zinakuwa *exported* dunia nzima. Utashangaa keki imeshakaa mwezi mmoja lakini bado inafika Zanzibar na unaila ni *first class.* Vitu vyote hivi ni viwanda na kwa kweli vinatakiwa vifanyiwe kazi kubwa. Wizara ya Biashara ikuze viwanda, viwanda ni vidogo, wananchi wamejitolea kufanya vyungu, vikapu, sawa. Sasa ni kazi ya serikali kuweza kuwashajihisha hawa na kuwasaidia kuwasukuma kuja juu zaidi na kuweza kutoa bidhaa hizo.

Mfano Omani na Saudia kule ukinunua tende imo katika kikapu. Vile vikapu vinafanywa katika viwanda vidogo vidogo. Hivyo vikapu ni *very good packing, local packing* ya kupeleka nchi za nje. Akija mtalii hapa akaona karafuu imekuwa *packed* katika ungo anaithamini zaidi kuliko katika *plastic bag*. Kwa hivyo nasema kwamba viwanda vimeshaanzishwa hivi ni vidogo lakini Wizara ya Biashara imeshindwa kuweza kuviendeleza viwanda hivi na imeshindwa kwa sababu bajeti yake ni ndogo sana. Naomba mwaka unaokuja serikali ione umuhimu wa bajeti hii.

Mhe. Spika, suala la maonesho ya biashara. Maonesho ya biashara ni suala muhimu sana, wasi wasi wangu mimi kwamba tulianzisha hapa Mwanakwerekwe palianzishwa maonesho ya biashara. Baadaye Wizara ya Biashara imeshindwa kuyachukua majumba yale yakawa maskuli na mambo mengine. Kule Tunguu tumefanya kazi *day and night* baada ya kwisha kujenga Wizara ya Elimu imechukua kwa sababu Wizara ya Biashara imeshindwa kuyaendeleza. Wasi wasi wangu na huko vile vile hata wakafanya haiwezekani kwa hivyo mimi ninachoomba Wizara hii ione kama uko umuhimu wa kufanya shirika, shirika liwe *registered*, sheria itungwe ili liwe linashuhulika na lile suala, litakuwa *answerable* kuliko wizara kuchukua lile eneo likawa ni lake yeye pakanyang'anywa kama eneo la Tunguu na eneo la Mwanakwerekwe. Liundwe Shirika liwe *registered* liwe katika sheria, linashtakiwa halipokonyeki, linafanya kazi zake nafikiri hapo ndio tutaweza kufanya suala hilo.
Mhe. Spika, naamini kabisa ile sera ya kuweza kufanya hapa hiyo Zanzibar kuwa ni sehemu ya f*ree zone* katika SADC na katika Afrika Mashariki ni *very viable* lakini ni suala linalotaka lifanyiwe kwa haraka kwa sababu biashara ni *time*, ukikosea *time* biashara umo katika mashaka makubwa sana.

Kwa hivyo nasisitiza kwamba suala hili liwekewe mkazo kabisa tuweze kuona kwamba inafanywa kwa haraka sana kwa sababu biashara ni muda, muda ukipotea mwenzako anawahi, akiwahi umeshapigwa bao umekwisha. Biashara ni kushindana ukikosa wewe mwenzako anachukua umepigwa bao kwa hivyo ufanye jitihada lipatikane suala hilo.

Vile vile suala la viwanda nasisitiza tena sasa hivi Serikali ya China ndio ambayo kwamba inatisha kwa viwanda katika dunia yetu. Lakini kwa bahati mbaya katika miaka miwili iliyofuatia au mitatu China itaanguka katika biashara ya *manufacturing.* Kwa sababu inakazaniwa sana sasa hivi na ulimwengu mzima kama Marekani na Wenzake, wanasindikiza China ipunguze thamani ya fedha zako. Kutoka na hali hiyo vitu china vitakuwa ghali na wafanyakazi itabidi walipwe mishahara mikubwa. Kwa hali hiyo *this is an opportunity* ya nchi hizi masikini kuweza ku- *penetrate* katika masuala ya

manufacturing kwa sababu *China within short time* uchumi wake utaanguka kutokana na hiyo *strategy* ya haya.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii kuichangia Bajeti hii ya Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. Sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kufanya kazi zao vizuri.

Nitaanzia na Idara ya Sera na Mipango, Kwa kweli Idara ya Sera na Mipango ameipanga vizuri na utekelezaji wake umekwenda kwenye hali ya kawaida isipokuwa kidogo tu kuna mapungufu mawili matatu kwenye Chuo cha Utalii. Chuo cha Utalii kinasomesha vizuri, tunatoa wanafunzi wa stashahada na shahada. Hao wawekezaji wanapokuja hapa kufanya uwekezaji wa Mahoteli namuomba Mhe. Waziri tuwawekee mkataba Nam. 1 kabla hawajafanya chochote tena tusaini.

Mhe. Spika, tatizo la ajira ni tatizo sugu kwa sisi tunaoishi hapa. Madhali wale wana cheti na wapo *qualified* kwanza kila hoteli lazima tuwawekee wachukue watu 15 wenye sifa ambazo wao wanahitaji, wakisha ndio watafanya mambo yao ya *interview* ya kuchukua watu wengine. Nahisi tukifanya hivi hili la malalamiko ya ajira litaondoka. Itakuwa ndiyo tayari tumeshafunga nao mkataba, watu wenye sifa tunao na sisi tunatafuta ajira. Kisiwa chetu kidogo kwa hiyo pale tumeshawawekea *comment* watu 15 kama *house keeping, waiter* na wangine watoke katika hao watu 15 pamoja na kuwa vyeti vyao wanavyo tayari na hao wasiwe kwenye *interview*. Hayo ndio masharti yetu tuyaweke ya uzalendo katika mikataba yetu.

Sekta ya Biashara ukurasa wa 34. Hapa kidogo nitamgusa Mhe. Mazrui kuna tabia biashara inavamiwa, nchi ikivamiwa na biashara kama mwaka jana ilivamiwa Bombay sasa hivi imepigwa na chini hakuna biashara. Mara hii wamevamia china na huko chini kutapigwa na chini baadaye kuwa hakuna biashara. Mwaka ujao watavamia kwengine. Sisi tunashukuru sana kuwa tumeingia kwenye hii Jumuia ya Afrika Mashariki na Kati. Hii nafikiri itatusaidia sana katika kulinganisha baina ya nchi yetu na nyengine.

Halafu vile vile tuibe ujanja wa zile *items* ambazo wanazitegeneza, tukichukua ujuzi wao na wetu tukiweka pamoja zetu nafikiri zitakuwa nzuri zaidi, halafu pia tutabadilishana mawazo kwa biashara. Tunaangalia biashara zao na zetu tunabadilishana vipi tuboreshe. Nafikiri hii itatusaidia sana kuingiza halafu vile vile kubadilishana *items* na tutapata soko zuri na watu wetu hawa wanaofanya biashara watakuwa ni wafanyabiashara wazuri. Ukilinganisha bei za nje na

Afrika kwa Afrika inakuwa ni rahisi. Naona kama pesa yetu itazunguuka na tutakuwa katika hali nzuri.

Utekelezaji halisi, hawa wenye mahoteli nafikiri kwa makusudi mazima kama wanavyofanya wenzetu na baadhi ya hoteli tayari naona wameanza kuchukua vile vitu halisi ambavyo tunatengeneza tukaviweka mle kwenye vyumba. Chengine hivi vifurushi vya karafuu tungevifunga tukawakabidhi wenye mahoteli baada ya muda wao tutakuwa tunawauzia kwa bei yetu ambayo inatuhalisi na wao tena watafanya wenyewe. Wanawawekea wageni kwenye vyumba akiondoka mgeni ile lazima anakuwa ananunua kifurushi kile, kwa hivyo hoteli inakuwa inaingiza na sisi tunakuwa tunaingiza.

Vile vile tunaweza kutangaza biashara zetu kwa kupitia vipepeo vya ukili, vifuu vya kutilia majivu ya sigara, ile inakuwa ni *surprise* akija mgeni kuona kifuu ndio kinatiliwa majivu ya sigara. Nafikiri tukieneza kama hivyo kwenye vyumba tutapata vile vile na wajasiri amali nao kuwainua, wale wanaona kitu kigeni, hata hizi *dustbin* za kutilia taka watu wanafanya vizuri kwa ribin na oya zinapepea vizuri na mifuniko yake zinakaa vizuri zinawekewa kwenye vyumba na nyengine tunamuekea ya kununua. Akiondoka atanunua ili akaoneshe kwao kitu gani ambacho tunatengeneza, kama ribin na ng'ongo zinapishana, yapo mambo chungumzima yanafanywa.

Halafu chengine Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hawa wote wanaofanya hizi kazi za ujasiri amali nafikiri tungewajengea mabanda mazuri au kwa sasa hivi kama hatuna hali nzuri tungewafanyia kama vibanda vya Tigo, Zantel na mashirika mengine. Nafikiri wala sio ghali kwa mbao tu wanajenga halafu wanakuwekea madude yao yale wanakaa vizuri. Tunawapanga pale hawa hapa wanasuka ukili, hawa hapa wanafanya mikoba, hawa mabatiki, nafikiri itakuwa kivutio tosha. Kwanza zile rangi zilizopangika pale wale wanatangaza biashara yao na sisi tunatangaza biashara yetu.

Biashara na ujanja Mhe. Waziri lazima unakuwa mbunifu, ukishakuwa mbunifu kitu ambacho umekianza wakija pale wanaona tofauti. Wakiona tofauti wanakuwa wanapenda wanavutika kunako kijani tunawafanya wale wanaotia rangi za kijani, kunako blue, tunawafanya wale wanaotia rangi za blue, kunako nyekundu wale wanaotumia vitu vyekundu, kwa hiyo tunapata mabatiki, tunapata vitu mbali mbali, zile rangi zinakuwa zinapendeza kulingana na vile vibanda vyao ambavyo wameviweka pale. Nafikiri hapo tutafanikiwa vizuri, tena hii tunajenga hizi sehemu za mahoteli zile zinakuwa hazina ushuru mkubwa, ushuru wake unakuwa mdogo tu. Zile unawafata tu wale Zantel wanakupa taratibu zao kwa sababu na wao wanatangaza biashara kwa hivyo wanakuwa kwenye taratibu nzuri wanapendeza na kazi zao zinakuwa nzuri na wale watu wanavutika kwa zile rangi ambazo zimepangika pale.

Sekta ya Uwekezaji, nafikiri haya Maeneo Huru bado, tumetanga Maeneo Huru lakini bado tunabanwa banwa na hawa wenzetu wa Tanganyika. Kwa sababu Maeneo Huru ninavyojua miye na hata Mhe. Waziri mwenyewe anafahamu nchi zote zilizokuwa na Maeneo Huru, nchi nyingi nimetembea nimeona Maeneo Huru yanakuwaje yanakuwa ni huru. Lakini hili tusubiri uwanja wetu wa Airport umalizike ukishamalizika pale ndio tutapata ule ni uhuru wa kuingiza mambo mengi. Na tutaona zaidi hapo ambapo tutakapofungua hiyo Airport yetu. Hata mimi nitamsaidia kwa sababu hii biashara mimi kidogo naifahamu.

Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia na nampongeza Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi wa Magogoni, naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kushirikiana katika kutekeleza shughuli zetu na baada ya hapo basi naahirisha kikao hichi hadi kesho siku ya Jumatatu tarehe 5/07/2010 saa 3:00 za asubuhi.

(*Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 5/7/2010 saa 3:00 asubuhi)*